ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo La Kwamtipura.
10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.

23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.

34.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
41. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
44.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
45.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
46.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.
47.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.

48.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
59.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
52. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
53.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
56.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
58.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
59.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
60.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
61.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
62.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
63.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
64.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
65.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
66.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
67.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.

68.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
69.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
70.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
71.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
72.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
74.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
75.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
76.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Sita – Tarehe 22 Oktoba, 2009

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Kwa ruhusa yako naomba kutoa taarifa inayohusu kuwasili kwa Kombe la Dunia Zanzibar, Kombe linaloitwa *FIFA World CUP*. Kombe hili lilipangiwa kuwasili …

Mhe. Spika: Mheshimiwa unachotakiwa kusema hivi sasa ni kusema kwamba unatoa taarifa ya kuja kutoa hiyo kauli. Hivi sasa ni hati mezani tu, kwahivyo, hebu soma kama ilivyo *order paper* kwenye eneo lako hilo, yakariri maneno yaliyopo hapo.

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Samahani Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa ya kuwasili kwa Kombe la Dunia kwa ziara ya siku moja. naomba kuwasilisha.

Mhe. Najma Khalfan Juma (Waziri Kivuli Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo): Mhe. Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya upande wa upinzani kuhusu taarifa ya kuwasili Kombe la Dunia Zanzibar kwa ziara ya siku moja.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani ya hotuba kuhusu Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya na Kuweka Masharti ya Uzuiaji, Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya ya Nakotiki na Aina za Saikotropiki na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya na Kuweka Masharti ya Uzuiaji Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya ya Nakotiki na Aina za Saikotropiki na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Rashid Seif Suleiman (Waziri Kivuli Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani maombi ya Kambi ya Upinzani juu ya Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya na Kuweka Masharti ya Uzuiaji Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya ya Nakotiki na Aina za Saikotropiki na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii utufungulie darasa kidogo, haya mameno mengine si mepesi sana.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 53

Kuanzishwa kwa Mfuko wa Jimbo

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza:-

Bunge la Kenya wana mfuko unaoitwa (*CDF*) unaosaidia maendeleo kwa kasi sana katika majimbo na kuwapunguzia shida wananchi kwa muda mfupi. Baadhi ya Wajumbe wa Baraza wamefanya ziara huko Kenya na kupata taaluma ya mfuko huo. Aidha, Wabunge wa Kenya walikuja Zanzibar na wao kujifunza baadhi ya mambo. Bunge la Jamhuri ya Muungano tayari wamejifunza jambo hili na tunasikia katika bajeti yao ya 2009/2010 mfuko huo umeanzishwa.

a) Je, Mhe. Waziri suala hili serikali inalitambua ?

b) Kwa kuwa wenzetu Bunge la Jamhuri ya Muungano tayari wameanza. Je, na sisi serikali yetu ina mkakati gani juu ya jambo hilo ?

c) Je, Mhe. Waziri huoni na sisi tukichelewa kuanzisha suala hili Wawakilishi tutadhalilika katika majimbo ?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 53 lenye vifungu a, b na c kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, dhana ya kuwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo imeanza kupata umaarufu katika nchi za Afrika Mashariki. Kenya tayari imeanzisha Mfuko huo na imo katika utekelezaji wa Mfuko huo. Hivi karibuni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilianzisha Mfuko huo wa Maendeleo na wanahitaji utekelezaji wa shughuli hizo na tunataraji utekelezaji wa shughuli hizo za Mfuko zitaanza hivi karibuni.

Lengo la kuanzishwa kwa Mifuko ya aina hiyo, ni kusogeza shughuli za maendeleo karibu zaidi na wananchi ili kupunguza tofauti za mpishano wa viwango vya maendeleo na kusaidia mipango mikuu ya serikali katika kuleta maendeleo kwa wananchi wake wote.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kumjibu swali lake Mhe. Ali Abdalla Ali lenye vifungu a, b na c kama ifuataavyo:-

a) Mhe. Spika, serikali inatambua suala hilo.

b) Mkakati wa serikali yetu ni kutaka kuanzishwa kwa Mfuko huo kwa ajili ya kufikia lengo nililolieleza hapo juu na kuleta maendeleo kwa wananchi wote kupitia ngazi za chini na mamlaka ya nchi. Ili kupunguza tofauti za mipishano ya viwango vya maendeleo katika nchi yetu.

c) Mhe. Spika, napenda kumhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inajali sana wananchi wake na inajali maendeleo yao majimboni. Vile vile serikali haina nia ya kuwadhalilisha Waheshimiwa Wawakilishi majimboni mwao na ndio maana inafanya jitihada kubwa kadiri itakavyowezekana kusaidiana na Waheshimiwa katika kufikisha huduma kwa wananchi kwa kuwapatia huduma za aina mbali mbali. Huduma zenyewe zikiwemo afya, maji safi, umeme, elimu pamoja na kuwawezesha katika shughuli zao za kiuchumi, kuwapatia fursa za mikopo midogo midogo na mafunzo ya ujasiriamali.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. kwa kuwa Mhe. Waziri ni mmoja kati ya waliokwenda katika ziara hiyo pamoja na muulizaji wa swali la nyongeza, na kwa kuwa utaratibu wa Mfuko wa *CDF* yeye anaujua kwamba iko kamati itakayoundwa ya jimbo. Hivyo haoni Mhe. Waziri kucheleweshe *CDF* Zanzibar wakati *CDF* Tanzania Bara itakuwa imeshaanza? Haoni kama

patakuwa na tatizo la kupangua kamati ili kuona mfumo gani wa kamati uundwe ?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, tunaelewa kwamba Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo unakuwa unaundiwa kamati ya maendeleo katika jimbo lenyewe husika. Kuchelewa kwa sisi Zanzibar kuanzisha Mfuko huo haitapelekea mgongano, lakini bado naendelea kusema kwamba nawashauri Waheshimiwa Wawakilishi tushirikiane na Wabunge wetu katika majimbo yetu. Pindi lile fungu la fedha litakapoanza kuingizwa kwa upande wa Zanzibar, ni vizuri vile vikao tukavifanya kwa pamoja. Kwa sababu tukisema kwamba Mbunge aandae kamati yake maendeleo halafu na Mwakilishi kwa jimbo hilo hilo aje aandae kamati yake maendeleo hapa ndio tutasababisha huo mgongano. Lakini pamoja na kwamba sisi Zanzibar hatujawa tayari kuanzisha huo Mfuko, na hatujawa tayari kwa sababu tumo katika kujipanga tunaangalia changamoto zinazojitokeza katika Mfuko huu na tutaweza kumudu vipi ili tusije tukaanza tukasita njiani.

Kwa hivyo, ndio maana nikasema naomba sana Waheshimiwa, fedha hizi ni fedha za wananchi, kwa ajili ya maendeleo ya wananchi, sisi Zanzibar tuna bahati ya pekee katika jimbo. Tuna viongozi wawili Mbunge na Mwakilishi, cheo kimoja na kazi yao ndio hiyo hiyo. Kwa hivyo, ile kamati inatakiwa iwe kamati ya wananchi Mbunge na Mwakilishi wao watakuwa mmoja Mwenyekiti japo hatakuwa Mwakilishi kama Makamo Mwenyekiti, lakini hata anapokuwa Mbunge hayupo Mwakilishi atakuwa anasimamia utekelezaji na matumizi ya fedha zile. Kwa hivyo, bado ninaendelea kuwaomba tena, hata sisi Zanzibar tukija tukianzisha huo Mfuko bado tutapendelea kwamba kamati iwe hiyo hiyo kwa sababu maendeleo yatakuwa ndio ya watu hao hao.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, *CDF* ambao ni Mfuko utaosaidia maendeleo katika jimbo una muundo wake na sheria uliowekewa. Katika wajumbe ambao wametajwa katika sheria hiyo Mbunge mwenyewe, Afisa Tawala wa Wilaya, Madiwani wawili, Masheha wawili kwa hapa Zanzibar, Mwakilishi hakuguswa sehemu yoyote.

Je, Mhe. Waziri kwa kuwa ulituambia kwamba Mbunge anaweza kuwa Mwenyekiti Mwakilishi awe Makamo Mwenyekiti ili shughuli muhimu ziende vizuri. Suala hili analielewa ?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba katika sheria ile imemtaja Mbunge na Madiwani wawili. Lakini inategemea na jimbo, kama jimbo lina madiwani watatu basi hao madiwani wote na wao watakuwa ni wajumbe. Ndio maana tukasema sisi kabla ya

kuanzisha huu Mfuko itabidi kwanza tutafakari changamoto zote zinazotukabili. Moja katika changamoto ni hii, ambayo katika ile kamati Mwakilishi hajatajwa. Kwa sababu ile sheria sio ya Muungano ni sheria ya Tanzania Bara, sisi huku Zanzibar inatugusa kwa sababu Wabunge wako mpaka huku Zanzibar. Kwa hivyo, ndio maana nikasema tunajipanga na tunaangalia changamoto zitakazotukabili, kama itakuwa vigumu basi itabidi tutaanzisha hiyo kamati nyengine.

Lakini bado tunaweza tukaweka mfumo ule ule Wajumbe wale wale ambao ni viongozi wa kamati ile ya *CDF* anayoisimamia Mbunge wakawa ndio wajumbe wale wale wanaosimamia *CDF* ambayo ataiongoza Mwakilishi. Kwa sababu hatutaki kitu cha kuwatenganisha watu. Kama tunavyofahamu Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania fedha itakayoingizwa katika mwezi kwa jimbo itakuwa ni nyingi sana, kamati ya Mwakilishi, fedha yake itakuwa ni kidogo sana. Sasa hii tofauti itakuja kutusababishia matatizo makubwa sana.

Mhe. Spika, kama tujuavyo mafungu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huwezi ukayalinganisha na mafungu ya Zanzibar. Kwa mfano, Kamati ya Maendeleo ya Jimbo la Mbunge ikiwa kila mwezi inatiliwa shilingi 20 milioni, kamati ya maendeleo ya Mwakilishi ikawa inatiliwa shilingi milioni mbili kila mwezi, patakuja kukalika hapo? Mhe. Spika, ndio maana tukasema kwamba sisi Zanzibar kabla ya kuanzisha huu Mfuko itabidi tuumize vichwa sana na tuangalie namna gani vya kufanya. Kwa sababu tunaweza tukaanzisha jambo kwa maendeleo ya wananchi lakini kwa mtafaruku wa Waheshimiwa, sasa hatutaki iwe hivyo.

Kwa hivyo, kama nilivyosema ni suala gumu hili na hata ninavyolijibu mnaliona liko *very complicated,* kwamba halijibiki moja kwa moja lazima tufanye *research* ya kutosha ili tutapoamua kitu kiwe kinawasaidia zaidi wananchi wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja lenye kifungu a na b. Mhe. Spika, nakumbuka ilifanyika ziara kutoka Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwenda nchini Kenya, mpaka Mheshimiwa husika akatunukiwa jina la George Saitoti. Sasa iliahidiwa kwamba ile ripoti ya ziara ile itawasilishwa Barazani hapa ili wajumbe wako waweze kufaidika.

a) Sijui ripoti ile itawasilishwa lini ?

b) Pia iliahidiwa kwamba tutafanyiwa semina ambapo mambo yote aliyoyajibu Mhe. Waziri hapa mazuri tutaweza kujadili katika

hiyo semina kwa upana na kina kabisa. Sasa naomba kuuliza kwamba hiyo semina itafanyika lini ili isijekuwa wenzetu tayari wameshapitishiwa kule sisi tukawa bado huku. Ahsante sana ?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, nakubali kwamba tulisema baada ya ziara ya Kenya tutakuja kuleta ripoti. Kwa sababu Spika yeye ndiye aliyetutuma twende na yeye mwenyewe aliongoza ule ujumbe basi ni busara ilikuwa lazima wenzetu wajue nini tulichokwenda kukiona na nini tunataka kufanya ili tuweze kushauriana kwa pamoja. Miongoni mwa hayo aliuliza swali Mhe. Ali Suleiman Ali ni moja katika eneo ambalo tungeweza kulijadili katika ripoti hiyo.

Mhe. Spika, baada ya kurudi ziara ile na kuona lile suala namna gani ugumu wake wa kutekelezeka na litaka *good wheel* katika serikali, mimi niliporudi nilimuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi aongozane na baadhi ya wenyeviti aende na yeye akaona ile hali halisi. Kwa sababu hili suala linakuja kwa wawakilishi lakini vile vile na Serikali Kuu ambapo Wizara ya Fedha ndio mdau mkubwa anayehusika katika kukubali hili wazo na kuona ile faida yake. Lakini kimsingi Mhe. Spika, nashukuru kwamba Waziri wa Fedha alikiri kuwa atakwenda ziara ile na nilimuomba afuatane na afisa wake anayeshughulikia miradi ya wananchi katika Wizara ya Fedha ili wakaone. Kwa sababu ile *CDF* kule *CDF* Taifa, *CDF* Wilaya, *CDF* Mkoa mpaka *CDF* Jimbo.

Kwa ngazi ya Wizara ya Fedha vile vile kuna Afisa wao anahusika katika maeneo yote hayo. Sasa ili wajue ule muundo ulivyo halafu tunapokuja kufanya ile semina, kwa sababu hata hiyo semina *sponser* ni yeye Waziri Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi. Kwa hivyo, akishakurudi kule ataweza kuona ule umuhimu wa kuona hili suala liko vipi na tuweze kufanya semina na baadaye yale mawazo tutakayotokana nayo hapa sasa sisi serikalini tutaweza kuyafanyia kazi vizuri, kwa sababu tutakuwa tumeshapata maoni ya Waheshimiwa na katika utekelezaji tusije tukapata tabu.

Lakini Mhe. Spika, suala hili kama tunavyojua linahitaji pesa na ile pesa inatakiwa inapoanza kuingia isisite. Kwa hivyo, ndio maana nikasema lazima Waziri wa Fedha aende na watu wake halafu baadae waone hii kapu yetu inavyoingia tutakuja kuumudu huu Mfuko? Yasijekuwa yale niliyowatolea mfano, Kamati ya Mbunge inaingiziwa shilingi 20 milioni ya Mwakilishi shilingi milioni mbili halafu zikaja zikakwama njiani itakuja kuwa mtafaruku majimboni. Ahsante.

Nam. 59

Huduma za Shirika la Bima

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Shirika la Bima limeanzishwa kwa minajili ya kutunza mali za wateja wake endapo janga litatokea. Lakini hujiendesha kibiashara kwa kuwa mteja wake hujazishwa mikataba maalum kwa mujibu wa sheria na atalipwa fidia baada ya shirika hili kujiridhisha na janga lilivyotokea.

(a) Mhe. Waziri, Askari wa Barabarani (*Trafic*) ndiye mkaguzi wa Bima za Magari Kisheria. Je, mkaguzi wa Bima za Mahoteli, Vituo vya Petroli ni nani Kisheria ?

(b) Je, Mhe. Waziri kuna sheria yoyote inayowataka Vituo vya Petroli na mahoteli kukata bima ya mali zao ?

(c) Tunasikia Bima ya Maisha kwa hapa petu itaishia mwaka huu baada ya kuwalipa wateja wake wote. Je, suala hili ni kweli na ni kwa sababu gani ?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 59 lenye kifungu a, b, na c kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza niseme kwamba Shirika la Bima la Zanzibar limeanzishwa kwa lengo la kutoa huduma za Bima za Mali na Ajali sawa na Kampuni nyengine 20 zinazoendesha biashara hiyo hapa Tanzania.

(a) Bima za magari ni kinga za lazima kisheria na hivyo Askari wa Usalama barabarani husimamia utekelezaji wa sheria hizo.

(b) Bima za Mahoteli na Vituo vya Petroli havikuwekwa katika sheria kuwa ni lazima viwekewe Bima. Mfanyakazi anayo haki ya kuamua kuweka bima au kuendelea na biashara hiyo bila ya kinga za bima na hivyo anachukua *risk* mwenyewe. Hivyo, hakuna mkaguzi wa Bima za Mahoteli na Vituo vya Petroli aliyewekwa na sheria.

Hata hivyo, kwa kuelewa faida za kukinga mali dhidi ya hasara inayoweza kutokea, wafanyabiashara wanashauriwa kuweka kinga za

bima ili kuepuka majanga yanayoweza kusimamisha kuendelea kwa biashara hizo na pia kuleta madhara kwa jamii inayozunguka maeneo hayo.

(c) Mhe. Spika, hakuna taarifa zozote zilizotolewa na Shirika la Bima wala Afisi ya Kamishna wa Bima kuwa Bima za Maisha kwa Zanzibar zinaisha mwaka 2009. Hivi sasa zipo kampuni tatu zinazoendesha biashara hiyo kwa Zanzibar ambazo ni *ZIC*, *NIC* na *African Insurance*.

Aidha, Shirika la Bima la Zanzibar limeajiri wataalamu kutoka nje kutusaidia kazi zifuatazo:-

1. Kufanya tathmini ya Mfuko wa Bima za Maisha (*Actuarial Valuation of the Life Fund*).

2. Kutoa mapendekezo ya kuboresha aina za bima zinazotozwa.

3. Kushauri aina mpya za Bima ya Maisha zinazoweza kuanzishwa kulingana na hali ya soko na mabadiliko ya uchumi.

Kazi hiyo inatarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwezi Novemba, 2010.

Hivyo bado wananchi wa Zanzibar wataendelea kupatiwa huduma za Bima za Maisha kupitia kampuni mbali mbali zilizosajiliwa na Kamishna wa Bima Tanzania ikiwemo *ZIC*.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri katika jibu mama amekiri kwamba mahoteli pamoja na vituo vya petroli havina sheria maalum ya kukata bima. Lakini hivi sasa vituo vingi vya petroli vinajengwa kwenye majumba wanayoishi binadamu na petroli ni hatari.

Je, haoni hiyo ni sababu tosha ya kuweza kuwekewa sheria vituo vya petroli ya kukata bima.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, nakubaliana na yeye kwamba biashara ya vituo vya petroli kidogo ni hatari na inahitaji kuchukuliwa hatua za ziada za tahadhari. Lakini kama nilivyosema ukweli kwamba hakuna sheria, sasa kama tunahisi tufanye sheria basi ushauri wake sisi tumeupokea tutaufanyia kazi, lakini kwa taratibu za bima hivi sasa hakuna. Lakini kama nilivyosema ile ilivyokuwa ni biashara nyeti na inaweza kutokea

mripuko au janga wakati wowote, basi kwenye masuala ya uchumi kuna lugha wanazungumza unaweka *risks and uncertainty.*

Samahani natumia neno la kizungu kidogo, lakini labda mwenzangu Mhe. Ali Abdalla yeye mfasiri mzuri sana atanisaidia. Huo ndio ukweli wenyewe kwamba lazima uchukue dhima ya majanga hayo kutokezea. Kwa hivyo, unapowekeza bila yakitokea hayo inakusaidia mwenyewe na si biashara kama hizo tu, lakini hata mashamba ya miwa kule Mahonda yanaungua moto, maduka, majumba yetu haya, yote ni vyema kuchukua hadhari kwamba likitokezea hili basi unaingia kwenye bima inakulipa, huo ndio uzuri wenyewe.

Vituo vya petroli kujengwa kwenye majumba suala la muhimu unajua ni zile hadhari za kuzichukua, hadhari zake pale unakuwa na zile zana za Zimamoto na nyenginezo. Lakini zamani kituo cha petroli ukitenge, ile ishapitwa na wakati, siku hizi kwenye *modern city* zote vituo vya petroli viko kati kati, lakini hadhari za kuzima moto zinachukuliwa.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, ilivyonipitikia kwamba vituo vya petroli ni moja kati ya vianzio vya mapato ya serikali, kwa sababu vinazalisha sana. Pamoja na kuwa petroli yenyewe ina kodi yake. Lakini hivyo haoni Mhe. Waziri kutokuviingiza vituo vya petroli katika usajili wa bima ni kuvujisha mapato ya serikali ?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, ukweli ni kwamba kama nilivyosema taratibu za vituo vya petroli kisheria, nasisitiza sana suala hilo, kisheria, kama inawekwa sheria kama hawa-*comply* hapo tunawakamata na tunasema wanavujisha. Lakini hakuna sheria, ile ni *jurisdiction* yake mwenyewe, ukija moto ikiungua lake mwenyewe, lakini akiweka bima atalipwa. Mfano mzuri hata gari lako, haidhuru kwenye gari unakamatwa na sheria, lakini kuna aina tofauti za bima, ukitia bima ya rahisi gari likiripuka utalipwa hicho hicho ulichotia Mhe. Ame Mati, lakini ukitia bila ile kubwa watakulipa kila kitu. Sasa hii zaidi ni biashara. Mhe. Spika, mimi nakubali pointi ya Mhe. mwakilishi kwamba imefika wakati tuliangalie suala hili na kwa unyeti wa biashara hiyo. Kwa hiyo, fikra yako tutaizingatia na tutatazama vipi tunaweza tukalifanikisha.

Nam. 65

Athari za Kuyumba kwa Uchumi wa Dunia

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Katika mwaka huu wa 2009 dunia nzima ilikumbwa na msukosuko kwa kuyumba kwa uchumi na kusababisha nchi kubwa duniani kuyumba na baadhi ya mabenki makubwa kufilisika na kufungwa kwa kushindwa kutoa huduma na wimbi hilo lililoendelea katika nchi zinazoendelea na za dunia ya tatu kama zetu za Afrika ya Mashariki.

(a) Je, Mhe. Waziri suala hili la kuyumba kwa uchumi duniani hapa petu limetuathiri?

(b) Kama ndio limetuathiri katika nyanja gani za kiuchumi?

(c) Katika kujihami na hilo nchi yetu imeweka mkakati gani?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 65 lenye kifungu a, b na c kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kama ambavyo nchi nyingi duniani zikiwemo nchi jirani ziliathirika na msukosuko wa kiuchumi, Zanzibar nayo ni miongoni mwa nchi hizo, hatukuweza kukwepa taathira hizo. Mapitio ya hali ya uchumi na mapato ya serikali yamedhihirisha athari kwa uchumi wa Zanzibar inayotokana na msukosuko huo wa kiuchumi duniani.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2008, tulishuhudia kupanda kwa kasi bei ya chakula nchini. Hali hiyo pamoja na kupanda kwa bei ya mafuta vile vile ilichangiwa na bei kubwa ya chakula iliyotokana na upungufu wa chakula duniani. Ongezeko hilo lilichangia ukuaji wa mfumo wa bei hadi kufika asilimia 20.6 mwaka 2008 kutoka asilimia 13 mwaka 2007. Aidha, idadi ya watalii waliongia nchini kwa kipindi cha mwaka uliopita ilipungua kwa asilimia 10 ikilinganishwa na mwaka 2007. Hali hiyo imeathiri sekta ya utalii ambayo imepunguza kasi ya ukuaji wa sekta hiyo pamoja na mchango wake katika uchumi. Kwa ujumla ukuaji wa uchumi Zanzibar ulishuka hadi kufikia asilimia 5.4 kutoka asilimia 6.3 mwaka 2007. Ukuaji wa pato la Taifa nao unatarajiwa kupungua zaidi mwaka 2009 hadi kufikia asilimia 4.5. Aidha, mapato yatokanayo na utalii, mauzo mengine ya biashara za nje kama vile

karafuu na mwani, pamoja na uwekezaji kutoka nje unatarajiwa kupungua katika mwaka 2009.

Mhe. Spika, katika kujihami na msukosuko huo serikali imekuwa ikiendelea na mikakati mbali mbali. Miongini mwa mikakati hiyo ni pamoja na kuongeza bajeti ya huduma za kilimo ili kuwalinda wananchi walio wengi, pia kulinda na kuendeleza programu na miradi muhimu ambayo tumeshaianzisha ili kuweza kuokoa maisha ya jamii. Mikakati mingine ni pamoja na kuweka mazingira mazuri ya biashara pamoja na uwekezaji wa ndani na nje, kuharakisha utekelezaji wa miradi ya umeme na maji safi na salama na kugharamia uimarishaji wa miundo mbinu huku serikali ikihakikisha utulivu wa uchumi.

Aidha, serikali inaendelea na mipango mbali mbali madhubuti ya kutafuta masoko mengine ya utalii mbali na nchi ambazo zimekuwa zikileta watalii zaidi na ambazo ndizo zilizoathirika zaidi na msukosuko huo wa kifedha kama vile Uingereza na Marekani.

Mhe. Spika, suala jengine kubwa na muhimu sana ni suala la udhibiti wa matumizi yetu. Hili suala tumelitilia mkazo kuona kwamba tunatumia ipasavyo na pasipo na umuhimu tunaweza kuacha kwanza mipango ile tufanye ya muhimu na tuendeleze yale yaliyofikia ili tusiathirike zaidi na taathira hii ya uchumi duniani.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa maelezo yake sahihi juu ya hali ya mtikisiko wa uchumi duniani.

Lakini pia nimpongeze kwa kusema kwamba zile nyanja alizozigusa za utalii na mambo mengineyo ni sahihi juu ya kuhakikisha kwamba utalii wetu kwa upande mwengine umeshuka, ili wananchi wajiandae katika mbinu za kuhakikisha kwamba tunaongeza watalii katika nchi yetu.

Mhe. Spika, katika mtikisiko wa uchumi duniani wenzetu wa China wamepiga hatua kubwa sana na mtikisiko huo kwao wao ulikuwa mdogo kuliko nchi nyingi duniani. Kwa upande wa utalii niseme tu kwamba hivi sasa China ni sehemu mojawapo inayoleta changamoto katika maendeleo ya nchi rafiki na kuutangaza urafiki mwema juu ya kutembeleana.

(a) Je, kwa upande huu Mhe. Waziri ameelekeza nguvu zetu huko ili kuhakikisha tunapata marafiki kwa kutuongezea pato katika nchi yetu?

(b) Kwa kuwa miundombinu ndio jambo ambalo linaleta maendeleo katika nchi na serikali kwa upande wake imejitahidi katika kuelekea huko. Je, Mhe. waziri ana mpango gani wa kuwatangazia wananchi juu ya hatua ambazo zimefikiwa katika miundo mbinu ya umeme, maji na kilimo cha umwagiliaji maji katika maeneo yetu ili kuongeza tija?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. mwakilishi kwamba ni kweli serikali yetu na taifa zima kwa jumla hivi sasa tuko katika harakati kuona kwamba hizi taathira za kiuchumi basi zisituguse sana. Mhe. Spika, serikali imekuwa ikichukua juhudi maalum mfano, katika suala zima la usimamizi wa kodi hasa za vyakula, pia kama nilivyosema kuhakikisha kwamba miradi yetu hii tuliyoianzisha inakwenda vizuri.

Katika kuhakikisha huko utakuta hata katika bajeti yetu ya maendeleo mwaka huu tumeongeza zaidi kwa makusudi kuona kwamba tunafanikiwa ipasavyo kwenye miradi ya maendeleo tusikwame.

Miradi aliyoitaja ya umeme, umwagiliaji, maji safi, hiyo ni miradi yetu muhimu na kama nilivyosema tunahakikisha kwamba tunaiendeleza vizuri na naamini tunaitangaza ipasavyo. Muhimu ninachoomba ni ushirikishaji wa wananchi wetu, sote tuone kwamba hii ni miradi yetu, hawa wanaokuja kutusaidia wanatusaidia wao ndio kama wanavyotarajiwa tu na shirika la *IMF* na *World Bank* kwamba katika michango yao ya kodi zao basi angalau asilimia 0.7 wachangie nchi hizi zinazoendelea.

Lakini ni wajibu wetu sisi wenyewe kuwa mstari wa mbele na kusimama kidete tuone kwamba hizi hatua tulizoamua tuziendeleze basi tuziendeleze kwa pamoja. Tuone kwamba hii ni miradi yetu, sio watu wa nje ndio wanakuja kutupa miradi hii. Naamini matunda yake tunayaona, Wajapan kazi nzuri sana wameshafanya kwenye awamu ya kwanza ya maji Mkoa wa Mjini Magharibi na sasa tuko awamu ya pili.

Pia Benki ya *ADB* imekubali kuratibu na kutusaidia miradi ya maji vijijini Pemba na Unguja. Halikadhalika mradi wa umeme ule aliosema Mhe. mwakilishi nao uko tayari. Lakini pia Wakorea wamekubali kutusaidia katika kilimo cha umwagiliaji maji na bado tunaendelea kuwatafuta wafadhili wengine waweze kutusaidia zaidi.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa tafsiri iliyomo ndani ya kichwa changu kuteteruka kwa taasisi za fedha ulimwenguni ni faida kwa

nchi ambazo zinaendelea. Kwa sababu kwa tafsiri ya ghafla kutikisika kwa thamani ya pesa kwa nchi zilizoendelea hushuka bei za bidhaa zao. Zinaposhuka bei za bidhaa sisi Waafrika tunapata faida ya kuzipata bidhaa hizo kwa bei nafuu. Lakini pia hupungua kwa bei ya malighafi na sisi tutapata changamoto ya kuongeza uzalishaji.

Je, Mhe. Waziri kushuka huko inatuletea athari kubwa au inatuletea faida katika nchi kama Zanzibar au Tanzania kwa jumla.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, naomba tutofautishe vitu viwili ambavyo vilitokea niseme labda kwa pamoja au kilianza kimoja kikaja chengine.

Kulikuwa na mtikisiko wa fedha *(financial crisis)* na hii zaidi iliikumba Marekani ndio ilikoanzia hasa huko, ndio ukasikia mabenki makubwa kina *City Bank* wamefilisika. Haijapata kutokea ulimwengu huu *City Bank* kufika kufilisika. Viwanda vikubwa vikubwa vile vya kina *Ford* wakawaondoa wafanyakazi wengi tu. Sasa hicho ndio kilichotikisika.

Wenyewe wanachosema ilitokana na kwamba ile *reserve bank* imeshindwa kudhibiti mikopo ya nyumba, mikopo mingine, kwa hiyo mabenki yakatoa mapesa tu mpaka yakafika kufilisika. Hilo ndio chimbuko hasa. Chimbuko hilo sasa ndio likaathiri nchi zetu ndio tukapata hiyo msukosuko wa kiuchumi *(economic crisis)* ambayo ndio mpaka sisi ikatuathiri.

Sasa matokeo yake ikawa wakubwa wale viwanda vyao vimelala, mali zimelala, ndio ikawa tena huku saruji rahisi, magari kwetu rahisi. Nasikia Mhe. Ame Mati Wadi ulipokwenda Dubai pale uliponunua dola 5,000 gari leo dola imeanguka zaidi tena unachagua unavyotaka. Kumradhi Mhe. Spika, nam-*refer* yeye kwa sababu nilimwona hasa alivyokuwa akichagua. *(Kicheko)*

Mhe. Spika, kuanguka kule kwa bidhaa huku kwetu ni kweli kwa sababu kuna viwanda vya saruji huko nje wanazalisha saruji hawaijui waifanye nini, hawana pakuiuza, ndio maana huku tukapata nafuu saruji ikawa nyingi, lakini bei nafikiri hazianguka sana, zimeanguka lakini kuna baadhi ya mambo kidogo yame-*maintain* pale pale. Hicho ndio kilichotokea.

Sasa wenzetu kule wao walikuwa zaidi mtikisiko wa fedha, lakini ule mtikiso wao sisi huku ikawa kiuchumi ndio tukaathirika. Kwa hiyo, baadhi ya mambo nakubaliana na wewe kweli tumepata faida lakini mengine ni ya hatari kwa sababu ile misaada yao sasa nao tuna wasi wasi tutaipata. Kwa sababu ikiwa wenyewe mapesa hawana watatusaidia nini, tuombe salama.

Nam. 54

Matengenezo kwa Barabara ya Bububu

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza:-

Barabara ya Bububu hupita magari mengi yanayokwenda Mkoa wa Kaskazini Unguja. Barabara hii ilijengwa na KAJIMA kiasi cha miaka 20 iliyopita. Kwa hivi sasa ipo katika hali mbaya yaani imejaa mashimo yasiyokwepeka hasa katika maeneo ya Maruhubi, Sharifumsa, eneo la kituo kidogo cha polisi Bububu na kuleta usumbufu mkubwa kwa watumiaji. Aidha, baadhi ya wakati husababisha ajali ambazo hupoteza maisha ya watu na mali kuharibika.

a) Je, Mhe. Waziri suala hili unalifahamu?

b) Je, kwa kuwa bado barabara ya Bububu ina umuhimu wake wizara ina mkakati gani ili kuondosha tatizo hilo?

c) Hivi sasa kuna vikundi kazi vinazifanyia usafi barabara za shamba kujenga misingi na kuzoa mchanga. Je, kazi hizi zinafanywa na wizara au kampuni?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu:-
Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 54 lenye kifungu a, b na c kama ifuatavyo:-

(a) Wizara yangu inafahamu kuwa barabara ya Bububu kuelekea Mkoa wa Kaskazini hasa kuanzia Maruhubi hadi kituo kidogo cha polisi Beit el Ras kuwa inaleta usumbufu kwa watumiaji kutokana na hali yake ilivyo hivi sasa kutokana na barabara hiyo kuwa ni ya muda mrefu.

(b) Kutokana na umuhimu wa barabara hiyo, wizara yangu kwa kushirikiana na Mfuko wa Barabara imetenga fedha kwenye bajeti ya mwaka huu ili kuweka tabaka jipya la lami *(overlay)* kuanzia Kinazini hadi Bububu pamoja na kusawazisha sehemu zinazotuama maji.

(c) Vikundi kazi vinavyoonekana na Waheshimiwa Wawakilishi pamoja na wananchi ni vikundi ambavyo vimepewa kazi ya usafishaji kwa mkataba maalum wa majaribio. Kazi hiyo inafanywa na Kampuni ya *Double J Construction* ya Mombasa Kwamchina Zanzibar baada ya kushinda zabuni iliyotolewa na wizara.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri anakiri kwamba hivi sasa viko vikundi vinafanya usafi katika barabara mbali mbali na anasema ilitangazwa zabuni. Je, kazi hii yote ya usafishaji katika barabara hii imegharimu kiasi gani. Je, tumetoa wenyewe serikali au tumepata wadau wa maendeleo wametusaidia.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kazi hii ambayo inafanywa na *Double J* inatarajiwa kugharimu shilingi milioni 222. Miongoni mwa kazi zake ni ujenzi wa *culvert* tisa Mwembemakumbi, Beit el Ras, Mwembeladu, Kibonde mzungu *culvert* sita na *culvert box* moja Miwani. Lakini pia kampuni hii inafanya kazi ya usafishaji wa barabara mbali mbali zikiwemo za Wilaya ya Kati, Wilaya ya Magharibi na Wilaya ya Mjini.

Kama alivyosema Naibu Waziri kampuni hii imepewa kazi kwa majaribio baada ya serikali kuona kwamba isiendelee kuajiri vibarua wa kufanya kazi hii kwa sababu baadae gharama zinakuwa kubwa sana. Kwa hivyo, tunatarajia baada ya kumalizika kwa mkataba wa kampuni hii ndani ya miezi mitatu ijayo, tutaziangalia tenda nyengine kwa ajili ya kuendelea na kazi hii.

Kuhusu fedha za kazi hizi, fedha hizi zinatokana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haziko kwa wahisani wowote.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, kwanza niseme tu kwamba Mhe. Waziri katika majibu yake ambayo tunaamini kwamba ni mazuri kwa kuhakikisha kwamba barabara zetu zinawekwa vizuri katika mji wetu na kuleta ufanisi kwa watumiaji wa vyombo mbali mbali.

Kwa kuwa Mhe. Waziri katwambia kwamba hii kampuni inakwenda kusafisha katika barabara mbali mbali za mji wetu ili kuziweka nadhifu na kutumika vizuri. Je, barabara inayotoka Miembeni kupitia Kwahani Baja hadi Kwaboko imo? Ili wananchi wangu wapate waelewe.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kazi ambazo wamepewa kampuni hii ni kusafisha barabara na kujenga *culvert* sio kujenga barabara. Kazi za ujenzi wa barabara zitaendelea kufanywa na Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara kwa kufadhiliwa na Mfuko wa Barabara na tunaushukuru sana mfuko. Kwa sababu kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kuwa barabara ya Kinazini kwendea Bububu karibu shilingi milioni 143 zimetengwa kwa *overlay*. Kwa hivyo, barabara ya Miembeni kwendea Kwahani juu nayo imo katika mpango lakini itajengwa kwa wakati wake utakapofika.

Tunamuomba Mhe. Mwakilishi astahamili kama tulivyomjengea barabara nyengine lengo letu na barabara hii nayo kuijenga, ili yeye na Mhe. Suleiman Othman Nyanga waweze kunufaika na wananchi wote wa majimbo ya Kwahani na Jang'ombe wapate manufaa haya.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza niishukuru serikali kwa kukubali mawazo ya wajumbe kuwa hivi sasa kutokana na kazi nyingi za mabarabara imekubali kutafuta mawakala na makandarasi kushughulikia matengenezo ya barabara zetu?

Mhe. Spika, wakati wa kutoa tenda sifa moja ni uzoefu wa yule mkandarasi juu ya kazi ile. Sasa Mhe. Waziri hapa ametwambia kampuni hii sasa inafanya kwa majaribio. Je, sifa hii ya kuwa na uzoefu wa kazi hii haikuwemo katika mikatabba yake?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kamati yetu ya tenda iliangalia uzoefu wa kampuni zote ambazo ziliomba kazi hii na kampuni hii iliteuliwa baada ya kuonekana uzoefu wake na umakini wake katika utendaji wa kazi. Lakini kwa sababu kazi hii ndio mara ya kwanza inafanyika hapa Zanzibar huwezi kuweka mkataba mrefu wa kufanya kazi hii, lazima tulikuwa tujaze mkataba kwetu sisi ni wa majaribio kuangalia ufanisi wao na uwezo wao wa kazi. Kwa sababu ni mara ya kwanza kufanya kazi kama hizi hapa Zanzibar.

Lakini wamefanya kazi vizuri na tunatarajia kwamba tutakapotangaza tena wanaweza wakaingia na wao na kampuni nyengine tutaziruhusu ziingie, lakini huu ni utaratibu mpya na waheshimiwa najua mwakani ni mwaka wa uchaguzi kwa hiyo kila mmoja anataka barabara nzuri. Kwa hivyo, nafikiri tutaendelea kushirikiana sote ili tuweze kufanikiwa. Sisi tutaendelea kujenga barabara zetu kama kawaida kampuni tutazipa hizi kazi ambazo wanaziweza kama ujenzi wa *culvert*, kusafisha, kujenga mitaro, kujenga vikuta vya barabarani, kampuni tunaweza tukazipa na wakazifanya vizuri.

Nam. 28

Uimarishaji wa Hoteli za Pemba

Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa.

Nam. 39

Zao la Karafuu

Mhe. Ali Abdalla Ali - Aliuliza:-

Wakulima wa karafuu huko Pemba wameanza kuvuna karafuu za msimu wa vuli mwezi Juni, 2009 hadi Septemba 2009 na tayari wameshaliuzia Shirika la *ZSTC* jumla ya tani 1,424 zenye thamani ya shilingi 4,124,951,000/= na makisio yanayotarajiwa hadi kumalizika kuchumwa na kuuzwa kwa zao hili kwa shirika hilo ni jumla ya tani 2,923.

(a) Mhe. Waziri unajua kuwa Shirika la Taifa la Biashara *(ZSTC)* linanunua karafuu za msimu huu kwa kukopa mtaji wenye riba ya asilimia kumi na tano (15%) kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar *(PBZ)?*

(b) Je, Mhe. Waziri kwa utaratibu huu wa biashara huoni shirika linafanya biashara kwa hasara?

(c) Kwa kuwa shirika hili linaidai serikali. Kwa nini lisilipwe fedha zake ili liweze kufanya biashara kwa uhakika?

(d) Kwa kuwa *ZSTC* inapokopa fedha benki hutakiwa kulilipa deni hilo pamoja na riba. Kwa nini shirika hili nalo lisilipwe deni linalolidai kwa muda mrefu pamoja na riba?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 39 lenye kifungu a, b, c na d kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli Shirika la *ZSTC* linanunua karafuu kwa kukopa fedha kutoka *PBZ* na linalipa riba ya asilimia 15 (15%).

(b) Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna uwezekano wa kufanya biashara kwa hasara kama tutaendelea na mikopo na riba ya asilimia 15.

(d) Mhe. Spika, wallahi sijui kwa nini *ZSTC* hailipwi. Kwa sababu mimi mwenyewe nataka walipwe hata leo.

MHe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, shirika letu la

ZSTC baada ya kukopwa na serikali na kuwa halilipwi hali ya mtaji wake unakuwa mdogo na inashindwa kukabili shughuli zake, lakini hata pia kulipa fidia kwa wanaoanguka mkarafuu. Kwa sababu moja katika tabia ya mashirika ni kuuzwa hisa.

Je, Mhe. Waziri anaonaje hivi sasa akatangaza taarifa ili wananchi wanunue hisa katika shirika hili ili mtaji uwe mkubwa imudu shughuli zake za kununua bidhaa pamoja na kutoa huduma za wale wanaoanguka mikarafuu?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, Shirika la *ZSTC* sasa hivi liko katika mageuzi ya sera za kiuchumi chini ya Wizara ya Fedha. Sasa Wizara ya Fedha katika mchakato wao wa mageuzi ya sera za kiuchumi wakihisi hili linafaa kwa Shirika la *ZSTC* basi *Central Reform Unit* itatuarifu na hatua zitachukuliwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuongezea lile jawabu la swali la mwanzo la deni la ZSTC kwa nini halilipwi.

Mhe. Spika, Shirika la *ZSTC* ni shirika la serikali, kama serikali tuna dhima ya kulisaidia kuona kwamba nalo linafanya kazi ipasavyo. Kwa hiyo, tumechukua jukumu hata nafikiri tumetia kwenye bajeti yetu ya serikali ya mwaka huu kwamba deni lote la *ZSTC* litalipwa ndani ya mwaka huu. Hiyo nakumbuka tumeitia kabisa ndani ya bajeti ya serikali.

Lakini pia Mhe. Spika, nataka nitoe taarifa tu kwamba kama serikali *ZSTC* wanapokopa huwa wanawawajibika kulipa baadhi ya kodi kama *stamp duty* na wakilipa wao inakaribia bilioni. Lakini ile tunawasamehe ili wapate unafuu wa kuendesha kazi zao. Kwa hivyo, sisi tuna *role* kubwa ya kulisadiia shirika kama serikali kuona kwamba linaendesha kazi zake vizuri. Naomba na hii waheshimiwa waifahamu, sio kama tumelitupa haliendi ipasavyo, tunafanya kazi nao kama Shirika la Serikali.

Nam. 45

Wataalamu Wa Michezo, Zanzibar Kupatiwa Elimu

Mhe. Ali Abdalla Ali - Aliuliza:-

Hivi sasa nchi nyingi duniani suala la michezo limepewa kipaumbele ili kujiweka katika nafasi nzuri Kimataifa. Naipongeza wizara kwa kuleta wataalam wa michezo wa fani mbali mbali. Kwa utaratibu huo tumepiga hatua

kwa kiasi fulani lakini tunahitaji mikakati zaidi ili na sisi tuwe katika nafasi nzuri kimichezo.

(a) Je, Mhe. Waziri Zanzibar ina makocha wangapi wa ngazi ya juu na ni wa fani gani?

(b) Je, wapo makocha waliosoma nje ya nchi?

(c) Kwa kuwa hivi sasa michezo ni sehemu ya ajira. Je, wizara ina mikakati gani ya kukuza michezo?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 45 lenye kifungu a, b na c kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla sijajibu swali naomba sana kumpongeza Mhe. Mwakilishi kwa kuona umuhimu wa namna suala la michezo linavyopewa kipaumbele na nchi nyingi duniani. Pia tunapokea pongezi zake za dhati kwa kuipongeza wizara yetu namna inavyowajibika katika kuleta wataalam mbali mbali wa michezo hapa nchini Zanzibar.

Mhe. Spika, napenda kumuahidi Mhe. Mwakilishi na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kuwa tutahakikisha hatua iliyofikiwa inadhibitiwa na mikakati zaidi itaandaliwa ili kujiweka katika hali nzuri ya kimichezo kimataifa.

(a) Hivi sasa Zanzibar ina makocha wengi wa ngazi za juu katika fani za michezo mbali mbali. Makocha hao wamepata mafunzo ndani na nje ya nchi kupitia serikali moja kwa moja, vyama vya michezo na asasi nyengine za kimataifa.

(b) Kwa takwimu za haraka tulizonazo tunathibitisha kuwa wapo makocha 33 waliosoma nje ya nchi.

MCHANGANUO:

- *Administration* - 3
- *Swimming* - 2
- *Weightlifting* - 3
- Riadha - 4

- *Volleyball* - 1
- *Handball* - 1
- *Basketball* - 1
- Mpira wa miguu - 7
- Karati - 3
- Judo - 8

(c) Ni kweli kuwa michezo ni sehemu ya Ajira, Wizara imepanga mikakati ifuatayo katika kukuza michezo nayo:-

- Imeandaa utaratibu utakaowezesha wanamichezo wetu kushiriki katika michezo ya kulipwa na mikataba ya majaribio nje ya nchi, yaani *trial*.

- Kushajihisha vyama vya michezo, vilabu pamoja na vilabu vyengine ili waweze kufanya mawasiliano kupata fursa za kucheza kwa kulipwa na kuwa na mikataba ya kimashirikiano kati ya vilabu vya hapa nchini kwetu na vile vilivyokuwepo nje ya nchi.

- Kufanya juhudi kupata wataalam wa nje kuja nchini kufundisha fani ya utawala ndani ya michezo, viongozi, walimu, waamuzi na wachezaji kwa ujumla.

- Wizara imo mbioni kushajihisha na kuanzisha vyuo vya taaluma ya michezo yaani (*Sports Academy*, ama *Sports Polytechnics*) kwa lengo la kuendeleza vipaji vya wanamichezo wadogo na vijana na kutoa taaluma mbali mbali za michezo.

  Wizara pia inatoa wito kwa vijana, wapenzi wa michezo na wana michezo wote kwa jumla, kuanzisha asasi zao za kiraia zinazohusiana na michezo kama vile ambavyo asasi nyengine huanzishwa katika fani nyengine mbali mbali. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwanza naipongeza wizara kwa jitihada kubwa inayofanya ya kutafuta makocha kwa lengo la kunyanyua michezo katika nchi yetu.

Swali. Hivi sasa kimataifa huwa kunatajwa ngazi mbali mbali kuanzia moja mpaka mwisho ki-*football*. Je, nchi yetu kwa juhudi hizi za sasa hivi tuko kwenye nafasi ya ngapi kimataifa?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Ahsante Mhe. Spika. Kwanza kabisa tunapokea pongezi zake za dhati kwa mara nyengine. Pili, nadhani swali lake angeliweka sawa, je amekusudia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ama Zanzibar kama ni nchi?

Mhe. Ali Abdalla Ali: Tanzania.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Ahsante. Mara ya mwisho Tanzania ilikuwa nafasi ya 186 katika mpangilio wa ulimwengu. Lakini hivi sasa imeweza kupanda kwa mara ya mwisho nilivyoangalia nafasi ya 122, lakini wiki hii sina uhakika kama imepanda zaidi.

Wajumbe: Nafasi ya 99 sasa hivi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Eeh! Nafasi ya 99 naambiwa Mhe. Spika, na wapenzi wa michezo ndani ya Baraza lako. Kwa hivyo, Tanzania iko kwenye nafasi ya 99. Kwa hivyo, Tanzania iko kwenye 100 bora na mikataba ya kimataifa inasema hivi, hasa kule UAFA na *European Union* kwamba hawachukuwi wachezaji wa nchi zilizokua zaidi ya 100, wanachukua waliokuwa chini ya 100. kwa hivyo, naweza kusema kwamba Tanzania sasa wachezaji wetu wanaweza kwenda katika Bara la Ulaya, sio Arabuni na kwengineko hapa, katika Bara la Ulaya kwa ajili ya kwenda kucheza michezo ya kulipwa.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Katika michezo ambayo inapendezesha au inastawisha sherehe zetu ni mchezo wa halaiki. Tuliona hapa katika sherehe za miaka 10, miaka 30 ya Mapinduzi ya Zanzibar uwanja wetu ulishamiri sana na ikawa mchezo huu ni kivutio.

Hata juzi Mhe. Spika, katika kutimiza miaka 60 ya Mapinduzi ya Uchina tuliona kwenye runinga jinsi uwanja kule Beijing ulivyoweza kujaa. Katika

mafunzo ambayo Mhe. Naibu waziri ametaja, sikumsikia kumtaja mwalimu ambaye amepelekwa kufundisha au kuja kufundisha mchezo wa halaiki.
Je, serikali ina mpango gani wa kumpeleka mwalimu ili aweza kuja kufundisha mchezo wa halaiki hapa nchini?

Pia na mchezo wa sarakasi. Mhe. Naibu Waziri hakumtaja kuwa atamtafuta kocha huyo, na huyu vipi kuna mpango gani wa kumleta mtaalamu au kocha wa kuja kufundisha sarakasi, kwa sababu ni moja kati ya michezo ya kiulimwengu inayoshindaniwa katika *Olympic* na kwengineko?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kweli tunakiri kwamba michezo ya halaiki pamoja na sarakasi ilikuwa ikichezwa sana hapa visiwani kwetu Zanzibar. Hili tutalichukua kama wazo naamini Mhe. Waziri yupo na ameshalipokea. Tutalichukua kama wazo la kushajihisha michezo hii ili irudi tena hata katika sherehe zetu za Mapinduzi ya mwaka 2010 ambazo naamini zitakuwa ni za hali ya juu kabisa, tutajaribu kufanya mambo mengi sana pamoja na haya ya halaiki.

Michezo ya sarakasi Mhe. Spika, naomba tukiri kwamba zamani walikuwa wakipelekwa wataalamu nchi za nje kwenda kusomea michezo ya sarakasi, nakumbuka mimi ilikuwa ni nchi ya Korea pamoja na China. Hivi karibuni haikuwa inafanyika hivyo. Kwa hivyo, nalo hili tumelipokea kama wazo na tutalifanyia kazi.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri, Katibu wa Wizara, Baraza la Michezo la Taifa na vilabu pamoja na idara zote za michezo, kwa shughuli zao mbali mbali za kukuza michezo hapa kwetu Zanzibar.

Mhe. Spika, pamoja na juhudi hizo, ishara tosha iliyojitokeza kwamba leo hapa katika Baraza lako tukufu Mhe. Waziri kasimama asubuhi kueleza kwamba ujio wa kombe la dunia, kwa Kiingereza linaitwa *FIFA World CUP*. Hiyo ni kudhihirisha wazi kwamba Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake zinaendeleza michezo hapa nchini kwa manufaa ya vijana wetu. Swali langu liko hapa.

Mhe. Spika, kikundi chochote kikifanya vizuri huwa kinapata sifa, na sifa zile kama Mhe. Spika, kamati yako moja umeituma pahala kwenda kushughulikia jambo lolote la msingi, na ikuletee taarifa nzuri na wewe taarifa ile ukishakabidhiwa uitangaze, ili sisi kamati tufanye ari zaidi linapotokea jengine tufanye vizuri.

Kwa kuwa wana michezo wetu, narudia lile swali la juzi ambalo nililikosa kwa bahati mbaya. Wana michezo wetu wa timu ya mpira wa miguu ya vijana ambao walishiriki katika mashindano ya Tanzania ya Copa Coca Cola na kuchukua ubingwa wa Tanzania, Mkoa wa Mjini Magharibi. Wakati huo huo riadha, timu ya Mkoa wa Mjini Magharibi imechukua ushindi na kupata kombe na pia kuwe timu bora katika mikoa yote ya Tanzania 26.

Je, kwa kuwa waliandaliwa ziara na Mhe. Rais na kwa bahati mbaya Mhe. Rais alidharurika kutokana na shughuli mbali mbali, lakini naamini bado Mhe. Waziri yupo na naamini kwamba hili atalifikiria. Je, lini vijana wale watapatiwa nafasi hiyo ya kwenda kuonana na Mhe. Rais na pia kumkabidhi lile kombe?

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kuhusu lini timu ambayo alikuwa anaiongoza kwenda nayo katika mashindano makubwa ya Copa Coca Cola na kupata ushindi wa Tanzania nzima itakwenda kwa Mhe. Rais.

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza hili kwamba ahadi ile bado ipo na mara tu Rais atakaporudi safari yake Mhe. Ali Suleiman Ali atapata fursa ya kuiongoza timu ile kwenda kulipeleka kombe kwa Mhe. Rais.

Nam. 50

Ujenzi wa Mabanda ya Kudumu Eneo la Saateni (Jua Kali)

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza:-

Eneo la Saateni la wauza mitumba kwa umaarufu Jua Kali lilianza kazi ya biashara kwa mabanda machache ya kudumu yaliojengwa na Baraza la Manispaa na mabanda mengi yalikuwa ya muda mfupi. Hivi sasa kuna wimbi kubwa la ujenzi wa mabanda ya kudumu ya biashara katika eneo hilo. Hatua hii itapunguza shida wakati wa mvua na jua, lakini pia imetoa haiba nzuri ya eneo hilo.

(a) Je, Mhe. Waziri mabanda hayo ya kudumu yamejengwa na serikali au watu binafsi?
(b) Kama ni serikali ni kiasi gani cha fedha zimetumika?
(c) Kama ni watu binafsi ni utaratibu gani uliotumika?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya (SMZ) – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 50, lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mabanda hayo ya kudumu yamejengwa na watu binafsi baada ya kukubaliana na Baraza la Manispaa.
(b) Hapana fedha ya serikali iliyotumika kujenga mabanda hayo.
(c) Utaratibu uliotumika kwa watu binafsi ni ule wa kufunga mkataba na Baraza la Manispaa kwa utaratibu wa *BoT*, yaani *Operate and Transfer*.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Waziri naomba ruhusa yako kumuuliza swali moja la nyongeza. Serikali kwa kupitia Baraza la Manispaa Zanzibar liliamua kwa makusudi kutenga eneo la Saateni kwa shughuli za biashara ndogo ndogo na mitumba ili kupunguza misongamano katika eneo la Darajani pamoja na maeneo mengine ya Mlandege, Kilimatinde na Mchangani.

Kwa kufanya hivyo, naipongeza serikali. Hivi sasa watu wanaweza kwenda kufanya biashara au kununua vitu katika maeneo hayo bila matatizo. Hivi sasa kumetokea na eneo jengine ambalo linaitwa Kivulini huko Mwanakwerekwe ambalo linahatarisha wafanyakazi au watembeaji pamoja na magari kusongamna.

(a) Je, Mhe. Waziri kule amefanya ni extension ya kule Saateni na badala yake akaita Kivulini?

(b) Kwa kufanya hivyo, haoni sasa hivi pale Mwanakwerekwe ni barabara kubwa ambayo inaunganisha vijijini na mjini ni hatari kwa magari makubwa ya mizigo na ya mawe kwa kujengwa banda lile linaloitwa Kivulini karibu na barabara?

(c) Kama anajua je, atachukua hatua gani kurekebisha hilo?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya (SMZ): Mhe. Spika, kwa kweli mipango inakwenda mmoja baada ya mmoja, kwa sasa tumewatoa Jua Kali tumewapeleka kivulini kule Saateni na tuhakikishe kwanza tunamaliza hao, halafu tunawaendea hao wengine ambao wako katika Kivulini kama ulivyowaeleza.

Nam. 55

Kuzuia Uharibifu wa Mazingira

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Naipongeza Wizara ya Kilimo kwa kuanzisha vikundi vya mazingira ambavyo vinafanya kazi ya kulinda mazingira yasiharibiwe hasa ya Baharini na kuzuia uvuvi haramu. Aidha vimepewa fursa ya kuwakamata wale wote wanaofanya uharibifu huo na kuwapeleka katika vyombo vya sheria kwa hatua zaidi.

(a) Kwa kuwa katika kukamata muhalifu kunahitaji sheria. Je vikundi hivi vya mazingira vina Sheria yeyote inayowalinda?

(b) Kwa kuwa Sheria haipo, Je, Wizara haioni haja ya kutunga japo sheria ndogo ndogo (*By law*) ili iwape nguvu katika kazi zao?

(c) Kwa kuwa maeneo mbali mbali ya mji wetu huchimbwa mchanga, wizara inaliangaliaje suala hili?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. mwakilishi swali lake Nam. 55 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Napenda kulijuilisha Baraza lako tukufu kwamba vikundi hivi vya mazingira vimepewa fursa ya kulinda maliasili tu kwa mujibu wa Ibara ya 23(2), (3) ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Toleo la 2003. Wakati inapolazimu kukamata wahalifu, vikundi hivi hutoa taarifa wizarani na kwa kushirikiana na vyombo vya dola, kama vile Polisi ambacho ndiyo chombo chenye mamlaka ya kukamata kisheria, wahalifu hao hukamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya Sheria.

Hata hivyo, Wizara kwa kuzingatia umuhimu wa vikundi hivi katika kusimamia na kulinda uhifadhi wa rasilimali za bahari na mazingira yake, imeona ipo haja ya kutunga sheria ndogo ndogo (*By Laws*) na tayari imeshatayarisha sheria hizo ambazo zitavipa nguvu vikundi hivyo katika kutekekeza kazi zao. Sheria hizo zipo katika hatua za mwisho kukamilika na kuanza kutumika. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 58

Kuendelezwa Kilimo cha zao la Mpira

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Ni muda mrefu sasa mashamba ya zao la Mipira ya Unguja na Pemba yamekodishwa kwa wafanyabiashara binafsi ili kuongeza mapato katika mfuko mkuu wa Serikali. Zao hili husafirishwa nje ya nchi kwa kuwa hatuna kiwanda cha kutengeneza mipira.

(a) Je, Mhe. Waziri ni kiasi gani cha fedha kinapatikana katika kukodisha mashamba hayo kwa mwaka Unguja na Pemba?

(b) Kwa kuwa faida inayopatikana ni kubwa katika zao hilo. Je, Serikali ina mpango wowote wa kuliendeleza zao hilo?

(c) Tunasikia kuwa mipira hii inagemwa kwa muda wa miaka (10) kumi tu na ikizidi hapo huwa basi. Je, suala hili ni kweli?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 58 lenye kifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, swali hili lilikwisha kujibiwa vizuri na Mhe Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Fedha na Uchumi katika kikao cha Bajeti kilichopita.

Lakini kwa manufaa ya Baraza lako tukufu, naomba kuongezea jibu la ziada kwamba katika suala la mpira serikali inapata dola 100,000 kwa mwaka, ahsante Mhe. Spika.

KAULI ZA MAWAZIRI

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamduni na Michezo: Mhe. Spika, , kwa ruhusa yako naomba kutoa taarifa ya kuwasili Zanzibar Kombe la Dunia, yaani FIFA World CUP kwa ziara ya siku moja.

Mhe. Spika, mnamo tarehe 20/11/2009 litafika Zanzibar kwa ziara ya siku moja kombe la dunia yaani *FIFA World CUP*. Sote Mhe. Spika, tunaelewa kwamba mashindano ya kombe la dunia yatafanyika Afrika ya Kusini mwaka 2010.

Kama kawaida Chama cha Mpira wa Miguu yaani *FIFA* huwa inaandaa kulitembeza kombe hili katika *continents* ambazo nchi moja wapo ilipata fursa ya kuendesha mashindano yale kwa mwaka ule. Kwa kuwa mashindano hayo yatafanyika Afrika ya Kusini, Bara la Afrika limepata fursa hiyo ya kombe hili kutembezwa katika baadhi ya nchi zetu za Afrika. Kwa maana hiyo Tanzania imebahatika.

Mhe. Spika, kwa kuwa kuna uhusiano mzuri kati ya wizara zetu mbili Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, tumewasiliana na tumefanikiwa kupata bahati ya kulileta kombe hili hapa Zanzibar hata kwa angalau siku moja. Kwa hivyo, kombe hili litafika tarehe 20/11/2009.

Mhe. Spika, kombe la dunia ni kombe maarufu, lenye sifa na ni kombe ambalo kuingia katika nchi yoyote ile huwa linasherehekewa na watu wanafarajika sana. Kwa sababu hiyo nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na kwa kutumia kifungu cha 44 cha kanuni za Baraza la Wawakilishi kuwasilisha taarifa hii adhimu na muhimu kupitia kwako na Baraza hili kwa wananchi ili wananchi wajitayarishe kulisherehekea kombe lao.

Mhe. Spika, mipango yote ya mapokezi ya ulinzi yameshakamilika. Kwa hivyo tunasubiri sasa tarehe ikifika kombe hili litawasili, na atalipokea Mhe. Rais katika eneo ambalo mwenyewe baadae ataamua lipelekwe wapi ili alipokee. Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa hii, ahsante.

Mhe. Najma Khalfan Juma: (Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo): Mhe. Spika, kwa niaba ya Kambi ya upinzani naomba kuchukua fursa hii kutoa maoni mafupi juu ya ujio wa kombe la dunia Zanzibar, litakalowasili tarehe 20/11/2009.

Mhe. Spika, kwa kuwa tuko hapa kwa mnasaba na mchezo wa soka, naomba uniruhusu kumkumbuka na kumpa heshima kocha mzalendo, aliyewahi kuipa Zanzibar sifa kwa kufikia kufundisha timu ya taifa ya Zanzibar na ile ya Tanzania, na kutumikia mchezo huo kwa miongo kadhaa Hassan Khatib Mzibondo, ambaye amefariki hivi karibuni.

Kisha natoa shukurani kwa hotuba ya Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mhe. Ali Juma Shamuhuna juu ya tukio tunalolizungumza hapa, yaani ujio wa kombe la dunia.

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Waziri kwamba tukio hili ni muhimu na heshima kwa Zanzibar, kila mmoja wetu ni vyema akalifurahia na kuliunga

mkono hasa kwa vile fainali ya kombe hilo la 2010 litafanyika ndani ya ardhi yetu ya Afrika, yaani huko Afrika ya Kusini.

Hii inaonekana kuwa ni ishara kuwa Zanzibar kwa kiasi inakubalika katika taasisi za kimataifa za michezo, na kwa sababu naamini kwamba ujio wa kombe hili hufanikiwa tu kwa sababu ya uhisani, bali kwa kuona kuwa Zanzibar ina nafasi muhimu katika Tanzania, nchi ambayo pia ni ya pekee kwa Afrika nzima ambapo kombe hili litakaa kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, hapo kabla Zanzibar ilisononeka pale pale mwenge wa *Olympic* ambapo ulifika Dar es Salaam, ikiwa ni mji pekee Afrika nzima kufika na kutembezwa haukuweza kuvuka bahari na kuja Zanzibar. Moja ya hoja ambayo ilitolewa wakati huo ni ufupi wa muda, lakini wako pia walisema kuwa kuipa Zanzibar nafasi ni kudhulumu mikoa mingine ya Tanzania.

Pia itakumbukwa huko nyuma heshima iliyofanana na ujio wa kombe la dunia ilikuwa ni ile ya mwenge wa michezo wa Jumuiya ya Madola na furaha ya kupokea na kuutembeza mwenge huo sote tunaikumbuka.

Mhe. Spika, niruhusu niseme kuja kwa kombe la dunia ni taswira ambayo ni lazima itiwe katika mitizamo maalum, ili kulipa jambo hilo stahiki yake na sisi tunaotembelewa na kombe hilo tupate nafasi ya kujiuliza maswali mengi na sio kutizama tukio hili kwa macho ya kisiasa.

Mhe. Spika, mpira wa miguu ndio mchezo maarufu na mkubwa kabisa duniani na hata hapa kwetu ndio mchezo unaopata umuhimu. Mchezo huu una ushawishi mkubwa miongoni mwa vijana, kama unatumiwa vyema unaweza kujenga mapenzi ya wananchi kwa nchi yao.

Mhe. Spika, sote tunajivuna kwa fainali za kombe la dunia zinafanyika Afrika, kwa sababu tunataka kujikurubisha na mafanikio ya kutambuliwa Afrika, kupewa heshima hiyo kwa mara ya kwanza ingawa tungependa nchi yetu ingekuwa dimbani, lakini hatukuweza kupata bahati hiyo na kwa hivyo tutakuwa watazamaji tu.

Hapa ndipo Mhe. Spika, ningependa kutoa hoja yangu ya kwanza kuhusiana na ujio wa kombe hilo hapa kwetu. Ujio huo utakuwa na maana sana, iwapo wazanzibari watapata fursa mbili. Ya kwanza ni kwenda kuona michuano hiyo huko Bondeni kwa mwenye uwezo na pili, kwenda kuona mechi hizo kwa kupitia televisheni.

Mhe. Spika, nimeona niseme hili na mapema, kwa sababu ya ghofu kuwa inaweza ikatokea kukosekana mipango ya uhakika ya michuano hiyo

kuonekana na wananchi, kama ambavyo tumeshawahi kukosa kuona michuano mingine mikubwa. Najua kuwa kuna suala la kununua haki za kutangaza, lakini hili tulitafutie ufumbuzi mapema na sio kungojea zimamoto.

Kwa hivyo, iwapo michuano hiyo itaoneshwa, basi wengi tunaamini itasaidia kuhabarisha mchezo wa soka hapa Zanzibar, ambapo baadhi ya watu wamekuwa wakisema kuwa kiwango chake kimeshuka. Hilo limekuwa likisemwa na kocha Maksio Maksimu na kushikilia kuwa hiyo ndio sababu ya kutochaguliwa wachezaji wa Zanzibar kujiunga na timu ya taifa ya Tanzania, yaani Taifa Stars.

Hivi sasa soka ya Zanzibar imepata mwamko mpya kwa matukio yaliyojiri hivi karibuni. Ikiwa ni pamoja na ujio wa kocha mpya wa Kimisri, kupata nafasi mchezaji wa Kizanzibari kwenda chuo cha soka huko Ureno na tukio la hivi karibuni la zoezi la kuchagua vipaji, vilivyofanywa na *Orange Academy* la kuchagua vipaji ambavyo vitaendelezwa, ili kulenga kupata wachezaji wa kulipwa.

Pia tukio la Zanzibar la kujiunga na shirikisho la nchi zisizo wana chama wa *FIFA*, yaani *International Football Union* ni hatua zenye mwelekeo mzuri. Kwa maana hiyo, Mhe. Spika, ujio wa kombe la dunia utakuwa na maana iwapo na sisi tutaweka dhamira ya kutaka kubadilisha na kuchukulia kuja kwake kombe hilo, kuwa ni changamoto ya mabadiliko. Watu husema “mkaa na waridi hawachi kunukia” Basi na sisi tulioletewa kombe hilo tupate angalau harufu yake.

Mhe. Spika, kwa kuwa mchezo wa soka unanguvu ya kuunganisha watu, ningependa ujio wa kombe la dunia iwe ni chachu ya kutuunganisha maana kama litakuja na kuondoka na sisi hatukupiga hatua katika eneo hilo, basi itakuwa na maana ndogo yaani ya kuja kwake. Tunapenda kupongeza wazo la kombe hilo kupokelewa na kufikishwa katika bustani ya Forodhani, pale ndio uso wa Zanzibar, mbali ya kuwa ni ndani ya mji wenye hadhi ya uridhi wa dunia. Sisi tunawaomba wananchi wote walipokee kombe hilo kwa moyo mkunjufu maana ugeni huu ni wetu sote.

Mhe. Spika, ni matumanio yangu basi kuwa mapokezi ya kombe hilo yatashirikisha pande zote za kisiasa, kona zote za kijamii na bila kusahau na kuwajali wachezaji waliofia jasho nchi hii ambao tunaamini watapewa nafasi muhimu katika mapokezi hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha, ahsante.

Mhe. Kamal Basha Pandu: Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kwanza kuipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa hatua yake hiyo ya kuleta kombe la dunia hapa Zanzibar kwa mara ya kwanza.

Pia nachukua fursa hii kutoa rambirambi zangu za dhati kabisa, kwa kifo cha kocha mstaafu Hassan Mzibondo, ambaye ameiletea historia Zanzibar wakati wa uwalimu wake.

Mhe. Spika, nakumbuka katika mwaka 1982 kwa mara ya kwanza Zanzibar iliingia *semi final* katika mashindano ya *Challenge CUP*. Kwa hivyo, na mimi namkumbuka kwa hilo na mengineyo Mhe. Spika, lakini nafasi hii tuliyoipata ya kulileta Kombe la Dunia hapa Zanzibar naomba itumike nafasi hii kwa kuendeleza michezo Zanzibar.

Miongoni mwake kufufua ile ari au *speed* na dhamira ya kujiunga na *FIFA*, ingawa matokeo mbali mbali na maeneo tofauti yamechangiwa na pamoja na masuala mbali mbali yameulizwa. Hata hivyo bado ningependa jitihada zile ziendelee hasa kwa kutumia nafasi ile ya Zanzibar kuwa Mwanachama wa Mpira wa Miguu cha Uingereza.

Mhe. Spika: Mheshimiwa Mjumbe, tunategemea swali ndivyo Kanuni inavyotuelekeza wakati tukiwa kwenye kipindi cha Maswali.

Mhe. Kamal Basha Pandu: Mhe. Spika, naomba kuuliza sasa ule uwanachama wake wa Chama cha Mpira wa Miguu cha Uingereza, ambapo kingetusaidia kusukuma mbele haya masuala yetu ya kujiunga na *FIFA* yamefikia wapi hadi hivi sasa?

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, na mimi nichukue fursa hii ya kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na wizara yake kwa mashirikiano mazuri baina ya wizara yetu ya Zanzibar na ile ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya michezo.

Vile vile niseme kwamba ninaipongeza Kampuni ya *Coca Cola* ambao ni wahusika wakuu kwa kuja kombe hili hapa Tanzania. Swali langu lipo hapa Mhe. Spika, naamini madhumuni makubwa ya kuja kombe hili baada ya wenzetu hawa kuambiwa kwamba Mashindano haya ya *Copa Coca Cola* yatafanyika Tanzania na Mabingwa wako Zanzibar. Kwa hivyo, ni fursa nzuri kwao na kusema lazima tuende kwa mabingwa hao kama kuwapa mkono wa hongera.

Je, Mhe. Waziri kwa kuwa vijana wapo pamoja na viongozi wao ambao walipigana kufa na kupona kwa ajili ya kuleta ubingwa Tanzania, siku hiyo watashirikishwa kikamilifu. ?

Mhe. Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Hivi asubuhi nilikuwa nikiangalia Gazeti la Zanzibar Leo, nimeona liliandikwa kwamba Mhe. Mbunge wa Jimbo la Uzini atalipeleka Kombe la Dunia katika Jimbo la Uzini, lakini ndani sikusoma sijui kama ameliona Mhe. Waziri na analifahamu suala hili kama kweli linakwenda Uzini au ni maneno ya gazeti tu ?

Mhe. Naibu Waziri Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, na mimi sina budi kwanza kukushukuru wewe binafsi pamoja na Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kwa jinsi juhudi alizozifanya na kupelekea Kombe hili la *World Cup* likaingia Zanzibar.

Lakini nataka kuuliza swali pamoja na ombi ndani yake kuona kwamba wakati kombe hili litakapokuja na kwa sababu ya thamani ya kombe hili, basi angalau Wajumbe wako wa Baraza hili tukufu tupate nafasi ya kulikamata kwa mikono yetu, ili tuthibitishe furaha yetu na sisi kwamba ni miongoni mwa watu duniani. Mhe. Spika, langu lilikuwa ni hilo *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, nami naunga mkono na kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri Kiongozi pamoja na serikali nzima kwa mipango hii ya kulileta Kombe la Dunia hapa kwetu.

Mhe. Spika, nataka kumuuliza swali moja Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, haiatkuwa busara kama kombe lile tutalipokea uwanja wa ndege kwa gari iliyowazi moja kwa moja na vijana pamoja na wananchi mbali mbali tukapangana mpaka huko linakokwenda.

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwa ruhusa naomba kujibu mswali yaliyoulizwa na Waheshimiwa mbali mbali kuhusu taarifa niliyoitoa hivi karibuni.

Kwanza Mhe. Kamal Basha Pandu. Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kutokana na mazungumzo yetu yaliyowashirikisha mawaziri wawili wa wizara mbili hizi, yaani Wizara za Habari Utamaduni na Michezo.

Kwa kweli tumefikia kwenye maamuzi mazuri kwamba mgogoro ule wa *TFF* na *FIFA* umemalizika na tumekubalika kuwa itaundwa timu ya *TFF* na *ZFA* kwa kushirikiana na mawaziri pamoja na viongozi wa vyama hivyo viwili kwenda kuzungumza na Rais wa *FIFA* Joseph S. Blatter, kwa ajili ya kuingiza Zanzibar kukubaliwa katika nafasi ya *FIFA* hata kama ile nafasi ya. *Associate Membership*.

Kwa hivyo, suala lile bado lipo na karibu litatekelezwa kwa utaratibu huo na utaratibu huo ndio tulioutumia tulipokwenda kuomba *Associate Membership* ya *CAF* na tulibahatika kuupata.

Mhe. Ali Suleiman Ali kuhusu vijana wetu walioshinda *Copa Coca cola* kwamba watapa nafasi ya kuhudhuria kwenye sherehe hii. Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Mwakilishi kwa kulizungumza suala hilo, kwa sababu tulikuwa na dhamira ya kuwapa nafasi vijana wetu hawa na wale wa timu zetu zote zilizoshinda katika michezo yetu mbali mbali, kuwepo pale ndani ya uwanja wa eneo ambalo kombe hilo litawekwa, ili wapate fursa ya kuliangalia kombe hilo.

Vile vile tutatoa taarifa hivi karibuni za *route* ambazo kombe hilo kutoka *Airport* kupitia sehemu moja baada ya nyengine na kurudi *Airport*. Hivyo tutatoa taarifa hiyo, ili wale ambao hawatapata nafasi ya kuja pale kiwanjani ambapo tutalionesha kombe hilo mbele ya Rais, basi watabakia kwenye maeneo hayo ambayo kombe hilo litapitia wapate fursa ya kuliona.

Mhe. Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja. Kwa kweli hata mimi nilishtuka nilipoiona taarifa katika Gazeti la Zanzibar Leo, kwamba Mhe. Moh'd Seif Khatib atalipeleka Kombe la Dunia Uzini. Kwa hivyo, kama ingekuwa fursa hiyo inapatikana basi nadhani mimi ningekuwa wa mwanzo kulipeleka Donge na wala sio Uzini, lakini fursa hiyo haitapatikana.

Mhe. Spika, baada ya kuisoma ile makala yenyewe iliona kile ambacho alichokikusudia. Kwa hiyo, taarifa ilikuwa hailingani na kichwa cha maneno cha taarifa ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, yeye alitaka wananchi wapate fursa ya kulikamata kombe lile. Kwa kweli kutokana na uzito au umuhimu pamoja na dhahabu iliomo kwenye kombe lile basi atayeruhusiwa kulikamata kombe lile ni Rais peke yake na sisi wengine tutakuwa mashahidi wa kushuhudia Rais amekabidhiwa kombe lile.

Miongoni mwa sababu nzito za kulileta kombe lile Zanzibar ni kwa sababu Zanzibar yupo Rais ambaye atakabidhiwa kulipokea kombe lile, vyenginevyo ingekuwa ni vigumu kidogo kulileta kombe lile hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi, yeye alishauri au aliuliza kwamba kutakufa na gari ya wazi ambayo italibeba kombe hili, ili kila mmoja alione.

Kweli inakuwepo gari ya wazi itayoletwa na *Copa Coca Cola*, ambao ndio wenyewe wanaoshughulikia ziara za kombe hili kwa hapa Tanzania. Kwa hivyo, litakapokuja hapa Zanzibar litaletwa gari hilo na kombe hilo litakuwa limewekwa nje na linaonekana na kila atayebahatika kuliona *(Makofi)*.

Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Spika: Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji alipiga makofi sana kwa ile *Associate Membership* cha *CAF*, lakini nadhani *CAF (Kicheko/Makofi)*.

Waheshimiwa Wajumbe, nadhani sasa taarifa tumeipokea basi nione kwamba taarifa imepokelewa, wale waliokubali wanyanyue mikono, waliokataa, taarifa imepokelewa *(Makofi)*.

SHUGHULI ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya ya Mwaka 2009

(Kusomwa mara ya kwanza)

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamwita Mhe. Waziri kwa kweli mswada uliopo mbele yetu ni mswada mkubwa ambao ni muhimu, lakini hali ya ukumbini tunaiona kama ilivyo. Kwa hivyo, ningewaomba tubaki, ili tufanye kazi hii na itakuwa jambo la ajabu sana kuja kufika pahala na kumwita Mhe. Waziri leo leo kwa sababu ya wajumbe wengi wamo ukumbini.

Kwa sababu hiyo basi niwaombe wale Waheshimiwa Wajumbe walioko nje kwa ajili ya kupata chai ni vyema kurudi, ili tushughulike na mswada huu ambao kama miswada mingine ilivyo una umuhimu wa pekee tena mkubwa, kwani unahusu masuala ambayo kwa kweli imekuwa ni janga kubwa katika nchi yetu kama vile ilivyojanga kwa maeneo mengine ya jirani na karibu duniani kote. Kwa hivyo, tuhakikishe kwamba tunauchangia vizuri, ili tuone hatimaye tunafikia pale tutakapoona inafaa juu ya mswada huu.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo sasa namuomba Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kuja kuwasilisha mswada huo *(Makofi)*.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya Nam. 16

mwaka 2003 na Kutunga Sheria Mpya ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya hapa Zanzibar.

Kwanza napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukurani zangu za dhati kabisa kwa Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, kwa ushirikiano wao mkubwa walioutoa katika kuupitia na kutoa maoni yao kwenye mswada huu.

Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar ni Sheria inayohusu suala la Kuzuia Utumiaji, Uingizaji na Usafirishaji wa Dawa Haramu za Kulevya hapa Zanzibar (*Prevention of Illicit Traffic in Narcotic and Psychotropic Substances*). Sheria hii ilipitishwa na baraza la Wawakilishi tarehe 23 Oktoba mwaka 2003 na kutiwa saini na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 3 Juni mwaka 2004.

Mhe. Spika, madhumuni ya wakara huu ni kufuta Sheria ya Nam. 16 mwaka 2003 ya Dawa za Kulevya Zanzibar na Kutunga Sheria Mpya ya Madawa ya Kulevya, utekelezaji wa sheria hapo awali umeonekana kuwa na mapungufu mengi na baadhi ya vipengele kupitwa na wakati.

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia *Secretariat* ya Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar, iliyoainishwa kwenye sheria hiyo ya awali iliweza kupitia maeneo mbali mbali na kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya sheria hiyo.

Aidha wizara iliweza pia kupata michango kupitia warsha na semina kutoka kwa wadau wengine waliomo katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya, kutoka taasisi mbali mbali za serikali na zisizo za kiserikali (*NGO's*) na hatimaye Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, kuhusu muhtasari wa maeneo ya marekebisho mfumo wa vikao vya tume. Sheria hapo awali ilishindwa kubainisha mfumo wa uendeshaji wa vikao vya Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya hapa Zanzibar, hivyo kupelekea vikao vya tume kutokuwa na uratibu mzuri au mwafaka kisheria wa uendeshaji wa vikao vyake.

Aidha vikao vya Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya hapa Zanzibar imependekezwa hivi sasa kufanyika mara nne kwa mwaka.

Mhe. Spika, kuhusu muundo wa tume. Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar ulioainishwa kwenye sheria hiyo iliyochini ya Mwenyekiti wake Mhe. Waziri Kiongozi na Katibu wake ambaye ni Katibu Mkuu ambaye ni Katibu Mkuu aliyechini ya Afisi ya Waziri Kiongozi.

Kwa hivyo, imeonekana kukosa kiungo hasa ukizingatia kwamba *Secretariat* ambayo ndiye mtendaji mkuu wa kazi za tume hiyo, iko Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii chini ya Mwenyekiti wake ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Mhe. Spika, Katibu wa *Secretariat* hiyo ambaye alikuwa ni Mkurugenzi wa Idara ya Kupambana na Madawa ya Kulevya wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Kwa nia ya kuipa nguvu tume, basi mfumo pamoja na muundo wa tume sasa umechukua sura itakayomwezesha Mwenyekiti wa Tume kuweza kupata taarifa za kila siku za *Secretariat*. Kwa mantiki hiyo wadhifa mpya wa Mkurugenzi Mtendaji umependekezwa ambaye atakuwa Katibu wa Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar, ambaye pia atakuwa ndiye mwenyekiti wa *Secretariat*.

Mhe. Spika, kuhusu Kamati za Ufundi, kwa lengo la kuongeza uwajibikaji na utendaji kazi kuwa na ufanisi zaidi. Tume itaanzisha Kamati za Ufundi, yaani *Technical Committees* ambazo zitakuwa na majukumu ya kushajihisha pamoja na kuchochea utekelezaji wa kazi za kila siku za tume juu ya suala zima la mapambano ya dawa za kulevya, ambayo matumizi yake yamekuwa yakichangia katika ongezeko la maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI.

Kuhusu muundo wa *Secretariat*, kwa nia ya kuifanya *Secretariat* ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar kuwa ya wajibikaji na kuitendaji zaidi. Mhe. Spika, ni wadhifa wa Mkurugenzi Mtendaji ambaye atakuwa ni Mwenyekiti wa *Secretariat* hiyo, atayekuwa na watendaji mwafaka tena wa kudumu ambao watawajibika moja kwa moja kwa Mkurugenzi Mtendaji, ambaye kwa mujibu wa mapendekezo haya atakuwa ndiye Mwenyekiti wa *Secretariat*.

Aidha Mkurugenzi Mtendaji ataweza kuunda kamati mbali mbali zitakazojumuisha taasisi za serikali na zisizo za kiserikali, ambazo kwa njia moja au nyengine zitasaidia kwenye mapambano dhidi ya dawa za kulevya na UKIMWI Zanzibar.

Mhe. Spika, kuhusu makosa ya kimaandishi, kweli kumekuwepo na makosa ya kimaandishi, yaani *spelling*, ambayo katika baadhi ya maeneo yalishindwa kutoa maana halisi iliyokusudiwa ndani ya sheria hiyo ya awali. Kwa hivyo, upembuzi wa kina wa maeneo hayo umefanyiwa kazi kwa lengo la kusahihisha dosari hizo.

Kuhusu ufafanuzi wa vipengele. Kwa nia njema ya kuimarisha Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar kumefanyika pia uingizaji wa istilahi

(*terminologies*) mpya, ambazo zimepelekea kufanyika kwa ufafanuzi na maana ya *definitions* ya istilahi hizo.

Mhe. Spika, kuhusu makosa na adhabu. Kwa kweli kumekuwa na malalamiko ya mara kwa mara kwa aina za adhabu zinazotolewa kwa makosa ya dawa za kulevya hapa Zanzibar. Kwa sababu adhabu iliyokuwepo hapo awali ya makosa ya dawa za kulevya imeonekana kupitwa na wakati na watuhumiwa wamekuwa wakikwepa adhabu mbali mbali zikiwemo za kifungo kwa urahisi zaidi. Kwa hivyo, kiwango cha adhabu na faini zimeongezwa.

Kuhusu suala la ufuatiliaji na upekuzi. Mhe. Spika, mbinu za ufuatiliaji na upatikanaji wa taarifa za dawa za kulevya kwa watuhumiwa zimeimarishwa na kuwekwa wazi kwenye mapendekezo ya sheria hiyo.

Hali hii inakwenda sambamba na miongozo ya kijitelensia ya upandikizaji wa maafisa na raia wema katika mitandao na kuongeza wigo wa kufuatilia watuhumiwa, yaani *control delivery trap* kwa upana zaidi ndani ya Mitandao hiyo ya Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya. Hivyo, kuongeza udhibiti pamoja na kusaidia katika kuvunja mitandao hiyo.

Mhe. Spika, kuhusu kanuni, miongozi na taratibu za uchunguzi wa *sample* na viwango vya dawa za kulevya. Kanuni zinazohusu viwango vya madawa ya kulevya zimeainishwa na pia miongozo ya uchukuaji *sample* za kufanyia uchunguzi wa kuzitambua na kudhibitisha aina tofauti za dawa za kulevya, vikiwa ni vielelezo vinavyodhaniwa au kushakiwa kuwa ni miongoni mwa dawa zinazodhibitiwa. Kanuni na miongozo hiyo haikuainishwa na kutolewa ufafanuzi katika Sheria ya Madawa ya Kulevya ya hapo awali.

Mhe. Spika, kuhusu udhibiti wa *chemicals* bashirifu. Kwa kweli *Chemicals* Bashirifu ni zile chemicals ambazo kwa njia moja au nyengine zinaweza kutumika kutengenezea dawa za kulevya, baadhi ya *chemicals* hizo ni zile zinazotumika viwandani na dawa nyengine za matumizi halali kwa mwanadam.

Aidha upo uwezekano wa matumizi haramu ya *chemicals* hizo hapa nchini, kutokana na ukosefu wa mfumo wa kudhibiti kiasi kinachoingizwa na kujua kama *chemicals* hizo zinatumika kulingana na makusudio yaliyoorodheshwa katika uingizaji wake. Mhe. Spika, orodha wa *chemicals* hizo umetayarishwa na kuingizwa ikiwa ni sehemu ya mapendekezo hayo katika sheria hii.

Mhe. Spika, matokeo ya marekebisho ni mategemeo ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na wadau mbali mbali wa mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini, kwamba waraka umependekeza sheria hii utakapopitishwa

utasaidia kwa kiasi kikubwa, katika kukabiliana na matatizo ya utumiaji na uingizaji haramu wa dawa za kulevya hapa nchini.

Matumizi ya dawa za kulevya yamekuwa yakiathiri vijana ambao ni tegemeo la taifa na pia kuchangia kwa kiasi kikubwa maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI, magonjwa ya akili, vifo na hata makosa ya jinai.

Hitimisho Mhe. Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, inapenda kutanguliza shukurani kwa Wajumbe wote na kuwaomba kuujadili waraka huu kwa nia ya kuuimarisha na kuyafanya mapendekezo haya kuwa mazuri zaidi ambayo yanaweza kutekelezeka. Kwa kweli ni muhimu maamuzi yatolewe, ili kupunguza athari mbali mbali zinazoweza kujitokeza katika jamii kutokana na matumizi ya madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kutoa maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya Nam. 16 mwaka 2003 na Kutunga Sheria Mpya ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa ya *Narcotic* na aina za *Psychotropic* na Utekelezaji Masharti ya Mikataba ya Kimataifa Juu ya Madawa Haramu ya Nakotiki na Saikotropiki na Mambo Yanayohusiana Nayo.

Mhe. Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Azza Wajalla*, kwa kunijaalia kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu nikiwa na afya njema, kwa ajili ya kuwasilisha mapendekezo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, katika Mswada wa Sheria ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya na Kuweka Masharti ya Uzuiaji Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Nakotiki na Aina za Saikotropiki na Utekelezaji Masharti ya Mikataba ya Kimataifa Juu ya Madawa Haramu ya Nakotiki na Saikotropiki na Mambo Yanayohusiana Nayo.

Mhe. Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa ya awali kuwasilisha taarifa ya kamati yetu kuhusiana na mswada huu.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Zanzibar pamoja na watendaji wake wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa kuwasilisha mswada huu muhimu mbele ya kamati, ili ujadiliwe kwa lengo la kutungwa Sheria mpya inayohusiana na Madawa ya Kulevya Zanzibar na hatimaye uwasilishwe mbele ya Baraza la Wawakilishi kwa kupata baraka na michango ya Waheshimiwa Wajumbe kwa lengo la kuuimarisha zaidi.

Vile vile napenda kuwashukuru tena kwa kutupatia mafunzo ya siku moja ya kuutolea ufafanuzi mswada huu kabla ya kujadiliwa Barazani, ili Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili, waujadili mswada husika kwa umakini zaidi na hatimaye watoe mchango au maoni yatakayokubalika mbele ya Baraza lako tukufu na wananchi kwa ujumla.

Mhe. Spika, kwa kweli nawashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wote wa kamati hii kwa ushirikiano wao mkubwa waliouonesha wakati wa kuupitia na kuujadili mswada huu, kwa kutoa maoni yao yaliyokuwa na shabaha ya kuimarisha Mswada wa Sheria hii. Naomba niwatambulishe Wajumbe wa kamati yetu kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Ali Suleiman Ali	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Ame Mati Wadi	-	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Abubakar Khamis Bakary	-	Mjumbe
4.	Mhe. Ali Mzee Ali	-	Mjumbe
5.	Mhe. Ali Haji Ali	-	Mjumbe
6.	Mhe. Mohamed Ali Salim	-	Mjumbe
7.	Mhe. Haji Faki Shaali	-	Mjumbe
8.	Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	-	Mjumbe
9.	Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak	-	Mjumbe
10.	Mhe. Salim Abdalla Hamad	-	Mjumbe
11.	Mhe. Raya Suleiman Hamad	-	Mjumbe
12.	Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu
13.	Ndg. Asma Ali Kassim	-	Katibu

Mhe. Spika, vijana wetu wengi hivi sasa wanajiingiza katika utumiaji wa madawa ya kulevya, jambo ambalo litapelekea hasara kubwa kwa Taifa letu. Hii ni kutokana na kuwa, nchi itapoteza nguvu kazi ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu baadaye.

Aidha, madawa ya kulevya huwafanya watumiaji kupungukiwa na nguvu za kimwili na huku wakiwa na mahitaji ya ziada ya kifedha. Jambo ambalo husababisha wengi kati ya watumiaji hawa kujitumbukiza katika vitendo

viouvu kama vile wizi na ujambazi na kupelekea kuhatarisha usalama wa maisha yao na jamii kwa ujumla.

Mhe. Spika, matumizi ya madawa haya yanapelekea ongezeko la maambukizi ya ugonjwa hatari wa UKIMWI hususan kwa wale wanaotumia madawa ya kulevya kwa njia ya kujidunga sindano.

Mhe. Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ililazimika kuupitia Mswada huu wa Sheria siku tatu mfululizo. Hii ni kutokana na kuwa:-
Kwanza, mswada uliowasilishwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa wakati ule ulikuwa wa Kiswahili pekee. Jambo hili lilisababisha usumbufu mkubwa kwa kamati hii wakati wa kuujadili na kuupitisha mswada husika.

Hivyo, kamati ililazimika kupatiwa tafrisi ya Kiingereza ya mswada husika ili mswada huu ujadiliwe kwa ufasaha zaidi kama kifungu cha 87(2) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kinavyoelekeza.

Mhe. Spika, mara nyingi baadhi ya vifungu kwenye Mswada wa Kiswahili huwa havieleweki na Waheshimiwa Wajumbe hulazimika kufanya rejea **(***reference***)** katika Mswada wa Kiingereza ili kuleta tija kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Spika, endapo Miswada ya Sheria itatangazwa na kuwasilishwa katika Afisi ya Baraza la Wawakilishi kama Kanuni ya 78(2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi – Zanzibar, Toleo la 2007 kinavyoelekeza. Nathubutu kusema kuwa itawasaidia Waheshimiwa Wajumbe kuzidi kutoa michango na maoni mazuri yatakayokubalika mbele ya Baraza lako tukufu na kwa wananchi kwa ujumla. Hii ni kutokana na kuwa Waheshimiwa Wajumbe watakuwa wamepata muda mzuri wa kujiandaa kwa kufanya utafiti kuhusiana na mswada husika, pia kupata michango kwa wadau mbali mbali kwa lengo la kuuimarisha mswada huo.

Mhe. Spika, aidha, kuwasilishwa miswada hiyo kwa wakati itaiwezesha Afisi ya Baraza la Wawakilishi kupanga ratiba ya shughuli zake kwa umakini zaidi na sio kwa kubahatisha. Hivyo, kamati yetu inaishauri Serikali kuandaa Miswada ya Sheria mapema ili kuondosha usumbufu kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili sambamba na kwa Watendaji wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi - Zanzibar.

Mhe. Spika, sababu ya pili iliyopelekea kamati yetu kukutana kwa kipindi hicho ni kutokana na kuwa, misamiati iliyotumika katika mswada huu ni ya kitaalamu. Hivyo, pamoja na kuuchangia mswada huo Wajumbe wa Kamati hii walihitaji kupata ufafanuzi zaidi kutoka kwa wataalamu ili wapate kuufahamu

mswada huo kwa umakini zaidi na hatimae waweze kutoa maoni sahihi yatakayosaidia kuimarisha mswada huo.

Mhe. Spika, wakati kamati ilipoupitia Mswada huu wa Sheria, Wajumbe walipendekeza baadhi ya marekebisho kwa madhumuni ya kuimarisha zaidi.

Mhe. Spika, Kamati yetu imehisi Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Kudhibiti Madawa ya Kulevya, iliyoelezwa kwenye kifungu cha 4 cha mswada huu ina wajumbe wengi. Hivyo, ili kupunguza gharama za matumizi zisiso za msingi kwa serikali, kamati ilishauri tume hii kuwa na wajumbe tisa. Wajumbe wenyewe ni kama wafuatao:

1.	Waziri Kiongozi	Mwenyekiti
2.	Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii	Mjumbe
3.	Waziri anayehusika na Elimu	Mjumbe
4.	Waziri anayehusika na Vijana	Mjumbe
5.	Waziri anayehusika na masuala ya Sheria	Mjumbe
6.	Waziri anayehusika na Tawala za Mikoa	Mjumbe
7.	Mkurugenzi wa Mashtaka	Mjumbe
8.	Mufti wa Zanzibar	Mjumbe
9.	Mkurugenzi Mtendaji	Katibu.

Mhe. Spika, katika kifungu hiki cha mswada kamati pia, ilipendekeza sifa za Mkurugenzi Mtendaji, ili kuziba mwanya wa kuchaguliwa au kuteuliwa mtu asiyekuwa na sifa za kushika madaraka hayo na kupelekea tume pamoja na sekreterieti kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Hii ni kutokana na kuwa Mkurugenzi Mtendaji ni kiungo muhimu kwani ndiye Katibu wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Kudhibiti Madawa ya Kulevya, pia ni Mwenyekiti wa Sekretarieti.

Mhe. Spika, sambamba na maelezo yangu haya, kamati yetu pia ilipendekeza Wajumbe wa Sekretatieti ambao ni:-

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Idara ambaye ni Mwenyekiti
2. Mjumbe kutoka Kitengo cha Polisi cha Madawa ya Kulevya
3. Mjumbe kutoka Afisi ya Mkurugenzi wa Mashataka
4. Mjumbe kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu
5. Mjumbe kutoka Custom Prevention Services
6. Mjumbe kutoka Afisi ya Mkemia Mkuu
7. Mwanasheria wa Wizara husika
8. Mjumbe kutoka Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali
9. Mratibu wa Idara ya Madawa ya Kulevya ambaye ni Katibu”

Mhe. Spika, tulipendekeza Wajumbe hawa kwa kuwa tumehisi ndio wadau wakubwa wa masuala ya madawa ya kulevya. Hapa simaanishi kuwa taasisi nyengine hazihusiki kupambana na kadhia hii, la hasha! isipokuwa, tulifikiria sana juu ya kubana matumizi kwa Serikali yetu. Mhe. Spika, iwapo tutapendekeza kila Taasisi – Zanzibar itoe Mjumbe basi Serikali itatumia gharama kubwa. Lakini pia sekretatieti inaweza kushindwa kutekeleza kazi zake kama zilivyoelezwa kwenye kifungu cha 7(2) cha mswada huu ipasavyo kutokana na idadi kubwa ya wajumbe, kwani kila mmoja atakuwa na uoni wake juu ya jambo fulani, ingawa wahenga walisema ”kwenye wengi kuna mengi”.

Mhe. Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ilipendekeza kufutwa kwa baadhi ya vifungu. Hii ni kutokana na kuwa baadhi ya vifungu vinakwenda kinyume na dhamira ya Mswada huu wa Sheria pia vinatoa mwanya kwa mtu kutumia kivuli cha Serikali kwa maslahi yake binafsi. Kwa mfano, kifungu cha 15 cha mswada kinaipa mamlaka Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Kudhibiti Madawa ya Kulevya kutoa ruhusa na kusimamia ukulima au mchanganyiko wa sehemu yoyote wa mkoka, uzalishaji na utengenezaji wa kasumba kwa ajili ya serikali.

Mhe. Spika, kamati yetu haikukubaliana na kifungu hiki kutokana na sababu nilizozieleza hapo awali. Aidha, kamati ilipendekeza kufutwa kifungu cha 16 cha mswada huu. Hii ni kutokana na kuwa tayari sheria imeshaeleza kuwa, kujishughulisha na madawa ya kulevya ni kinyume cha sheria. Hivyo, kamati imehisi hakuna haja ya kuwekwa kifungu hiki. Mhe. Spika, vifungu vyengine vilivyopendekezwa kufutwa na kamati vinapatikana kwenye waraka wetu wa mapendekezo ya marekebisho.

Mhe. Spika, kwa kuwa mswada unatumiwa pia na wananchi wa kawaida kamati imeona sio busara kutumika kwa misamiati ya kitaalamu ambayo haifahamiki sana na jamii. Hivyo, ili kuondosha usumbufu kwa wananchi kwa kuangalia Kamusi kila mara, kamati ilipendekeza kuwa yale maneno yaliyoandikwa kwa Kiingereza yaandikwe kwa Kiswahili kwa kuwa maneno haya yanapatikana kwa Kiswahili. Baadhi ya maneno hayo ni kama vile neno **”**Protokali**”** linalopatikana katika ukurasa wa 107 wa mswada. Kamati ilipendekeza lisomeke ”Mkataba wa Nyongeza” kwa madhumuni ya mswada huu. Halkadhalika, neno **”**waranti**”** lililojitokeza kwenye kifungu cha 33 cha mswada lisomeke ”hati ya upekuzi”. Marekebisho mengine ya maneno kama haya yanapatikana kwenye waraka wetu wa mapendekezo ya marekebisho.

Mhe. Spika, kamati yetu ilipendekeza baadhi ya makosa kuongezwa adhabu na mengine kupunguzwa kutokana na uzito wa makosa yenyewe. Baadhi ya vifungu hivi ni kifungu cha 26(1) kamati ilipendekeza faini ya ”shilingi Milioni

40” badala ya ” shilingi Milioni 10”. Hii ni kutokana na kuwa mtu atakayetiwa hatiani chini ya kifungu hiki inaonekana ni sugu. Hivyo, ni busara atozwe faini kubwa ili aongeze pato la taifa, pia adhabu hii itamfanya awe raia mwema endapo ataitafakari.

Mhe. Spika, vifungu vya 45 na 46 vya mswada, kamati ilipendekeza viwekewe adhabu inayolingana kwani uzito wa makosa yanalingana.

Halikadhalika, kifungu cha 14 cha Mswada, adhabu iliyowekwa ni ”faini ya shilingi milioni 30 na kifungo cha maisha”. Kamati haikukubaliana na adhabu hiyo ya kifungo na ilipendekeza isomeke ”kifungo kisichopungua miaka 30”. Hii ni kutokana na kuwa kuweka adhabu kubwa kwa namna moja *”by implication***”** inamaanisha kuwa ni adhabu ya maisha.

Mhe. Spika, ingawa kamati yetu iliipongeza wizara husika kwa kuongeza adhabu mbali mbali, hata hivyo ilihisi kuwa kuna uwezekano mkubwa kwa watu wenye uwezo kutokutumikia kifungo kwa yale makosa yaliyowekewa adhabu ya faini. Hivyo, inazishauri Mahakama kutoa adhabu hizi kama Mswada wa Sheria hii unavyoelekeza.

Mhe. Spika, tulipendekeza pia, baadhi ya maneno yaliyotokana na makosa ya kiuchapaji. Baadhi ya maneno hayo ni neno **”**jingo**”** liliopo ukurasa wa 109 wa mswada kwenye aya ya tano kutoka chini, kamati ilipendekeza neno hilo lisomeke **”**jengo**”,** ukurasa wa 111, kifungu cha 3(2) mstari wa pili neno la tatu **”**Seerikali**”** lilipendekezwa lisomeke **”**Serikali**”**, ukurasa wa 120 wa Mswada kwenye kifungu cha 29 mstari wa tatu neno la sita **”**utvu**”** lilipendekezwa lisomeke **”**utovu**”**. Mhe. Spika, Marekebisho mengine ya maneno kama haya yanapatikana kwenye waraka wetu wa mapendekezo ya marekebisho.

Mhe. Spika, kabla sijawasilisha kwa ruhusa yako ningeomba uniruhusu na mimi kama mmoja wa wadau wakubwa wa masuala haya ambayo tunayapiga vita nichangie kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani.

Mhe. Spika, na mimi pia niipongeze serikali kuona kuja kwamba hivi sasa wakati umefika tukapambana na vita vikali tulivyokuwa navyo katika nchi yetu juu ya madawa ya kulevya. Mhe. Spika, dunia nzima hivi sasa inaelewa kwamba baadhi ya nchi kuna vita vya silaha, wenzetu hawa wasafirishaji wa madawa ya kulevya wana silaha nzito, wana majeshi wana kila kitu katika nchi zao hivyo huhatarisha usalama wa amani katika nchi jirani.

Mhe. Spika, mimi nasema hii sheria imekuja kwa wakati lakini nafikiri ni kwamba lolote la msingi la kupangwa kwa hatma ya watu huwa linataka subra, na subra hiyo ikifikia ndipo itolewe. Kwa hivyo, naipongeza serikali kwa

kuona hilo limefika wakati nzuri na ndio maana ikaamua kwamba hivi sasa imefika wakati kutoa mawazo yao juu ya kuharakisha mikakati ya kuweka sheria na kufanya kazi ili wahusika wachukuliwe hatua zinazofaa.

Mhe. Spika, tukiangalia kwenye adhabu kuna mambo ambayo yanajitokeza na tunasema kwamba demokrasia katika mambo yote huwa ni kukubaliana. Hapa kuna mambo yalikubaliwa kwamba kuna vifungo vya maisha, wengine tunakasema vipunguzwe viwe vya miaka 30. Mimi ndiye mmoja niliyesema kwamba mtu yeyote atakayekamatwa kwa makosa hayo basi afungwe maisha. Hilo nalipenda sana kwani kama watapatikana watu 3 au 4 itakuwa ni fundisho katika nchi, pia huenda yakapotea kabisa maovu kama haya yasiingie katika nchi.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wangu mimi napongeza sheria iliyokubaliwa ya kifungu cha maisha na mimi kwa upande wangu nayakubali hayo. Mhe. Spika, tukiwapata watu kama 3 tu wakikamatwa kwa makosa hayo basi itakuwa ni fundisho na sio rahisi kuingia wengine. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri mimi nimechangia kwa niaba ya wananchi wangu hili kama litakuwa linafaa lizingatiwe zaidi.

Mhe. Spika, jengine nataka niwaelekeze waheshimiwa wenzangu kwamba huu mswada tuuchukulie kama ni janga la taifa, na kama janga la taifa sote tunaguswa kwa upande mmoja au mwengine hakuna hata mwakilishi mmoja asiyeguswa kwa upande fulani. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuepushie kwa yule aliyekuwa hana mtu anayetumia madawa ya kulevya basi hakosi japo jirani yake atakuwa anatumia. Kwa hivyo, mimi nataka niseme kwamba jambo kama likimfika mmoja basi limetufika taifa zima. Mimi ningeomba sana waheshimiwa tuuchangie mswada huu na tuuangalie kwa jicho la huruma ili kuhakikisha tunampa msaada mkubwa Mhe. Waziri juu ya kuhakikisha anapata michangio mizuri ya kuufanikisha mswada huu.

Mhe. Spika, nakiri kwamba tatizo limejitokeza nakuomba Mhe. Spika kama nilivyoomba katika kamati yetu kwamba bado kuna haja ya kuletewa mapema katika Baraza lako tukufu. Miswada ikiletwa mapema Mhe. Mjumbe anaishiba na kuipitia vizuri ili kuhakikisha anachokuja kukizungumza hapa inakuwa ni rahisi.

Mhe. Spika, pamoja na hayo nampongeza Mhe. Waziri kupitia Baraza lako kwamba tumepata semina ya siku moja, ile semina imetupa ufafanuzi mbali mbali naamini ufafanuzi huo umetupa mawazo mengi yatakayotusaidia katika kuuchangia mswada huu kwa manufaa ya nchi yetu na vijana wetu.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nitalizungumza kwa ufupi ni kwamba sisi ni wana siasa na kama wana siasa basi sisi ndio walezi wa majimbo yetu. Nataka niseme kwamba mtu anatakiwa yeye kumuangalia yule anayekaa naye pale kwake na jirani yake yule aliyekuwa na kasoro kidogo basi aelekezwe juu ya mambo hayo ya madawa ya kulevya. Kwa hivyo, wanawaomba wenzangu tuwe walimu wa kuielimisha jamii katika maeneo yetu juu ya athari ya madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kwa niaba ya Kamati yangu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi na kwa niaba ya wananchi wangu wote wa Jimbo la Kwahani ambao wamenichagua na kunileta hapa niseme kwamba mimi mwenyewe naikubali asilimia mia moja hotuba hii. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (Mhe. Rashid Seif Suleiman): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa maoni ya kambi ya upinzani. Namshukuru Mwenyezi Mungu kutuweka katika uhai na uzima na tukiwa tupo katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, mswada huu kwa jina jengine unaweza kusema kuwa ni pambano au vita dhidi ya biashara na madawa ya kulevya, kwa ujumla wake hivi ni vita vigumu na vinahitaji kupatikana mambo mengi. Moja wapo ni kuwepo kwa sheria inayokwenda sambamba na hali ya nchi na hali ya biashara wenyewe.

Mhe. Spika, kwa kuwa sheria iliyokuwepo ya Nam. 16 ya mwaka 2003, lakini hali ya madawa ya kulevya hapa Zanzibar ni mbaya sana na haikupatikana nafuu yoyote sio kwa mapungufu ya sheria wenyewe tu, bali kuna mambo mengi ya kimaamuzi na kiutendaji ambayo yameipelekea Zanzibar kuingia katika kiunga uzi cha athari ya madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, karibu kila familia hasa maeneo ya miji na ukanda wenye hoteli za kitalii, vijana wetu wameathirika na kusononeka hali zinazowatia simazi kubwa wazazi wao na wengine hupoteza hata maisha yao kwa machungu ya kizazi. Wakati haya yakitokea katika baadhi ya nyumba nyingi wengine wanatanua eti wanafaidi faida ya mauzo yao.

Mhe. Spika, pamoja na mapungufu na kasoro zilizokuwemo katika ile sheria Nam. 16 ya 2003 kwa maoni ya wengi wanaona serikali haijakuwa na maamuzi ya kisiasa katika kupambana na usafirishaji na biashara ya madawa ya kulevya. Mbali ya hilo serikali haionekani kweli kuwa makini katika suala hili, kuna mianya mingi na unaweza kusema kuna uzembe au uzembe wa makusudi unaofanywa na kupelekea kudhorota kwa vita dhidi ya madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, sheria Nam. 16 ya 2003 ambayo leo ndio tunatarajia kufutwa na kuwekwa sheria hii mpya ilitumika kuanzia Septemba au Oktoba, 2004 zaidi ya mwaka mmoja tokea kupitishwa kwake. Mhe. Spika, hapo kweli serikali iko makini au sheria hii ilikuwa na mapungufu tokea haijaanza kutumika.

Mhe. Spika, ni jana tu tarehe 21-10-2009 katika kipindi cha maswali na majibu Mhe. Hamza Hassan Juma alijinata kuhusu kuwekwa choo maalum hapa Uwanja wa Ndege kwa kupambana na usafirishaji wa madawa ya kulevya. Akitilia mkazo namna walivyojipanga upya katika kutimiza haja ya huu mswada wa sheria mpya ambayo tunaijadili. Kwanza napenda nichukue nafasi hii kumshukuru sana kwa kuweza kutupatia taarifa hii, lakini napenda Mhe. Waziri atuambie kwa kweli hicho choo tokea kinunulie ni mwaka wa ngapi? Kwani kwa taarifa tuliyonayo sio cha mwaka huu wala mwaka jana. Je, huyo kigogo aliyezuia kufungwa choo hicho ameshatoa ruhusa au ameshasafisha fedha zake.

Mhe. Spika, tukiwa pale pale katika umakini wa serikali katika sheria Nam. 16 ya 2003 ilikuwepo Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Madawa ya Kulevya chini ya Uenyekiti wa Mhe. Waziri Kiongozi. Napenda nimuulize Mhe. Waziri je, tokea 2004 hadi hii leo imekutana mara ngapi?

Mhe. Spika, tume hii ilitarajiwa iwajibike kufafanua, kuboresha na kuratibu sera ya serikali iwapo haikutani huo umakini wa serikali uko wapi, hali inayoashiria kuwa yasemwayo yapo. Jambo jengine ambalo lingepaswa kuangaliwa kwa umakini kabisa ni jinsi gani unavyoandaliwa utaratibu wa kwamba sheria ziwe zinafanya kazi na kutekelezwa.

Mhe. Spika, katika kipindi kilichopita wako wengi waliozitupia lawama Mahakama kwa kukosekana kutiwa hatiani wengi wanaofikishwa hapo. Pamoja na udhaifu wa sheria inayotarajiwa kufutwa rushwa ilionekana kutawala katika vyombo hivi vya Mahakama. Hali hii ilishirikisha baadhi ya hata polisi waliokamata kwa kupotosha ushahidi.

Mhe. Spika, kambi ya upinzani inapendekeza kuwepo na Mahakama maalum inayohusiana na usafirishaji na matumizi ya kulevya ili hali ya kutoweka ushahidi unga wa aina hiyo ukaita sembe au saruji. Mhe. Spika, ucheleweshaji wa uchunguzi wa mambo hayo pamoja maabara iliyokuwa haikukamilisha ndio linalopelekea kubabaishwa ushahidi wenyewe.

Mhe. Spika, kupitia mfuko wa udhibiti wa matumizi mabaya ya madawa ya kulevya katika kifungu cha 12 cha mswada huu ni lazima Maabara ya Mkemia

Mkuu iwezeshwe na kuyatarishwa kwa ajili ya kuzifanyia uchunguzi wa haraka na dharura vitu vinavyofikishwa hapo.

Mhe. Spika, katika uimarishaji wa hii Maabara ya Mkemia muda wa kufanyiwa uchunguzi kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 54 cha mswada huu baada ya kutumia neno haraka isomeke kwa muda wa uchunguzi ulingane na ule wa kimataifa utakaowekwa na mamlaka husika.

Mhe. Spika, jeshi la polisi ni chombo muhimu sana katika mapambano ya biashara hii haramu ya madawa ya kulevya. Hata hivyo, ni lazima zichukuliwe hatua za dharura kufanya kazi hii. Mhe. Spika, hiki ni chombo cha muungano na mswada huu wa sheria ni wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hivyo kupitia huo mfuko uliotajwa katika kifungu cha 12 cha mswada huo jeshi la polisi liwezeshwe kupitia usimamizi wa sekreterieti ili mambo kadhaa ikiwemo ufuatiliaji, uajiri wa njia za kivuli na nyenginezo.

Mhe. Spika, kuna malalamiko kuwa wanapofuatilia nyendo za wale mapapa wanaoshukiwa katika biashara hii. Kwa maneno mengine wapo baadhi ya viongozi wanaowatishia polisi katika kufanya kazi zao hususan magwiji wa biashara hii wanapohusika.

Mhe. Spika, hali ya kulindana ilikuwa imeshamiri katika kipindi cha tokea 2004 baada ya kutumika sheria Nam. 16 ya 2003 ndio sababu moja wapo iliyopelekea kuwa hali mbaya hivi sasa.

Mhe. Spika, ni kwamba ukweli usiofichika kuwa tatizo la madawa ya kulevya ni kwamba limeshapita kiwango cha kuweza kudhibitiwa. Mhe. Spika, huu ni wajibu ambao hatuwezi kuukwepa na tukijaribu kuukwepa ni hasara kubwa kwenye jamii, unga umo ndani ya jamii kama ulivyo ndani ya damu za vijana wetu na hauna faida zaidi ya hasara na kwa hivyo nguvu yetu ya pamoja inahitajika.

Mhe. Spika, jambo hili la madawa ya kulevya si la kuzungumzwa kwenye majukwaa ya kisiasa au warsha, bali ni lazima upatikane msukumo mpya wa kisiasa uwepo na uonekane na utokane na ngazi za juu za uongozi.

Mhe. Spika, vijana kwa masikitiko makubwa wanaendelea kuumia wamefikia mahali ambapo wao na wazee wao hawana matumani, licha ya hayo limezaa utapeli, wizi, udhuruaji na hata uporaji wa mali za watu. Je, tunangojea nini tena?

Mhe. Spika, kifungu cha 4 cha mswada huu kimeanzisha Tume ya Kitaifa ya Kuratibu Udhibiti wa Madawa ya Kulevya ambayo mbali ya kuwa Waziri

Kiongozi ndiye Mwenyekiti lakini mawaziri wengine saba. Mhe. Spika, tume hii ni kubwa mno ama tukubali sehemu ya Baraza la Mapinduzi asiyekuwa Rais lote lichukue jukumu. Njia nyengine ni kuwa mawaziri wasiozidi wanne na mwenyekiti wake akiwa ni Waziri Kiongozi ndio wawe mawaziri husika.

Mhe. Spika, mawaziri ambao wangepaswa kuwemo ni Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi, Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora, Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji na Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Spika, jambo jengine linalokwamisha utekelezaji wa sheria ya kutaifishwa mali haramu inayotokana na biashara na madawa ya kulevya ni kukosekana kwa utaratibu mzima wa kutaifisha katika misingi ya kisheria.

Mhe. Spika, ni dhahiri vita hivi vya kupambana na madawa ya kulevya vinapiganwa katika maeneo tofauti zikiwemo,

1. Kuchafua na kuharibu masoko ya madawa ya kulevya.

2. Njia za kinga zikiwemo zile za kuanzisha vikundi vya kiraia, kuelimisha jamii juu ya madhara na hatari ya kutumia madawa ya kulevya.
3.
4. Utekelezaji wa sheria zinazohusiana na mtandao na mlolongo wa kupatikana kwa madawa ya kulevya katika kufuatilia kwa kina mwenendo ya biashara hiyo pamoja na kupandikiza vivuli ndani ya mtandao huo.
5. kutoa huduma inayofaa na iliyoelekezwa kwa wale waathirika.

Mhe. Spika, kama kweli pana maamuzi ya kisiasa, mawaziri wengine wote watapaswa wafuate maelekezo kulingana na Wizara zao.

Kuhusiana na wajumbe wengine wa tume hii, kifungu (m) kisomeke mtu mwengine atakaeteuliwa na Waziri Kiongozi mwenye utaalamu na ujuzi maalum kuhusu myenendo ya biashara ya madawa ya kulevya.

Katika Muundo wa Tume kifungu (n) pamewekwa mtu mwengine yeyote ambaye atateuliwa na Waziri Kiongozi, lakini huyu anatakiwa awe ni mtaalamu katika fani hii.

Mhe. Spika, kifungu 3(a) na 4 kinazungumzia kuhusu sekreterieti. Hili si jina zuri, kwani linaonekana labda ni kazi za ndani tu, ni afadhali kingeitwa kitengo maalum cha Serikali cha kupambana na madawa ya kulevya ambacho wajumbe wake watatoka katika sekta mbali mbali zenye mahusiano na hayo

zikiwemo polisi, uhamiaji na kastam. Hii ndio inayopaswa kuita kamati ya kiufundi.

Mhe. Spika, kuundwa kwa kamati nyengine za ufundi na tume au Mkurugenzi Mtendaji kutaongeza urasimu tu na hali ya uajibikaji itazorota vile vile. Vita hivi vya kupambana na madawa ya kulevya vinapiganwa katika maeneo tofauti, zikiwemo kuchafua na kuharibu masoko ya madawa ya kulevya, njia za kinga zikiwemo zile za kuanzisha vikundi vya kiraia, kuelimisha jamii juu ya madhara ya hatari ya kutumia madawa ya kulevya, utekelezaji wa sheria zinazohusiana na mtandao wa mlolongo wa kupatikana kwa madawa ya kulevya katika kufuatilia kwa kina myenendo ya biashara hiyo pamoja na kupandikiza vivuli ndani ya mtandao huo, kutoa huduma inayofaa na iliyoelekezwa kwa walioathirika.

Mhe. Spika, tukichukua kipengele cha 4 cha maelezo hayo ya juu, ni wazi kuwa kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kutibiwa hawa wanaowaita wateja. Namuomba Mhe. Waziri atueleze Wizara yake imefikia wapi juu ya kupatikana kwa kituo hiki cha kutibia wateja akifahamu kuwa hivi sasa tunakaribia kuingia mwaka 2010 na suala hili limo katika ilani ya uchaguzi ya CCM.

Mwisho kabisa napenda nitoe tahadhari kwa Serikali juu ya kifungu cha 32 cha mswada huu juu ya uvamizi na kuingia wakati wa dharura. Kwa kuwa matumizi ya madawa ya kulevya ni janga kubwa na vita vyake ni vizito duniai nzima, Serikali isije ikakitumia kifungu hiki au chengine chochote kuwadhibiti viongozi au wanachama wa Chama cha Upinzani au kuwalinda wale wa chama tawala, kuzitumia vibaya kisiasa sheria hii itapelekea athari kubwa zaidi na vita zidi ya madawa ambayo hutegemea pia taarifa kutoka kwa watu wema vitakuwa haviwezekani tena.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Kabla sijamuomba mmoja kati ya Waheshimiwa Wajumbe waliyoomba, naomba nitoe tangazo moja dogo. Kuna mwenzetu mmoja alipokwenda kujisaidia katika sehemu ya msalani upande wa wanawake, amesahau saa ya mkononi. Kwa hivyo, anaombwa mwenye saa hiyo amuone ndugu yetu Ubwa, ndiye ambaye anaweza akamkabidhi saa yake. Nashukuru.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia asubuhi ya leo kuwepo hapa katika Baraza letu tukufu kwa madhumuni ya kuuchangia mswada huu unaohusiana na masuala mazima ya madawa ya kulevya, mswada ambao ni muhimu sana kwa nchi yetu.

Pili nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii nami nikaweza kutoa michango yangu, lakini pia nimshukuru na kumpongeza Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na watendaji wake wote kwa kuwasilisha mswada huu muhimu. Pamoja na kwamba ni mswada unaoonekana umechelewa na hasa ukizingatia kwamba nchi yetu ipo katika janga kubwa sana la madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, kama yalivyo madhumuni ya mswada huu ambayo ni kufuta sheria ile ya zamani ya kuzuia usafirishaji haramu wa madawa ya kulevya sheria Nam. 16 ya mwaka 2003 na kuanzisha sheria mpya. Kwa kweli madhumuni ni mazuri na yanaweza yakasaidia matatizo mbali mbali ambayo yanaonekana sasa hivi yapo.

Mhe. Spika, mimi bado nimekuwa na wasi wasi na sheria hii mpya na jinsi ya utekelezaji wake na yale madhumuni ambayo yamekusudiwa. Kwa nini Mhe. Spika, nimesema nimekuwa na wasi wasi? Kwa sababu kabla ya sheria ya Nam. 16 ya mwaka 2003, kulikuwa na sheria ya aina hii ambayo nayo ilikuwa inafanya shughuli za aina hii hii ya kupambana na usafirishaji wa madawa ya kulevya hapa nchini.

Mhe. Spika, kama kabla ya sheria hii Nam. 16 utakumbuka kwamba katika enzi za utawala wa Awamu ya Tano ya Mhe. Dr. Salmin Amour Juma kuliwahi kukamatwa idadi kubwa ya madawa ya kulevya katika kiwanja chetu cha ndege cha Zanzibar. Nakumbuka waliwahi kushikwa wananchi wawili wenye asili ya ki-*Asia*, walikamatwa nayo. Lakini kutokana na udhaifu wa sheria ile kwa wakati ule, wananchi wale waliachiwa huru kutokana na udhaifu wa kisheria, nadhani hatimaye ndio kukafanywa marekebisho ikaanzishwa sheria hii ya Nam. 16 ya 2003.

Sasa hivi ni miaka sita tokea kufanywe mabadiliko, lakini pamoja na mabadiliko ambayo yamefanywa wakati huo wa mwaka 2003, lakini bado sheria hii imeonekana ina mapungufu makubwa. Mhe. Spika, inaonekana bado hatujawa makini katika suala zima la kudhibiti usafirishaji wa madawa haya haramu ya kulevya ama tunaweza kusema kwamba sheria hizi zinafanywa kwa makusudi.

Ni ukweli usiofichika kwamba wananchi wengi wa Zanzibar wanakosa imani na Serikali yao na kwa namna ya jinsi gani inavyoweza kushughulikia janga hili la taifa, ambapo nguvu kazi nyingi zinaonekana zinapotea. Kumekuwa na wimbi kubwa la vijana wetu mitaani ambao hujiingiza katika hatari hii ya kutumia madawa ya kulevya kwa kweli ni jambo la kusikitisha Mhe. Spika, kuona kwamba bado udhibiti wa jambo hili unaonekana si wa kuridhisha.

Mhe. Spika, wewe ni shahidi juzi wakati Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi alipokuwa akijibu swali hapa Barazani alielezea kwamba katika kipindi cha miezi 9 Januari hadi Septemba mwaka huu, kati ya watu 132 waliokamatwa kwa tuhuma za kukamatwa na madawa ya kulevya ambao walifikishwa mahakamani, ambapo kesi 47 zilizosikilizwa wameachiwa huru. Wote wameachiwa hutu ambapo ni sheria hii hii Nam. 16 ya 2003 ndio iliyokuwa ikitumika. Hakuna hata mshitakiwa mmoja aliyeweza kutiwa hatiani.

Mhe. Spika, kwa kweli hili ni jambo la aibu kwa vyombo vyetu, na ni jambo la aibu kwa wakati kama huu wa karne ya 21 ambapo kesi 47 ambazo zimepelekwa Mahakamani, idadi kubwa kama hiyo watu wote wanaachiwa. Mimi Mhe. Spika, naamini hata hao waliobakia mbao kesi zao hazijatolewa uamuzi na wao wataachiwa huru.

Mhe. Spika, sote tumeshuhudia kwa nyakati tofauti kesi za madawa ya kulevya zilivyovurugwa ili washitakiwa waachiwe huru na waendelee kuleta madawa haya ambayo kwa kweli yanaathiri sana nguvu kazi. Mtu utashitukia amekamatwa namadawa tena ndani ya tumbo! tunaoneshwa ndani ya vyombo vya habari kama televisheni, lakini baada ya muda mfupi utakuja kushitukia kwamba eti vifurushi vile vilivyokamatwa vilikuwa ama unga wa sembe au saruji. Jamani! Hatuoni hata aibu? Hivi kulikuwa na haja gani ya mtu yule kuweka vifuko vya saruji ndani ya tumbo lake wakati saruji inapatikana tele nje? Lakini huu unaonekana dhahiri ni uvurugaji wa makusudi wa vyombo vyetu ili kuona kwamba biashara hii inaendelea.

Kwa hivyo, mambo kama haya ndiyo yanayofikia pahala au wananchi wetu kuwa na kila aina ya sababu ya kuwafanya wasituamini. Wakati mwengine wanathubutu kusema kwamba biashara hii inafanywa na watu wakubwa. Ukiangalia mifano ambayo ipo utathubutu kufika pahala kusema kwamba ni kweli biashara hii inafanywa na watu wakubwa. Sasa hili ni jambo la aibu kwa nchi yetu na zaidi ukizingatia sasa hivi dunia imeelekea zaidi katika mapambano ya madawa ya kulevya, lakini katika visiwa vyetu inaonekana bado kuna uvurugaji wa makusudi juu ya jambo hili na huku tukiendelea kuona kwamba shughuli hii inaendelea kwa nguvu kubwa.

Mhe. Spika, biashara hii haifanywi kwa uficho hata kidogo, ni biashara ambayo iko wazi. Biashara ya madawa ya kulevya inafanywa wazi, utakapotembelea mitaa ya Kwahani, Miembeni, Malindi na maeneo mengine mengi utawakuta vijana waliojikusanya kwenye baraza za nyumba fulani wamekaa wamejipanga huku shingo zao zikining'inia kama vile kuku waliopatwa na maradhi ya mahepe. Kwa kweli ni jambo la kusikitisha, wako mitaani wamekaa kwenye

baraza shingo zinaning'inia. Wale ni dhahiri wanajulikana kwamba hawa wametumia kitu fulani na wako mtaani.

Vijana wale wala unga hawendi tu kukaa katika nyumba nyengine tu, kwa sababu zile nyumba zinakuwa zipo nyingi mtaani, lakini wote wanakaa katika nyumba moja hapo panaashiria nini? Panaashiria kwamba pale walipokaa ndipo penye biashara ile ambayo wao wenyewe wanaifatilia, hawawezi kutoka wakaja wakakaa kwenye nyumba yangu mimi kwa sababu sifanyi shughuli hiyo, lakini wanachagua pale pahala ambapo wao ile biashara yao au ile shughuli yao wanayoifuata pale wanafanikiwa. Sasa tuseme Mhe. Spika, kweli ndio inafanywa kwa Kificho au iko wazi wazi?

Mhe. Spika, mimi naamini kama Seikali itakuwa tayari kupambana na suala hili au kukomesha jambo hili basi inawezekana. Na kwa sababu kuna mifano mbali mbali ambayo inatokea na pale Serikali inaposimama kidete katika kupiga vita jambo fulani inawezekana, iweje leo tushindwe kupiga vita haya madawa ya kulevya? Ni dhahiri kwamba bado hatujawa tayari katika jambo hili.

Mhe. Spika, kama Serikali haitosimama kidete na tukawa na dhamira ya kweli ya kupamba na jambo hili basi nchi yetu itaangamia. Tutakosa nguvu kazi za baadae kwa sababu vijana wetu watakuwa wanajiingiza, watakuwa hawana nguvu, lakini pia maambukizi ya virusi vya UKIMWI yataongezeka. Kwa sababu moja kati ya njia wanayoitumia wateja ni kudungana sindano, sindano moja wanaweza kudungana watu sita mpaka saba, pengine miongoni mwao mle wamo walioathirika lakini pia wanakuwa hawana hadhari juu ya kujikinga na jambo hili. Kwa hivyo, maambukisi ya virusi vya UKIMWI yataongezeka. Kwa hivyo, jambo hili kwa kweli kama tuko *serious* tupambane nalo kweli kweli.

Mimi sioni kama litakuwa tatizo, wala sioni kama ni kwenda kinyume na haki za binadamu kuwashika wale vijana ambao tayari tunaona shingo zao zinaning'inia na kuwapeleka katika vipimo na kuangaliwa kama wametumia madawa au hawajatumia madawa. Akigundulika kwamba huyu mtu damu yake tayari imeshaathirika na madawa basi akafikishwa Mahkamani moja kwa moja. Mimi sioni kama tutakwenda kinyume na haki za binadamu. Kwa sababu vijana hawa wamo na wako mitaani na wanaonekana na dalili zote zinaonekana, sasa kwa nini wasichukuliwe wakapelekwa katika vyombo wakapimwa , wakaangaliwa damu zao na kutizamwa, ikigundulika huyu katumia basi akapelekwa katika chombo cha sheria na sheria ikachukua mkondo wake.

Mhe. Spika, ninaamini tukifanya hivyo basi hata vile vikundi vinavyojikusanya mle kwa ajili ya shughuli ile vitapungua kwa sababu wataona sasa Serikali iko *serious* katika kupambana na jambo hili, lakini sasa hivi hawajifichi wako open na tunawaona, kila mmoja akiwaona wale anajua hawa wametumia kitu fulani ni tofauti na bangi.

Mhe. Spika, mvuta bangi yeye si rahisi kumfahamu, lakini mtumiaji wa madawa ya kulevya akishatumia utamuona na hana kificho, utamuona kwamba huyu keshatumia kitu hiki. Kwa hivyo, Mhe. Spika, jambo hili ni lazima tulizingatie na tulione umuhimu wake, tujue athari zake na tuone kwamba taifa hili linakwenda pabaya.

Mswada huu wa sheria umemtaja Mkemia Mkuu wa Serikali, ambao umesema kuwa ni Mkemia yeyote aliyeteuliwa na Waziri kwa ajili ya sheria hii na kanuni zake. Lakini nimuulize Mhe. Waziri Mkemia huyu ambaye ametamkwa, ambaye unamteuwa wewe na yule Mkemia Mkuu wa Serikali ni tofauti au ndiye huyo huyo Mkemia Mkuu wa Serikali ambaye ametajwa katika sheria hii, anayeelezwa kuwa atakuwa anatumia sheria hii? Je, yeye atakuwa anafanya kazi hizi tu kwa mujibu wa kanuni zake? Hapo ningehitaji kidogo kuja kupata maelezo kama ni Mkemia Mkuu wa Serikali au ndiye Mkemia huyu tu ambaye atakuwa anashughulika na kitendo cha madawa ya kulevya?

Mhe. Spika, kifungu cha 55 cha mswada huu kinasema kwamba, "kutakuwa na Mkemia wa Serikali atakaeteuliwa na waziri", lakini haikuelezwa sifa za Mkemia huyo. Kwa kwali kazi za Mkemia ni kazi za kitaalamu, zinahitaji kuwa na Mkemia ambaye amebobea, mwenye sifa, na hapa Mhe. Spika, ndipo penye matatizo. Kwa sababu unapomuweka mtu ambaye hana sifa hususan shughuli hizi za kitaalamu, basi tutakuwa hatuna tunalolifanya hata moja, na ndio maana wakati mwengine utamkuta Mkemia huyo leo anasema hili na kesho anasema hili, leo anasema mchele mbovu, kesho anasema mchele mzima! Lakini kama tutampata Mkemia aliyebobea, ana vyombo, ana utaalamu, maana yake shughuli zetu hizi zitakwenda vizuri na tutakuwa hatupati tabu.

Sasa tungemuomba Mhe. Waziri huyo Mkemia utakaemteuwa ,huyo basi awe na sifa za ukemia, ripoti zake ziwe za uhakika zisiwe za kubahatisha, asiwe na kauli mbili leo hili kesho hili. Ningeomba Mhe. Spika, Mkemia aelezwe sifa zake sio kuchukua chukua mtu tu, tukamuweka pale tukamwita Mkemia Mkuu na huku shughuli zetu zikawa zinaharibika.

Mhe. Spika, kuna tume humu ambayo imeundwa ambayo tumeita Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Madawa ya Kulevya, ambayo tume hii ina mlolongo wa Waheshimiwa Mawaziri, mwanzo iliitwa Tume ya Mawaziri lakini kamati nadhani imebadilisha kwenye marekebisho yao. Lakini ina mlolongo wa

mawaziri wengi tu. Hebu Mhe. Waziri utapokuja kufanya majumuisho tushibishe wajumbe wako, tushibishe tushibe kweli kweli, kwa nini tume hii imekuwa na mawaziri wengi mno wakati mawaziri wetu wana kazi nyingi, shughuli nyingi, wanasafiri huku na kule, leo tunapowapa kazi hii nzito yenye matatizo, yenye janga la nchi yetutunahisi tume hii inaweza ikafanya kazi vizuri.

Sasa hivi Mhe. Spika, tumeshaanza kuogopa, kwa sababu tumeanzisha sheria mbali mbali, mambo mbali mbali lakini tunaona bado mambo yetu hayaendi vizuri. Sasa tumeshakuwa na wasi wasi, Waswahili wanasema unapomkanyaga nyoka, basi ukikanyaga ukuti unashituka. Sasa tumeshaanza kushituka na kwa sababu tunaona mambo yetu haya hayendi vizuri tuna wasi wasi na tume hii imekuwa na wana siasa wengi watendaji tena mawaziri ambao wana kazi nyingi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hebu tupe sababu za msingi hasa ambazo zimepelekea kuwa na mawaziri wengi ambao watakuwemo katika tume hii. Tume ambayo tungetarajia kwamba itaweza kusimamia shughuli zetu imepewa kazi za kusimamia mambo mengi humu wakati na wao huku watakuwa wanasimamia sera za kudhibiti madawa ya kulevya. Lakini huku wana sera zao za serikali za kusimamia wizara zao, huku huku watakuwa na sera zao za kusimamia vyama vyao. Sasa Mhe. Waziri hebu tushibishe kuona kwamba kweli kuna haja ya kuwa na mlolongo mkubwa kama huu wa Waheshimiwa Mawaziri kwa ajili ya kufanya shughuli hii.

Mhe. Spika, kifungu cha 4 (5) kinasema kwamba “Mhe. Rais kwa amri iliyotangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali atamteua Mkurugenzi Mtendaji”.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa najiuliza ni amri ipi hiyo iliyotangazwa kwa sababu humu katika Mswada hatukupata maelezo kwamba mkurugenzi huyu atakuwa ana sifa gani. Pengine humu kwenye Gazeti Rasmi la Serikali limetoa hizo sifa ambapo Rais atapata nafasi ya kumtangaza huyu mkurugenzi.

Mkurugenzi huyu kwa mujibu wa mswada huu atakuwa ni mtu mkubwa sana kwa sababu yeye kila wakati atakuwa yupo ofisini, tume hii itakutana mara nne kwa mwaka. Lakini mkurugenzi pamoja na sekretarieti yake watakuwa wao *full time* wapo pale ofisini wanaratibu shughuli hizi. Sasa ni lazima tuwe na mkurugenzi ambaye ana uwezo wa kufanya shughuli hizi. Pengine hii amri iliyotangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali itakuwa imeeleza, maana hapa pamejificha ficha.

Huko nyuma tulipokuwa tunapitisha Miswada hii tulikuwa tunaelezewa kwamba, Mhe. Rais atamtangaza mkurugenzi mwenye sifa hii na sisi wenyewe huwa tunaridhika kuona zile sifa ambazo zimewekwa kwamba sasa tutapata

mtu ambaye ni *competent* na zile shughuli ambazo anataka kuzifanya. Sasa hapa kidogo pamezongwa.

Kama nilivyotangulia kusema mwanzo tumekuwa tuna mashaka juu ya sheria za nyuma zilizopita na namna ya utekelezaji wake. Kwa hivyo, tunapozongwa namna hii kidogo tunakuwa na wasi wasi. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atutoe wasi wasi juu ya mkurugenzi huyu ambaye amri iliyotangazwa katika hilo Gazeti Rasmi la Serikali inasema labda kuna hivi na hivi, tuweze kujua na kupata kujenga imani juu ya mkurugenzi wetu huyu.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Mswada huu wa sheria inaonekana ni dhahiri kwamba kuna sera ya serikali ya kudhibiti matumizi mabaya ya biashara ya madawa ya kulevya. Utekelezaji wowote wa sheria ufanisi wake unaweza ukapatikana kutokana na sera zilizo bora. Sasa mimi Mhe. Spika, nilikuwa na wasi wasi, sera hii ambayo ilitandikwa huko nyuma ambayo ilizaa hizi sheria zilizotangulia inaonekana labda haikutandikika vizuri au ina mapungufu na ndio maana inazaa sheria zilizokuwa zina matatizo.

Mhe. Spika, wasi wasi wangu tutakuwa kila wakati tunabadilisha sheria. Tulikuwa na sheria nyuma, baada ya muda mfupi mwaka 2003 tukaunda sheria, tumeshafika mwaka 2009 tunaunda sheria lakini pengine sera bado inaonekana ni ile ile. Sasa kinachozaliwa kutokana na sera ile maana yake inaonekana sera ile ina mapungufu.

Mhe. Spika, hivi Mhe. Waziri hakuona haja ya kufanya marekebisho ya sera iliyopo juu ya udhibiti wa madawa ya kulevya. Mhe. Spika, kwa kweli mimi binafsi naona ipo haja kubwa. Pengine sera hii ya kudhibiti madawa ya kulevya inaonekana ina matatizo. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kwamba sera hiyo basi aitayarishe aiwasilishe hapa Barazani na sisi wenziwe basi tumsaidie. Kunaweza kuwa kuna mapungufu ambayo tunaweza tukatoa michango yetu kuboresha zaidi, ili sheria hizi zinazotungwa ziweze kusaidia katika suala zima la mapambano haya dhidi ya madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, kifungu cha 8 kinazungumzia juu ya tume kuwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi ripoti ya kila mwaka inayoelezea hali ya kitaifa na maendeleo yake kuhusu mapambano dhidi ya madawa ya kulevya na mapendekezo na maboresho yake.

Hili Mhe. Spika, mimi naliunga mkono kwa asilimia mia kwa mia kwa sababu suala hili la madawa ya kulevya ambayo ni dhahiri inaonekana ni tatizo la kijamii, basi ni busara kuwasilisha hapa kwa kila mwaka taarifa ya utekelezaji wa jambo hili. Sisi tukiwa ni wawakilishi wa wananchi basi tutaona ni namna

gani serikali inavyochukua hatua juu ya utekelezaji wa jambo hili, tutapata kutathmini maendeleo ya jambo hili.

Lakini tutakaposikia tu kwamba watu 132 wamepelekwa Mahakamani, watu 47 wameachiwa huru hawana mashtaka. Kwa kweli nafsi zetu pamoja na wananchi tunakuwa hatufurahi na tunaona kwamba hapa hapajawa na umakini katika jambo hili, wanaweza kuachiwa mmoja au wawili. Kwa hivyo, jambo kama hili kuwasilishwa hapa katika ukumbi kama huu kwa kila mwaka litatupa faraja. Kwa sababu tutafanya tathmini, tutajua na tutaona ni jinsi gani maendeleo ya jambo hili na jinsi gani serikali inavyopambana na hatua mbali mbali juu ya kudhibiti suala hili.

Mhe. Spika, kifungu cha 24 kinazungumzia adhabu kwa kusaidia kufanya kosa chini ya sheria hii. Mswada umeelezea kuanzia kifungu 24 (a) mpaka (d) juu ya namna mtu anavyosaidia kufanya kosa na adhabu ya huyo mtu ambaye anasaidia. Mhe. Spika, ni kweli kuna watu wanasaidia kufanya makosa. Mmoja ni yule anayepokea rushwa. Kwa mfano, ameshayashika madawa badala ya kumchukulia hatua kumpeleka katika vyombo vinavyohusika na hatimae Mahakamani basi anapokea rushwa. Anapokea rushwa maana yake anasababisha sasa kosa lile liendelee kutendeka.

Mhe. Spika, ukiangalia humu sheria haisemi moja kwa moja kwamba mtu wa aina hii ambaye anasaidia kufanya mambo kama haya, hilo ni moja nililolizungumza la rushwa lakini kuna mifano mingi. Anaweza kumtorosha mtuhumiwa, anaweza kumzuia pengine askari kufanya ukaguzi na mambo mengine. Lakini sheria haikueleza moja kwa moja kwamba mtu huyu atapewa adhabu gani, imesema tu kwamba ataadhibiwa kama vile mkosaji mkuu. Sasa mkosaji mkuu sijui yupi. Kuna mkosaji mkuu na mkosaji mdogo, lakini sheria imesema mkosaji mkuu.

Mimi pendekezo langu ni kwamba sheria hapa isitoe mwanya kwa sababu mwanya kama huu ambao tunautoa ndio hatimae tunatoa nafasi kwa watu sasa kuachiwa huru Mahakamani. Wenzetu Mahakimu wale wanakuwa wako makini sana, anatafuta njia ndogo ukiteleza unamkuta mtu yuko nje. Kwa hivyo, ni lazima sheria sasa hivi iwe ina-*cover* maeneo yote, tusiache nafasi kwamba huyu ni mkosaji mkuu.

Pamoja na kwamba Mswada unaelezea baadhi ya maeneo ambayo hayakutolewa adhabu, kwa hivyo adhabu yake itakuwa hivi na hivi. Lakini huyu naye anapaswa atajiwe adhabu yake kwamba mtu anayefanya kitendo kama hicho adhabu yake iwe moja, mbili, tatu sheria iwe wazi.

Mhe. Spika, kifungu cha 29 (1) kinazungumzia makosa yasiyo na dhamana. Mswada umeelezea kwamba "Bila ya kujali kitu chochote kilichomo katika kifungu hiki cha 29 (1) hakuna mtu atakayepewa dhamana wakati akisubiri kusikilizwa kwa kesi yake".

Mhe. Spika, ukiangalia maelezo ni mazuri kwamba hakuna dhamana ikatakayotolewa juu ya mshtakiwa kabla ya kesi yake kusikilizwa. Kwa maana hiyo, inaonesha dhahiri kwamba kesi yake inapoanza kusikilizwa tu basi pale dhamana yake itakuwa iko wazi, nilivyofahamu mimi.

Kwa kweli Mhe. Spika, dhamana ni haki ya mshtakiwa lakini kama tuko *serious* katika kupambana na jambo hili, basi mimi nadhani tuondoshe dhamana juu ya watuhumiwa kama hawa. Akishakuwa *suspect* na kufikishwa Mahakamani, hata kama kesi yake inaanza kusikilizwa basi kusiwe na dhamana juu ya mtuhumiwa huyu, aendelee kuwepo mpaka kesi yake itakapotolewa hukumu.

Kuna kesi za aina hii ambazo zinazungumzia jambo hilo kwa sababu tunataka kukomesha jambo, tunataka kufanya dawa ya jambo, mtuhumiwa unapomuacha nje matokeo yake sasa anapoteza ushahidi. Kama tunavyojua kwamba mambo haya yanafanywa na watu wazito na tuamini hivyo, wenye fedha, ushahidi unaweza ukapotea. Kwa hivyo, kama kweli tuko *serious* katika hili basi kusiwepo na dhamana ya aina yoyote kwa mtu ambaye tayari ametuhumiwa kwa mambo kama haya. Kesi yake iende akiwa ndani ili ushahidi usipotee. Nazungumza kama mwanzo dhamana ni haki ya kila mtu, lakini si kwa kesi za aina hii. Mhe. Spika, kesi hizi ni hatari sana na zinaweza zikatupotezea mambo mengi.

Mhe. Spika, jengine kwenye mswada huu kifungu cha 36 kinazungumzia zawadi na kinasema, "Tume inaweza kuidhinisha malipo ya zawadi kwa watu wanaotoa taarifa sahihi za kweli kuhusiana na makosa, ambazo taarifa hizi zinaweza zikasaidia kukamatwa kwa mkosaji".

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba matumizi haya ya madawa ya kulevya hapa visiwani yapo hadharani hayajifichi isipokuwa tunakuwa tuna kawaida ya kuoneana muhali. Pengine biashara ile inafanywa na jirani yako unachukiwa lakini huwezi kupenya ukenda ukasema jamani jirani yangu fulani anafanya hivi. Lakini sasa tuko katika hatua za kukomesha jambo hili.

Hivyo Mhe. Spika, suala hili la zawadi lisiwe kwamba tume inaweza, tume itoe zawadi kwa mtu yeyote atakayetoa taarifa na taarifa zile zikawezesha mtu fulani kukamatwa ama muingizaji, muuzaji au kwa aina nyengine yoyote ambayo itasaidia serikali kumkamata mtu yule kiudhati na kumpeleka

Mahakamani. Kwa sababu zawadi ndio itakayowashawishi watu kutoa hizi taarifa. Maana yake sasa hivi hakuna kitu, anasema nikenda nikimtaja jirani yangu, nitakuwa nimesema tu sina chochote kitakachoongezeka kwangu. Sasa kukiwa na kitu kama kile kivutio basi kitasaidia, tunaweza tukapata taarifa mbali mbali ambazo zitatuwezesha kusaidia katika kuzuia jambo hili. Mhe. Spika, suala la zawadi lisiwe la kuweza kwa tume, liwe ni jambo ambalo la kutangaza kabisa.

Mhe. Spika, nakumbuka kipindi fulanil wenzetu Tanzania Bara walipokuwa wakipambana na ujambazi walitangaza hasa, mtu yeyote anayetoa taarifa juu ya upatikanaji wa silaha na silaha ile ikakamatwa basi atapatiwa kiasi kadhaa cha fedha. Mbona silaha zilikamatwa kwa wingi, ikawa watu wanatoa taarifa na watu wanapata chochote.

Mhe. Spika, hii ni njia mojawapo ya mapambano. Kama tulivyosema mwanzo kwamba haya ni mapambano dhidi ya madawa ya kulevya. Kwa hivyo, mapambano lazima yaende katika sura hii ya mabadiliko, lazima tubadilike kuendana na wakati. Mhe. Spika, nimshawishi Mhe. Waziri akubali kuliweka hili kwenye sheria kwamba mtu yeyote atakayetoa taarifa zitakazosaidia na kuwezesha taarifa sahihi basi apatiwe zawadi na pengine itajwe hasa, au pengine itajwe thamani kulingana na bidhaa yenyewe.

Mhe. Spika, jengine sehemu ya tano ya mswada huu inaeleza makosa na adhabu mbali mbali zitakazotolewa baada ya mtuhumiwa kutiwa hatiani. Mhe. Spika, mimi kimsingi nakubaliana na adhabu zote zilizotolewa kwa wakosaji kwa sababu ni adhabu zinazokwenda na wakati na kwa kweli kama watuhumiwa watafikishwa Mahakamani na kama sheria hii tunayotaka kuipitisha leo ama kesho itakuwa iko sawa sawa, basi ni matumaini yangu kwamba vitendo hivi vya uingizaji wa madawa haya vitapungua au vitaachwa kabisa.

Mhe. Spika, sote tunaelewa kwamba wenye biashara hizi hasa hawa vigogo wao wako pembeni wanasubiri kukinga tu. Anakwambia chukua kontena hili kafanye hivi ukikamatwa mimi nipo, ukipelekwa Mahakamani nitakutoa, ukitiwa ndani nitakutoa, basi itasaidia katika kuona kwamba mapambano haya dhidi ya madawa ya kulevya yanafanikiwa.

Kwa mfano Mhe. Spika, kifungu cha 18 kinasema kwamba, “Mtu yeyote ambaye atapatikana au anafanya kitendo chochote, au anaacha kufanya kitendo au kitu kuhusiana na madawa ya *Nakotiki* na *Saikotropiki*, au matayarisho yoyote yenye madawa yaliyotengenezwa atakuwa mkosa na akipatikana na hatia atashtakiwa kwa kutozwa faini isiyopungua shilingi milioni 20 au kifungo cha miaka 14 au adhabu zote mbili kifungo na faini”.

Mhe. Spika, kwa kweli adhabu kama hizi ni adhabu zinazokwenda na wakati. Kwa hivyo, tunampongeza Mhe. Waziri kwa kuweka viwango kama hivi vya adhabu ambavyo vitatusaidia kupambana na haya mambo ambayo yanatuathiri katika nchi yetu.

Mhe. Spika, mwisho baada ya maelezo yangu hayo, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magomeni naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mhe. Aziza Nabahan Suleiman: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu na mimi nichangie kidogo maneno mawili matatu kuhusu Mswada huu wa Madawa ya Kulevya.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kunipa pumzi ya kusema. Pili Mhe. Spika, nauchangia Mswada huu kwa uchungu mkubwa sana kwa maana mimi nimeathirika, mwanangu niliyemzaa tumboni mwangu anahusika na madawa ya kulevya. Kwa hivyo, nitakachokisema nistahamilieni.

Mhe. Spika, nafurahi sana kuona kumetungwa sheria labda itaweza kutusaidia katika nchi yetu kupunguza hili janga tulilonalo. Mhe. Spika, nasema mimi nimeshazoea kusimama sana hapa toka nimeingia kwenye Baraza hili, kikija kitu kama hiki nakichangia sana na natoa ushauri sana kwa serikali nini tufanye, lakini bado hatujafanikiwa hata robo ya kupunguza madawa ya kulevya labda kuzidi.

Mhe. Spika, madawa ya kulevya yamezidi bila ya kiasi katika nchi yetu, vituo tokea vilikuwa viwili sasa vimeshakuwa 12, tokea walikuwa wakila madawa ya kulevya watoto wa mjini sasa mpaka mashamba, kwetu Kiboje tayari yapo kwa ushahidi yanapelekwa yanauzwa.

Mhe. Spika, niseme kufanywa hii sheria si kama ndio kumetungwa sheria itafanya kazi bila ya kuwa na utekelezaji, sheria inataka itekelezwe. Tunaweza tukaunda sheria kila siku tukija hapa tunaunda sheria inaletwa Miswada tunafanyaje lakini kazi hazitekelezeki, watu hawafanyi kazi inayotakiwa. Mimi naona ajabu nchi ina serikali, ina ulinzi, ina kila kitu, haya madawa ya kulevya yanapita wapi, yanateremka juu. Isipokuwa serikali ulinzi wake ni mdogo na hapafanywi kazi kihalali.

Mhe. Spika, hapa juzi paliulizwa swali, tukajibiwa kwamba kuna ulinzi mkubwa bandarini, kuna ulinzi mkubwa uwanja wa ndege, ulinzi huu wa kulinda nini, maana madawa ya kulevya yamejaa katika nchi, unapopita unawakuta watoto wanasinzia. Mjumbe aliyechangia sasa hivi anasema wanasinzia vichwa vinagonga chini.

Mhe. Spika, zamani bangi ilikuwepo hapa atafanya kazi mpaka umuonee huruma akisha kuvuta bangi yake. Lakini hawa wanaokula madawa ya kulevya hawawezi lolote zaidi ya kusinzia na hii ni hasara kubwa katika nchi yetu. Sijapata hasara mimi tu niliyekuwa mwanangu ameathirika, lakini serikali na watu wote wa nchi hii wanapata hasara kwa sababu wale watoto si wa mtu mmoja.

Kuna siku nilisimama hapa nikasema baada ya miaka mitano tutakuwa tuna wendawazimu wengi humu ndani ya nchi hii kwa sababu ya madawa ya kulevya. Ni kweli watoto wengi sasa hivi hawana akili na wakipelekwa hospitali ya *Mental* wakikaa miezi miwili akili zinarudi kwa sababu hawapati unga.

Mhe. Spika, ikiwa sheria hii itapitishwa hapa Barazani na haikutekelezwa sote tuliokuwemo humu Barazani tutakuwa tuna dhima kubwa kwa Mwenyezi Mungu, kwa sababu tunakuwa tunachangia tumepitisha sheria lakini haikufanyiwa kazi. Kufanyiwa kazi si kama kuandikwa ndani ya hili gazeti au tukaletewa sisi Miswada tukaipitisha hapa asilimia mia kwa mia halafu watoto wetu wanakula unga ambao unateremka juu haupiti kwenye vituo vyovyote kwa sababu ulinzi upo na wao wanaathirika.

Mhe. Spika, nalichangia hili jambo kwa uchungu sana kwa sababu serikali haitutendei haki wananchi wake. Leo sisi kama tuko Pakistan huko kunakolimwa au na hapa unalimwa huu unga sisi hatujui. Waziri wa Kilimo vipi. Maana Pakistan ndio kunakolimwa unga huko kukafanywa kila kitu, lakini hapa Unguja kimekuwa kituo kikubwa sana. Hata wenzetu wa Pemba kidogo afadhali, lakini pia sasa hivi umejaa tele nao. Sisi tuna watoto kama wale waliokwisha kuathirika tunaumia kweli kweli. Sasa nawaapiza wale wanaoleta unga Mwenyezi Mungu atawapa laana na wao watoto wao kila wanayemzaa wawe kama hivi walivyokuwa watoto wetu.

Leo watoto wetu wanakula unga baadae serikali inawatuma askari kawakamateni wale, si mnawaonea jamani. Wao kama hauletwi watanunua wapi na kuweza kuuvuta. Mhe. Spika, huu ni uonevu na serikali haitutendei haki. Wakamatwe wanaoleta unga na uwezo huo serikali wakitaka wanaweza, kwa nini washindwe. Ukikaribia uchaguzi hapa panakuwa na ma-*rocket ranger* nyingi sana hapa na bunduki kupigwa watu na maji ya kuwasha, lakini waletaji unga hamuwakamati kwa sababu gani. Hebu twambieni kuna nini.

Msitwambie sheria kwa sababu hili jambo tafadhali Mhe. Haji usiseme nyamaza, itabidi nikulipe. Aah! unasema na Spika kakunyamazia, kwa hivyo ukisema nitakujibu.

Mhe. Spika: Twende kwa utaratibu tumuachie nafasi azungumze yasitoke mengine.

Mhe. Aziza Nabahan Suleiman: Mhe. Spika, mimi nizungumzie hii tume. Mhe. Spika, Mhe. Salmin Awadh Salmin pale kamwambia Mhe. Waziri atulishe mpaka tushibe, kwa nini hii tume iwe ya mawaziri.

Mimi namuunga mkono kwa hili, kwa sababu nilikuwa tayari nimeshalinukuu. Tume Waziri Kiongozi ndio mwenyekiti wake, mawaziri ndio wajumbe wake. Mhe. Spika, pana nini au ndio maana watu wakawa hawakamatwi? Tuelezwe kuna nini? Mimi nafikiri hii tume ingekuwa ina watu mchanganyiko labda ingeweza kufanyakazi, kuliko kuwa na mawaziri watupu, halafu baadae akija Mkemia anatuambia ni unga wa sembe.

Mhe. Spika, mtu anakamatwa na pipi keshazibeba ndani ya tumbo lake, anatoka nazo huko anakotoka , anafika nazo hapa, zinatolewa, tunaoneshwa ndani ya matelevisheni, halafu leo Mkemia anakuja kutuambia kwamba ule ulikuwa sio unga ni unga wa sembe au saruji, hafai huyo! Kwa nini mwanzo uwe ni unga unabadilishika kivipi? Kimiujiza au kimazingaobwe? Labda kuna mazingaobwe yanabadilisha badala ya kuwa unga kunusa unakuwa ni unga wa sembe wa kupika! Tuleteeni basi majumbani tupike. Ukishasikia sio wa kunusa ni unga wa sembe hujui unapelekwa wapi? Unarudi unauzwa mule mule kwa watoto wetu na kutuulia watoto wetu.

Mhe. Spika, hapa pana mambo chungu nzima ambayo yameandikwa kwenye hii sheria. Mimi sitaki kuchangia au kuupitisha nataka niseme tu kisha nikae kitako. Kuna mambo chungu nzima yameandikwa humu, lakini hakuna hata moja linalofuatwa humu. Kesho *ambush* humkuti mtu, inakuaje mambo yanapangwa polisi halafu pale inakuwa hapatikani mtu! Kuna ripoti lazima inakwenda, na inakwenda kwa sababu mtu anapata *percent* yake pale, pakiuzwa anapewa chochote, wanaoumia ni watoto wetu.

Mhe. Spika, mimi mwanangu namwita maiti kwenenda, ndio anajipiga sindano ni nini. Mhe. Spika, inauma, inauma.

Wajumbe: Basi kaa kitako.

Mhe. Aziza Nabahan Suleiman: Sikai, niache hivi hivi. Nitasema japo kidogo.

Mhe. Spika, sheria huwa sheria na ikitungwa iwe sheria. Sheria ni msumeno inakata mbele na nyuma, isiwakate wadogo wakubwa wakaachwa. Wenzetu katika nchi nyengine wana mavituo ambayo wanawaweka na wanawatibu

watoto wao, ukibahatika anaweza akapona. Mimi wangu nimeshampeleka kila pahali, akishafika hapa akikaa miezi minne mitano au sita anarudia kama kazi.

Mhe. Spika, jana inatolewa mada hapa mimi nalia. Juzi nimeletewa kesi si ndogo ya mwanangu, mwanagu hana shida. Lakini kuna hii inayoitwa "hauonjwa" , ukishakula hiyo mara moja basi inatabu sana kuuacha. Sasa bado leo Serikali tunaiona inawatizama tu watoto wanakufa. Baadae tutapata viongozi gani hapa? Au nani atakuwa kiongozi ikiwa viongozi wa baadae wote wanakufa kwa unga? Nani atakuwa kiongozi? Watoto hawasomi, watoto wanaacha kila kitu na wala hawana madhehebu ya dini wala hawana chochote Mhe. Spika, kwa ajili ya kula unga.

Mhe. Spika, vituo vimezidi mara dufu na vituo vyote vinajulikana, askari wanavijua na Serikali inajua. Kwa sababu havina siri, viko wazi. Ukipita Miembeni hapo utachefukwa na roho. Nyumba zote za Miembeni pale watu hawana hata la kufanya, kwa sababu humo humo wanakaa kula unga na kuwaibia watu. Kwa sababu mtu akishakula unga Mhe. Spika, huwa watu wote anawaona kama paka tu. Kwa hivyo, hata akikuta kitu cha mtu anachukua na anajiona yeye ni mfalme. Akikaa pale akisinzia anajiona yeye keshakwenda mpaka Marekani na hali kumbe yuko kwenye baraza ya Miembeni keshanusa unga.

Kwa hivyo, hii Mhe. Spika, tunaumia sisi wazazi na Serikali ni lazima iangalie nini cha kufanya ili kuisaidia jamii isimalizike. Watoto chungu nzima wameshakufa kwa kujidunga masindano, watoto chungu nzima wameshakuwa wenda wazimu kwa kuvuta unga. Sasa ikiwa Serikali inatunga sheria kisha inaziwacha humu ndani ya makaratasi, itakuwa sisi haitusaidii kitu.

Mhe. Spika, mimi nafikiri tume iliyoundwa haifai kuwa ya mawaziri peke yao, ni lazima watafutwe na watu wengine watiwe mule, mawaziri na wabakie. Au ikiwa tumeunda tume za kupeana posho tu sawa tuendelee, kwa sababu ukikaa kikao ni lazima utapewa posho. Kwa hivyo, kama sio tume ya kupewa posho ni tume ya kufanya kazi, basi lazima tutafute na watu wengine watakaoweza kutusaidia.

Mhe. Spika, Kamishna wa Polisi yumo humu ni yeye tu, lakini kuna watu wake chungu nzima sijui kama anawaona wanafanya hiyo kazi, kama hawaoni basi mimi nafikiri nimwambie awatizame sana. Hao wanaotoa ripoti leo, sijui wanafanyiwa kikao kesho tunakwenda kukamata pahala fulani ikawa watu hawakutikani, basi Kamishna awaangalie vizuri watu wake.

Mhe. Spika, huu uuzwaji na usafirishwaji wa dawa za kulevya, hapa vinauzwa na pia ni kituo na milango ambayo ni ya kupitia hapa na kwenda nje. Kwa nini

iwe hivyo, Serikali ikubali kuwa na kituo hapa au tuwe na milango ya kupitishia madawa ya kulevya. Kwa sababu sisi hatulimi, kwa nini iwe hivyo na sisi tukubali kuwa na sifa ya kuwa na milango ya kupitishia. Tunakwenda kuchukua huko inakochukuliwa mtu anakuja navyo na tuna uhakika kwamba mizigo inajulikana kuwa hii ni mizigo ya fulani basi haisachiwi, kwa bahati mbaya wanakamatwa wale wanaobeba ndani ya matumbo yao.

Lakini hivi kweli Mhe. Spika, wale wanaobeba ndani ya matumbo ndio watalisha wote na vitasafirishwa vyengine, sio kweli. Lakini kuna mizigo inakuja inapita *Airport* na inapita bandarini haisachiwi. Sasa unga wa madawa ya kulevya umekaa sawa sawa na unga wa Bombay Bazaar ulivyojaa ndani ya nchi. Haitufikishi pahala jamani. Ni lazima tuwe makini sana kwa ajili ya watoto wetu. Tuwaonee huruma.

Mhe. Spika, isiwe kwa sababu mtoto wangu mimi au mtoto wa mwenzangu mimi, lakini na nyinyi kuna siku mtakuja kukuta katika familia zenu wamo, Serikali ni lazima itizame vijana wake, vijana ndio nguvu kazi ya baadae. Ikiwa nguvu kazi tunaiua sasa hivi baadae atafanya nani kazi, kutakuwa hatuna mfanyajikazi.

Jambo jengine Mhe. Spika, niliwahi kuzungumzia hapa kuhusu *rehab*. Nchi kama Dar es Salaam wanayo *rehab* sasa hivi. Kenya ndiko ilikoanza hasa, wanawaweka watoto wao. Mimi niliwahi kushauri, nikasema jamani chuo cha manunda Tunguu kiliwekwa kwa ajili ya manunda na hawa ni manunda, hawasikii kitu hawa, wameshakuwa kama wanaume wana wake zao wa Kipakistani juu ya vichwa au mwanamke na mumewe wa Kipakistani juu ya kichwa hasikii kitu.

Mhe. Spika, ile sehemu tuifanyeni iwe *rehab* ili watoto wetu wende tutalipa, kwa sababu tunaumia. Mwenye uwezo atalipa, asiyekuwa na uwezo Serikali imsaidie kwa sababu yule mtoto si wa mtu ni wetu na ni wa Serikali. Kwa nini tulifanya elimu bure hapa, si kwa sababu ni vijana wa Serikali wasomeshwe, basi na hili ni muhimu kwa sababu hupati hao wanafunzi, watoto wanaumia sana jamani ni wengi sana.

Mhe. Spika, mimi juzi nilikwenda sokoni Malindi nikakikuta kitoto kinakaa Rahaleo pale kidogo sana Mhe. Spika, nilitokwa na machozi nilipokiona, ni mdogo tena mdogo labda ana miaka 13 au 14 anakula unga keshabadilika uso wote, kakaa kama kizee kuliko mimi bibi yake, akaja chini yangu ananiambia “nigee pesaa, sijanywaa chaiii bibi leoo”.

Hii! Wewe umeshafikia hivi? Akanambia “aaah bibi ndio maishaaa”. Maisha? Mwanangu maisha?. Nikamwambia nitakupa Shs. 500/= kwa sababu najua kete

inauzwa Shs. 2,000/=. Kete moja inauzwa Shs. 2,000/= Mhe. Spika. Leo mtoto yule asiibe? Ataiba. Atafanya kazi gani ili apate. Wengine wanakula kete 10 kwa kutwa. Ndio. Kila mmoja na kiwango chake alichofikia. Sasa Shs.20,000/= mnafikiri ataipata wapi, hana kazi hana bazi. Wengine ndio wanaishia pwani kubeba ndoo za vibua wakitoka pale ile pesa haiwasaidii kitu wanakwenda kununua unga wanakula.

Mhe. Spika, Serikali lazima iwe kali, na iweke sheria kali ya hawa wanaotuletea madawa ya kulevya. Mimi nalia na hawa wanaoleta madawa ya kulevya na nalia na Serikali. Kwa sababu kama kweli Serikali imeamua basi ingewazuia hawa, Serikali ikitaka kuwajua basi ni dakika tano tu watawajua wote na wanawajua.

Mhe. Spika, *please*, tuvisaidie visiwa vyetu ni vidogo sana. Tuvisaidie visije vikazama, maana mwisho wake tutazama, Mwenyezi Mungu atatupaza humu. Hali ni mbaya sana Mhe. Spika. Kwa hivyo, na sisi tuweke hizi *rehab* ili zitusaidie hivyo hivyo, japo atakwenda atakaa mwaka au miaka miwili, lakini atapumzika na yeye akirudi labda Mwenyezi Mungu anaweza kuwajaalia.

Mhe. Spika, mimi mwanangu nimeshampeleka kila pahala, shahidi yangu bi Fatma Sukwa yule pale. Yeye alijaribu, kwa sababu anakitengo pale. Anawaita anawasomesha na anawafanyia kila njia, lakini haisaidii kitu kwa sababu akishawasomesha hapo walipowekwa hawana ulinzi wa kuwa wakae ndani, wanaambiwa wajitegemee, mla unga mwendawazimu, *half mental*, hawezi kabisa kuji-*control* na utamuona hasa akiukosa anavyokuwa anababaika.

Mhe. Spika, mimi naona uchungu mwanangu kwangu kafukuzwa na baba yake. Sijui hata nifanye nini? Wala sijui hata nitende nini? Mwanangu mzuri, mwanangu mtii lakini kaharibika.

Mhe. Spika, Serikali itusaidie, itusaidie sana kisheria. Tumesikia hapa Mhe. Salmin alisema kwamba wakamatwe, wapelekwe mahakamani. Ukishamkamata akipelekwa mahakamani akafungwa yule anayekula unga na unga unaletwa katika nchi, bado hujafanya jambo. Itasaidia kwamba yule kakamatwa katiwa ndani, lakini wanachimbuka wapya tele. Wakienda huko jela sikwambii kitu. Mimi nimeambiwa na mtu wa huko huko, wewe mama. Maana yake humchukua wangu nikampeleka huko huko, nikamwambia hebu niondosheeni kiasi miezi sita nisimuone hapa, mtafutieni kesi yoyote mumbandike. Lakini wakaniambia unahangaika bure mama, huku jela wanaupata. Mhe. Spika, wataupataje kama haupelekwi?

Mhe. Spika, tupenye kila pahali ili kuangalia namna gani tunaweza kuzuia unga usiingie katika nchi hii. Bila ya kushirikiana wananchi, Serikali na ulinzi

haiwezekani. Kwa sababu mimi nitasema pahala fulani nimeukuta uko, sina haja ya kusema kunajulikana. Lakini ulinzi haufanyikazi yake kikawaida, Serikali ndio kwa sababu sheria ilikuwa *loose* likuwa ile ndio imetungwa mpya labda itakuwa kali. Ndio hivyo tena mkemia akipelekewa asubuhi atasema unga jioni akija anasema sembe.

Tujitahidini jamani tena sana. Hii *rehab* Mhe. Spika, lazima ifanyishwe kazi kubwa sana, iwekwe hii *rehab*, ili tuweze na sisi kupata kituo cha kuwapeleka hawa watoto wetu wakapumzika. Maana yake kule ni kufa na hakuna hata mtu mmoja anayetaka mwanawe afe, tunataka waishi, lakini wataishije na wanauliwa, huku ni kuuliwa.

Mhe. Spika, hapa nimeona adhabu, kuna adhabu za milioni 20, kuna adhabu za miaka 7, miaka 14. Hizi si adhabu milioni 20, kwa muuza unga ni *northing*. Ikiwa kete moja anauza Shs. 2,000/= mlaji mmoja anaweza kwa kutwa akala za Shs.20,000/=. Mhe. Spika, unafikiri hizi milioni 20 kwake zitakuwa ni adhabu kwake.

Mhe. Spika, nataka nikuambie, kuna watu huwa wanatumwa, hawa watoto wetu na roho zinawatoka kwenda kubeba, mnajua wanapewa kiasi gani? Sijui kama ndio bado mpaka leo au vip? Mtu unaambiwa unakwenda kubeba mzigo nitakupa milioni 15 na ukirudi milioni 15 ni ngapi hizo, ni milioni 30 kaweza kumpa mbebaji wa kwenda kuchukua. Je, atashindwa kulipa faini ya milioni 20, hii sio faini kwa mla unga.

Mhe. Spika, leo tunawaona hatuna choyo, lakini tunawaona vijana wetu ambao waliojishirikisha na uuzaji wa madawa ya kulevya, sasa hivi wanapanda gari kuliko yako Mhe. Spika, ana nyumba kuliko zako. Kweli na nyinyi wawakilishi huko hamuwafikii hata kidogo wauza unga, kwa sababu wana pesa na wana sherehekea pesa ya kuuwa wenziwao na sisi Serikali tunawatizama.

Wajumbe: Wafungwe kifungo cha maisha.

Mhe. Aziza Nabahan Suleiman: Eeh! Kifungo cha maisha mimi nakiunga mkono, kwa sababu akifungwa maisha yule mwengine hatokei. Tulikuwa tuna televisheni hapa tukipigwa majiwe, yalikuwa yanaitwa majiwe kitwana, televisheni za rangi zilipoingia Zanzibar, suala hili nalisema leo mara ya pili. Ikawa hivyo hivyo anakamatwa mwizi tu, lakini siku Serikali ilipoamua kuwakamata wale wanaonunua televisheni hazikuibiwa tena. Sasa kwa nini hata hili lishindwe, wakamatwe wavutaji na waletaji wasikamatwe?

Mhe. Spika, kwa sababu kuna daraja tatu, kuna mletaji, kuna muuzaji na kuna mvutaji. Huyu aliyetoa nyumba akasema mimi nakodisha nyumba yangu Mhe.

Spika, kwa kifungo au faini ya Shs. 20 haijasaidia, mnyang'anyeni nyumba, anafanya uhalifu yule ni kesi ya jinai anauwa, mnamuachia auwe watu na nyumba yake anapata na kodi na posho zaidi anapewa, kwa sababu kaitowa kuuziwa unga? Hii si halali tusiwape adhabu za aina hii za kama mtu kenda kwetu Kiboje kaiba mkungu wa ndizi. Tuwape adhabu ya kujua mtu mimi napata adhabu ya sifanyi tena kosa hili.

Mhe. Spika, naona mimi niishie hapa.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi hii kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Madawa ya Kulevya. Kabla ya yote nichukuwe nafasi hii Mhe. Spika, kumshukuru kwa dhati Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa jamii na wasaidizi wake kwa kuona kwamba ipo haja ya kufanya marekebisho makubwa sana ya sheria inayohusika na madawa ya kulevya kutokana na matatizo yake kwa jamii.

Mhe. Spika, kwa kweli moja katika tatizo moja kubwa sana, sio hapa Zanzibar tu lakini dunia nzima. Mimi naweza kusema moja katika tatizo kubwa sana pengine la mwanzo ni madawa ya kulevya. Hata watu wamefika kusema kwamba madawa ya kulevya ni mabaya zaidi kuliko ukimwi. Kwa sababu waathirika wa ukimwi Mhe. Spika, tunaishi nao, wana akili zao, wanafanyakazi za kuzalisha kwa taifa na mpaka wakati wao ukifika wanaondoka.

Lakini Mhe. Spika, wenzetu hawa wanaotumia madawa haya na hasa ilivyokuwa kwamba wengi wao ni vijana ambao tunasema ni nguvu kazi, wana matumaini makubwa kwa familia na taifa lenyewe basi kama alivyosema mchangiaji wa mwisho hapa kwamba mambo haya hayaonjwi, na kweli ukionja tu tayari ni tabu sana kurejea, ifanywe kazi ya ziada labda ndio watarejea.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, hili ni tatizo kubwa sana kuliko ukimwi, kwa sababu ukimwi wanaweza kufanyakazi zao na wanaakili zao na wanakubalika na jamii. Haidhuru kuna jamii nyengine wanakasirika nao kwa kiasi fulani, lakini hawa wa madawa ya kulevya wanaathirika zaidi kwa sababu hawa ni vijana ambao ndio nguvu kazi na ni wengi, hawa vijana wakishaanza haya madawa basi inakuwa hawawezi tena kufanya lolote, akili yao iko pale pale tu ni lazima wapate madawa basi kwa njia yoyote ile.

Kwa hivyo, mambo haya yanaathiri nguvu kazi kwa vijana wetu, taifa linapata tabu, familia zinapata tabu, jamii inapata tabu. Kwa sababu inasemekana kwamba ni kweli kama takriban sasa hivi ni kila mtaa wapo watu hawa. Inasemekana kwamba katika familia ukiwa naye mmoja tu basi ataanza kuiba

kila kitu kilichokuwemo ndani, mpaka sufuria ili mradi tu aende akapate dozi ili iweze kumsaidia. Kwa hivyo, hili ni tatizo kubwa sana kwa taifa.

Mhe. Spika, katika nchi kama zetu hizi ndogo ndio imekuwa hasi kwa sababu hawa ndio tunawatumainia keshokutwa kuwa viongozi wa taifa hili. Sasa kila siku kukicha wanazidi kupungua ni tatizo kubwa sana.

Mhe. Spika, tatizo hili ni kubwa sana na kwa nini likawa kubwa sana. Ni kwa sababu biashara hii ni moja katika biashara kubwa sana yenye mapesa mengi tu. Tunasoma magazeti, tunatizama televisheni, tunabahatika kusafiri, tunakaa na watu tunawasikia wanazungumza nini. Kwa hivyo, ni biashara kubwa sana, katika biashara kubwa sana katika dunia hii basi ni hii ya madawa ya kulevya, sio hapa kwetu tu ni dunia nzima.

Mhe. Spika, wanaofanya biashara hii ni watu wakubwa sana, hawa wadogo wanatumwa tu, au wanatumia tu, lakini wafanyaji hasa ni watu wakubwa sana. Hii kwa kweli wanasema ni mnyororo, yaani cheni tangu yule mlimaji, mpaka mnunuaji na muuzaji. Sasa ikiwa kitu cheni ni tabu sana kukiuwa mara moja.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba hawa watu wana mapesa mengi sana, kwa hivyo wanatumia mapesa yao kwa njia zote wanazozijua wao kwamba wasiweze kupatikana.

Sasa basi kutokana na hali hiyo Mhe. Spika, dawa ni moja tu, kama ilivyokuwa Ukimwi dawa ni kuacha tu masuala haya. Lakini na haya vile vile dawa ni moja tu. Dawa itakapofika wakati jamii yenyewe wakasema sasa basi, nikisema jamii kila mmoja wetu na sio hapa visiwani tu ni dunia nzima, sio mwanasheria, si walinzi, si watu wa dini, si wana siasa na sio raia wa kawaida waseme basi na baada ya kusema basi washirikiane, hapo afadhali kidogo huwenda yakapungua mambo haya.

Lakini tukisema sisi hapa visiwani Mhe. Spika, kwamba basi, bado itakuwa ipo kazi, kwa sababu ni kitu *global*, yaani ni kitu ambacho kinakamatana. Hapa kwetu yanaletwa tu sisi hatulimi, kwa hivyo sisi au dunia nzima mpaka tuseme basi, hapo kidogo ndio itakuwa afadhali. Kwa hivyo, ipo kazi ya kufanya ziada Mhe. Spika.

Mhe. Spika, utungaji wa sheria ni kitu kimoja lakini utekelezwaji wa sheria ni kitu chengine, na hapa ndipo tunaposhindwa. Sheria zetu Mhe. Spika, tumezitunga nyingi tu tena nzuri na madhumuni ya sheria zote zinazotungwa zinakuwa zinalenga maslahi au maendeleo ya nchi au wananchi wake zote, hakuna hata sheria moja ambayo inatungwa kwa kuleta ubaya katika taifa zote

zina maslahi kwa nchi na maendeleo ya nchi. Kwa hivyo, kutungwa sheria ni kitu kimoja lakini utekelezaji ndio mara nyingi tunashindwa.

Kwa hivyo, ningeiomba sana hii tume pamoja na vyombo vyote vya ulinzi na usalama na sisi raia sote kama nilivyosema hebu tushirikiane kwa pamoja tuseme basi na tusimame sote kwa pamoja tusimamie sheria hii.

Jambo ambalo Mhe. Spika, naona litakuwa ni la busara, sijui wewe Mhe. Waziri kwa sababu sijaisoma sana hii, kwa hivyo siwezi kusema uongo, pengine yamo haya mambo ndani. Nafikiri ipo haja Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii najua kule kuna kitengo maalum kinachoshughulika na Ukimwi tu na sio kazi nyengine. Basi nafikiri ipo haja na suala hili nalo Mhe. Waziri namshauri akawa na kitengo maalum kwa kazi hii tu kuhusu suala hili la madawa ya kulevya. Tena sio kuwa na kitengo tu ni kuwa na watu ambao wamefunzwa na wamefunzika katika masuala haya ya madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, baada ya kuwa na kitengo hicho pamoja na kazi zao ambazo zimeainishwa hapa, mimi sijazisoma. Nafikiri moja katika kazi zao kubwa sana iwe ni kuelimisha jamii nini athari za madawa haya ya kulevya na ikiwezekana washirikiane na vyombo vyetu vya televisheni na radio, ili wapate wanasema *airtime* ya kutosha waweza kuelimisha jamii juu ya athari, haya madawa ya kulevya ni nini, athari zake na kwa jumla vipi, kiuchumi inakuwa vipi na kwa taifa inakuwa vipi na kadhalika. Liwe ni suala la kuendelea la kudumu. Isiwe kwamba ni wiki sita, miezi minne au mitano ikawa tena basi, hapana iwe ni ya kudumu Mhe. Spika, kutokana na umuhimu wa suala hili la matatizo ya madawa ya kulevya kwa maendeleo ya nchi zetu.

Mhe. Spika, kama msemaji wa mwisho alivyosema hapa kwamba hawa ni vijana wetu, ni binadamu hawa, ni wananchi na wala tusiwaone wajinga. Kila mmoja ashukuru amwombe Mwenyezi Mungu kwamba yeye mwenyewe hajaingia humu au watoto wake hawajaingia humu, tusiwe na mawazo kwamba tunamuona mtoto wa mtu kaingi humu kwenye haya madawa halafu tukaanza kucheka, aah! Yule hivi na hivi hapana tuone huruma tulie, kwa sababu yule ni binadamu kama sisi na ni mwananchi kama sisi na ni watoto wetu.

Kwa hivyo, tufanye kila njia ikiwezekana Mhe. Spika, katika hicho kitengo tufikirie vipi tutaweza kuwasaidia hawa, isiwe kuwa basi ndio wameshaharibika iwe ndio basi, hapana. Nafikiri kitengo hiki ipo haja ifikirie vipi tutaweza kusaidia.

Kwa mfano, imetolewa rai hapa kwamba kule kulipokuwa Tunguu kwenye maeneo maalum ya watoto nunda, basi tufikirie mambo kama yale kwa mfano. Lakini najua wale wakipata maradhi ninavyojua mimi sasa hivi wanapelekwa

kule *Mental Hospital*. Mimi nafikiri ingekuwa hapana budi Serikali itazame uwezekano wa kujenga chuo maalum kwa kesi kama hizi, kwa sababu kesi kama hizi ziko nyingi na zitaendelea kuwepo. Ukimwi tumejenga pale sehemu japokuwa ni ndogo, lakini tunajua ipo afisi yao pale na wapo watu pale maalum. Kwa hivyo, na hawa vijana nafikiri tungejenga Hospitali yao mbali na wakawa na watendaji wao wa kazi wataalamu wao kule kule. Tuwasaidie kimatibabu na ikiwezekana tuwasaidie *social*, kwa sababu hawa ni wetu na sisi kama ni Serikali ndio wadhamini wa mwanzo kwa watu hawa.

Mhe. Spika, kwa kweli haya mimi ndio yalikuwa dhamira yangu nichangie mswada huu, nimetizama hapa katika *notes* zangu, nimeona kwamba nimemaliza. Kwa hivyo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, lakini naomba sana Mhe. Waziri haya tuliyozungumza ajaribu kuyafikiria kwa kushirikiana na Serikali kuu, hasa katika suala lile la kujenga eneo maalum kwa vijana wetu hawa. Mhe. Spika, nakushukuru. Mhe. Spika, naunga mkono hoja, vile vile mimi mwenyewe na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni tunaipongeza sana hoja hii na tunaiunga mkono.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Ali Denge Makame: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi hii ya kwanza kwa jioni hii ya leo kwa ajili ya kuchangia mswada huu unaohusiana na madawa ya kulevya.

Kwanza awali ya yote ni kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kuutayarisha mswada huu na kuuleta hapa kwa ajili ya kuujadili na baadaye kuupitisha.

Mhe. Spika, kwa kuletwa mswada huu ambao unahusiana na madawa ya kulevya, kama tunavyoelewa vijana wengi wa rika tofauti, wakiwemo wanawake na wanaume kwa hivi sasa muda mrefu vijana hawa wameshaathirika na madawa haya. Kwa hivyo, kuletwa kwa mswada huu kwamba haya mambo yapo, lakini tunayafumbia macho.

Sasa kwa kuletwa Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya Nam. 16 mwaka 2003 na Kutunga Sheria Mpya ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa ya *Narcotic* na aina za *Psychotropic* na mambo yanayohusiana nayo.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza mwanzo kwamba tatizo la madawa haya yameshaleta athari kubwa sana kwa vijana wetu kama walivyotangulia kusema waheshimiwa wajumbe wenzangu hapa. Kwa mfano, hivi sasa ukitembea mitaa mingi kwamba wale vijana tuliokuwa na mategemeo ya nguvu kazi kwenye mawizara, mashirika mbali mbali na hata kwenye familia zao.

Kwa kweli hivi sasa wamekuwa hawajiwezi na wala hawana nguvu, yaani muda mwingi huwa wanalala mabarazani au vichochoroni. Kwa hivyo, tatizo hili limekuwa ni kesi kubwa sana kwa nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, sasa kwa umakini wa hali ya juu vyombo vya sheria pamoja na taasisi husika tulivalie njuga suala hili na tuhakikishe linapungua au linaondoka kabisa. Kwa sababu tukiangalia uwezo wa kulifanya suala hili la kupungua au kuondoka kabisa tunao.

Kwa kuwa mletaji ni binadamu na mwenye kupewa kusambaza pia ni binadamu. Kwa hivyo, si kweli kama yule mletaji atakuwa hana mwenzake ambapo siri inaikajulikana au yule mwenye kusambaza kwa ajili ya kuuza katika zile sehemu anazouza asionekane na wala asijulikane na kupata kudhibitiwa, ili kuhakikisha suala hili tumelipunguza.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nende kwenye ukurasa wa 72 kifungu cha 22 kuhusu maombi ya amri ya kutaifisha. Kama ilivyoelezwa kwenye kifungu hiki kuomba amri ya kulipa faini ya fedha dhidi ya mtu kutokana na faida aliyoipata kwa kutenda kosa hili. Kwa kweli kama tutazingatia mtu aliyefanya kosa hili au tendo hili kwa kutegemea apigwe faini tu, kwa kulingana na hali ya mtandao huu ulivyokuwa na watu wazito, yaani matajiri, basi itakuwa hatujafikia pahala.

Kwa mfano, mtu anafanya kosa kama hili kubwa na ukapatikana ushahidi kwa kuwa tunataka tulikomeshe lisiwepo, basi ni vyema zikatayarishwa adhabu za kumtisha yule mtu na kuogopa kifanya kitendo hiki. Lakini kwa matayarisho ya kusema apigwe faini tu, kwa kweli itakuwa hatujafanya kitu, kwani wanayo mitandao mikubwa tena yenye uwezo mkubwa. Kwa hivyo, vyovyote vile faini italipwa na mtu yule ataendelea kufanya matokeo yale.

Mhe. Spika, nawaomba watu wa sheria wakatafuta kipengele kizuri cha adhabu cha kumfanya mtu yule asiendelee kufanya tena masuala haya. Kwa sababu imeshatuathiri sana, yaani tukipita mitaani kila leo maagizo makubwa tunayopewa na wananchi ni suala la kutafuta mbinu ya kulipunguza suala hili la madawa ya kulevya au kuliondoa kabisa.

Kwa hivyo, pindipo ikipangwa mipango mizuri ya kuwadhibiti hawa, *Inshaallah* wananchi wetu watakuwa na maisha mazuri na wala vijana wetu hawatopotoka na masuala haya.

Mhe. Spika, ombi linaweza kufanywa chini ya kifungu hiki kuhusiana na kosa moja au zaidi ya moja. Kwa mfano, mtu kusema amefanya kosa hili na kupelekwa kwenye vyombo vya sheria na kuonekana amefanya kosa moja na kuachiwa au kupunguziwa adhabu, basi hapa itakuwa hatukufanya jambo.

Kwa maana hiyo, kwa makosa kama haya ni mazito sana na kama tunataka tuhakikishe kuwa yanapungua au yanaondoka kabisa, basi mtu hata afanye kosa moja ajulikane kwamba amefanya kosa. Kwa hiyo, jambo la msingi ni kupewa adhabu inayostahili tena adhabu hiyo tusipendelee kuwapa adhabu ya faini kama nilivyosema na nitakuwa nikirejea humo kwa humo.

Mhe. Spika, nadhani ni vyema ikatafutwa adhabu inayolingana na kosa hili, ili yule mwengine ambaye huko nje anaposikia basi ajue kuwa suala hili limekatazwa rasmi.

Sasa naomba niende kwenye ukurasa wa 83 unaozungumzia masuala ya kutaifishwa, yaani uwezo wa kupekuwa na kukamata. Mhe. Spika, ni vyema wahusika wa suala hili la kupekuwa na kukamata wasiwekewe vikwazo vikubwa, isipokuwa wapewe nafasi ya uhuru wa kupeleleza, kutafuta mpaka haya masuala watapoyaona, basi kusiwe na urasimu mwingi kwamba lazima kuwepo na mashahidi watatu au wanne.

Kwa sababu suala kama hili kwa kumsubiri akachukuwe mabuku ya uthibitisho nadhani ushahidi utapotea na yule mtu kile kitu pale alipokiweka anaweza kukihamisha, kwa hivyo kazi ya upelelezi na upekuzi haifanyiki.

Mhe. Spika, nadhani tukubali wazi kuwa masuala kama haya kwa kutaka kuhakikisha kwamba watu wanaogopa na yanafanyiwa kazi vizuri ya upekuzi, basi mtu aone tu wahusika na kazi ile wamefika ghafla, kwa ajili ya kufanya upekuzi na kuchunguza matatizo yale yapo kwa sehemu waliyoishakia.

Lakini tukisema tutafute watu wawili au watatu kwa lengo la kutafuta ushahidi au mabuku ya upelelezi, kwa kweli suala hili kwa kulingana na hali yetu ya nchi zetu zilivyo kwamba kila mtu anayo mitandao, yaani anayo mawasiliano na wengi tumehusiana. Kwa hivyo, ikiwa suala hili litalifanyia urasimu mkubwa basi hawatopatikana, yaani wale wakorofi wanaokusudiwa hawatopatikana.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kushirikiana na taasisi husika katika kazi hii ya upelelezi pamoja na upekuzi ifanywe kwa kina, ili kuhakikisha kwamba masuala haya tunayaondosha kabisa.

Katika kufanya upekuzi tunaambiwa tupate ridhaa ya yule mtu anayehusika. Kwa kweli hakuna mtu yeyote ambaye ametenda kosa na halafu umwambie kwamba unakwenda kwa ajili ya kumpekuwa au uchunguzi akaridhika.

Nadhani atafanya kila njia ya udanganyifu kama utakwenda nyumbani kwake au ile sehemu iliyoshakiwa. Kwa hivyo, wakiwepo wenzake wawili tu, wao watapeana alama za kutizamana au vyengine vyovyote vile yule mwenzake ambaye yupo pale afahamu kama kitu fulani kakiondoe upesi na kukipeleka sehemu nyengine, kwa sababu hawa waliokuja ni wapelelezi ambao wanataka kunipekuwa.

Mhe. Spika, kama tutafanya hivi basi tutakuwa hatufanikiwi, kila siku tutakuwa tunawasaka na kuwapekuwa na wakati wanapoondoka wapelelezi machafu yale yanarejeshwa pale pale. Kwa hivyo, hapa naomba vyombo vinavyohusika vipewe uhuru wa kufanya upelelezi na upekuzi, ili tuweze kufanikiwa kulipunguza au kulitokomeza janga hili.

Sasa niende kwenye ukurasa wa 116 kifungu cha 18 (ii) kuhusu makosa na adhabu. Mhe. Spika, kama ilivyoelezwa kwenye kifungu hiki, adhabu hupatikana au kununua madawa koka au nakotiki, kuwe na adhabu kama kulipa fedha au faini.

Mhe. Spika, nadhani hii ni adhabu ndogo. Kwa sababu kama tunavyojua janga hili la kuuza madawa ya kulevya unaingia nchini na wanaoathirika ni vijana rika tofauti, wengine wanaathirika akili na hata kupoteza maisha kwa kujitunga sindano. Kwa hivyo, tunaona janga hili ni sawa na kusababisha kifo.

Kwa maana hiyo, watu wanaoleta madawa haya hawana tofauti na wale wanaowadhalilisha na kuwapotezea maisha wale wenzetu wenye ulemavu wa ngozi, kwa sababu kuna watu wanafikia hatua ya kuwapotezea maisha, kwa kutaka viungo vyao.

Kwa hivyo, na wao hivi karibuni yalitolewa matangazo ya kifo kwa kufanya masuala yale ya kuwapotezea maisha watu wenye ulemavu wa ngozi. Mhe. Spika, baada ya kutangazwa kuna watu wameanza kulalamika na kusema nyinyi mnapinga haki za binadamu, kwa hiyo tunapinga haki za binadamu kwa yule anayetenda, je, yule anayetendewa?

Mhe. Spika, nadhani kama tutazingatia hivi tunaweza kujikuta kuto pabaya, kwamba yule anayetendewa hana haki ya binadamu, isipokuwa yule mwenye kutenda ndiye mwenye haki ya binadamu na wala isitolewe hukumu ya kifo kwa yule mwenye kutenda kwa kuwa inapinga haki za binadamu. Kwa hali hii nadhani tutakuwa hatwendi mbele na wala hatufiki. Kwa hivyo, litizamwe kosa amethibiti kuua basi na yeye ahukumiwe kuuliwa.

Mhe. Spika, kwa hawa wanaoleta madawa ya kulevya vitendo vyao vinakaribia na hivyo, kwa sababu wanawapotezea maisha vijana wetu, hivi sasa wengi wameshafariki na wengine kuwa wagonjwa wa akili. Kwa kweli inafahamika kuwa shida pamoja na matatizo ya kumzaa mtoto, kumlea mpaka anapata fahamu zake, sasa leo tayari ameshapata fahamu zake kwa ajili ya kukusaidia katika maisha, tunaambiwa anashiriki kuuza mzigo wa madawa ya kulevya au kutumia madawa ya kulevya. Kwa hivyo, suala hili ni kitendo cha kumpotezea maisha yake.

Kwa maana hiyo, wanasheria wasione ugumu na wala kigugumizi cha kutoa adhabu inayolingana na hao wanaowakata viungo walemavu wa ngozi. Kwa sababu na wao tayari wameshafikia hatua ya kuwapotezea maisha, basi pasiwe na shida ya kutoa hukumu kubwa ikiwa kama si ya kifo basi afungwe maisha. Lakini leo anafungwa miaka 15 mpaka 20 na kesho kutwa anatoka anarejea kazi ile ile kwa hiyo tutakuwa tumefanya nini?

Mhe. Spika, namuomba Mhe. waziri akae pamoja na wanasheria kwa ajili ya kuangalia adhabu ya kuhakikisha hiki kitendo kimekomeshwa. Kwa sababu muda mrefu vitendo hivi vimeshaua watu wetu na wengi wao hawana nguvu tena za kufanyakazi.

Kwa hivyo, hivi sasa tuache kufumbia macho kuna haja ya kujaribu kubadilisha sheria zetu hizi. Je, wataendelea kufanya tena au wataacha kabisa na wala tusiogope tukasema kwamba labda huyu anayeleta ni mtu ambaye anatufadhili au anatoa misaada fulani. Kwa kweli tusikubali kufadhiliwa kwa kupoteza maisha ya watoto wetu.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri suala hili akaliangalia sana, yaani itolewe adhabu inayostahili kwa vitendo kama hivi na wala tusiogope kutoa adhabu kubwa. Kwa sababu tunataka kuiweka nchi yetu katika hali ya usalama, kama si hivyo kila siku watatuchezea, kwani serikali inapata hasara kubwa ya kuwakusanya na kuwapa matibabu vijana hawa waliathirika.

Kwa hivyo, kwa nia njema ya kutaka kuilinda serikali yetu isipate hasara, basi ni vyema kupanga mikakati ya kuhakikisha kwamba tunayasimamia vizuri masuala haya na kutoa adhabu inayostahili *(Makofi).*

Mhe. Spika, kama mheshimiwa mjumbe mwenzangu hapa kwamba watoto wengi wameshaathirika pamoja na watoto wake wamo na masuala haya. Kwa hivyo, kama tutayafumbia macho yatatuletea matatizo makubwa sana. Sasa kama walikuwa wakishawishiwa au kutoa rushwa au kupewa zawadi kwa ajili ya kuyafumbia macho masuala haya yawe ndio mwisho. Kwa maana hiyo, tuhakikishe kila mtu anawajibika kwa *section* yake, ili kuhakikisha masuala haya yasitokezee.

Kwa kweli masuala haya yanaeleweka ulimwengu mzima, yaani nchi nyingi sana hivi sasa masuala haya kwa maneno ya vijana imekuwa ndio *issue*. Kwa sababu nchi nyingi utakazotembelea hasa mijini basi utakuta masuala haya yamejitokeza kwa nguvu.

Mhe. Spika, tatizo liliopo baadhi ya mataifa yetu, wakubwa wanaangalia masuala ya silaha nzito, *chemicals* za kutengenezea vifaa vikubwa kama vile vya *nuclear*. Lakini suala hili la madawa ya kulevya bado halijapewa kipaumbele zaidi ambalo linaathiri sana vijana wetu wa Bara la Afrika.

Kwa hivyo, nadhani hapa tuzinduke na masuala haya tuyaangalie kwa makini, ingawa mataifa makubwa wanaangalia sana masuala ya silaha nzito nazo pia zinaleta faida katika ulimwengu na kulinda masuala ya ujambazi uhalifu pamoja na usalama mbali mbali.

Lakini tatizo la madawa ya kulevya tukiachia matumizi machache ambayo yanayotengenezewa dawa za hospitali. Kwa kweli, kwa asilimia kubwa yanathiri vijana wetu kwa kuyatumia kinyume na utaratibu uliokubalika. Mhe. Spika, namuomba mhe. waziri suala hili kuliangalia kwa kina, ili kuhakikisha haya masuala hapa kwetu yanaondoka.

Mhe. Spika, kwa kweli mswada huu kwa jinsi ulivyowasilisha hapa kwa ajili ya kuujadili pamoja na kuuchangia imekuwa ni jambo la busara sana. Kwa sababu muda mrefu sana masuala haya yalikuwa na utata na watu wengi wameathirika kwa matatizo hayo. Kwa hivyo, sasa kuna haja kama nilivyoeleza tuyaangalia kwa kina, ili tuhakikishe na sisi tumefanikiwa katika kupiga vita suala hili la madawa ya kulevya.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 87 kifungu cha 51 kinachozungumzia masuala ya amri za kuzuia, Mhe. Spika, naomba kunukuu.

Kifungu cha 51 (1) kinachosema hivi:-

> "Ikiwa mtu atakuwa ametiwa hatiani kwa kosa kubwa au anataka kushtakiwa kwa kosa kubwa, Mkurugenzi wa Mashtaka ataiomba mahakama itoe amri ya kuzuia kwa mujibu wa sehemu hii dhidi ya mali zote au mali yoyote iliyoorodheshwa ya mtu huyo pamoja na mali aliyoipata baada ya kutolewa kwa amri ya kuzuia na mali ya mtu mwengine ambaye hajatiwa hatiani".

Mhe. Spika, kama vitu hivi vitakuwa vimethibitisha kidhati, yaani vinahusika na masuala ya haramu ya madawa ya kulevya, pindipo vikifikishwa mahakamani wakati kesi inaendelea basi ni vyema vikapewa ulinzi wa kutosha, ili wachache wasijeviharibu au kuvibadilisha kwa ajili ya kupoteza ushahidi.

Kwa hivyo, kwanza tuhakikishe kwamba hivi vitu vimepatikana kwa njia ya haramu hayo madawa ya kulevya viwe na ulinzi wa kutosha. Kwa sababu kama tunavyofahamu huko nyuma baadhi ya vifaa mbali mbali vilivyotokana na masuala haya viliwahi kupatikana.

Lakini baadaye katika kuchukua hatua ya kuendesha kesi muda uliopangiwa kesi, basi wachache kwa tamaa zao tu, wamekwenda kuvibadilisha na kuweka vyengine na siku ya kesi ilipofika havikuonekana vile hali na matokeo yake ushahidi umetupiliwa mbali, yaani kesi *dismiss*.

Mhe. Spika, nawaomba wale wanaohusiana na masuala ya mashtaka kwamba wakati mambo haya yanapopelekwa mahakamani, basi vile vielelezo vihifadhiwe na viekewe ulinzi mzuri zaidi, ili kuhakikisha mambo haya tunayasimamia kwa dhati na kuweza kuyaondoa.

Mhe. Spika, kwa kweli mswada huu naunga mkono, kwa sababu athari zake masuala haya nimeyaona. Kwa sababu humo mitaani sisi ndio tunaopewa kesi nyingi sana za matatizo haya. Kwa mfano, kuna vijana wadogo mtaani kwangu hawapungui watano wamefariki kwa masuala haya, tena ni watoto wenye umri wa miaka 20 mpaka 25.

Kwa kweli vifo vyao ni kutokana na kujidunga sindano, kutumia unga kipimo kimezidi na matokeo yake wamepoteza maisha. Kwa hivyo, hapo kwangu hali ndio kama hiyo je, majimbo ya wenzangu. Mhe. Spika, naomba wahusika wa vyombo vya sheria tulisimamie kwa dhati, yaani kwa nguvu zetu zote, ili tuweze kufanikiwa *Inshaallah*.

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Amani *(Makofi)*.

Ahsante sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na ninakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo ya kuweza kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya Nam. 16 mwaka 2003 na Kutunga Sheria Mpya ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa ya *Narcotic* na aina za *Psychotropic* na na Mambo Yanayohusiana Nayo.

Mhe. Spika, mara nyingi sana huwa sheria au miswada kwa ajili ya kujadili pamoja na kuziunga mkono kwa asilimia mia moja. Lakini nilichogundua ni kwamba ile kusema kuunga mkono kwetu kumbe hatari yake inatukuta baadaye.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri, Katibu Mkuu wake pamoja na watendaji wake wote, kwa kufikiria suala hili na kulipitisha kwa wanasheria na mpaka kuletwa hapa ukiwa ni mswada, kwa ajili ya kujadiliwa na baadaye iwe sheria halali ya kuweza kulinda masuala hayo ya madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, leo asubuhi Mhe. Aziza Nabahan Suleiman alisema kwa huzuni kabisa na mimi naomba kanuni ilininde nitakuwa mmoja kwenye huzuni hiyo. Kwanza niingie kwenye huzui ya Mhe. Waziri, kwa sababu huu mswada kila nikiutizama naona kwamba Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii hana ubavu kwa sheria hii.

Kwa sababu yeye tutakuwa tunamuonea tu kusema kweli, hususan suala hili linaonesha kuwa yeye ndiye atakayekuwa msimamizi mkuu. Lakini Mhe. Spika, naomba kama ikiwa tunayo nia hasa ya suala hili kwa ajili ya kuliondoa kabisa katika nchi yetu, basi pendekezo lingeelekea katika Wizara ya Afisi ya Waziri Kiongozi, yaani huku ndiko kwenye ubavu.

Kwa kweli Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, yeye kazi yake ilikuwa tumpe moja tu ya kukinga pamoja na kutibu, hiyo ndiyo iliyokuwa tumuachie mwenzetu. Lakini inavyoonesha sheria hii kunakohusika sasa hatukupeleka na ndio maana ikawa mizizi ya madawa ya kulevya bado inaendelea kuwepo na itaendelea kuwepo.

Mhe. Spika, ndio maana nilisema kwamba Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, nilipoangalia na kuona kuwa wapi nimsifu kutokana na kuwepo kwa

kitengo ambacho kipo mkabala na Hospitali ya wagonjwa wa akili niliwahi kutembelea pale, basi niliwaona vijana walivyo katika hali nzuri sana.

Kwa sababu vijana wale ambao walikuwa tayari wengine wameshakonda sana wamo katika kusafiri kimawazo. Lakini hivi sasa kitengo kile kimefika mahala pazuri sana, yaani kimewaondoa katika fikra mbaya, tena ni mahodari sana wale vijana.

Mhe. Spika, wakati mmoja nilipokuwa nikichangia bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii nilisema kwamba Mhe. Waziri hatumuwezeshi, kwa sababu kuna mambo lazima apatiwe. Kutokana na hali hiyo, ndio maana nilisema kwenye bajeti ile kuhusu wale mbwa kichaa zile fedha ziondoshwe zipelekwe Idara ya Afya kwa mantiki yangu. Mhe. Spika, kwa sababu leo Mhe. Waziri fedha haikidhi haja, ndio maana tukasema kwamba hata bajeti zinakuwa hazikidhi haja kutokana na hali ilivyo ingawa anajitahidi kusema kweli. Lakini ukiangalia mandhari ya ile hospitali wenyewe mimi naona haya kusema kwamba ile ni hospitali ya rufaa kutokana na hali ilivyo. Kwa hivyo, tunaomba aongezee mheshimiwa fedha kwani ameshaonesha nia nzuri kwa vijana, sasa hivi vijana utakuta wanawaelimisha vijana wenzao ili waondokane na madawa ya kulevya. Mhe. Spika, ndio maana nikasema kutokana na mswada huyu bado hatujampa nguvu Mhe. Waziri kuweza kusema kuwa hili suala liondoke.

Mhe. Spika, nikiendelea kuchangia ni kwamba bado serikali haijawa makini juu ya suala hili. Kwa sababu kwamba wale wahusika wakuu wanaowaumiza watoto wetu hatujawatafuta, wenzetu kule Bara walitoa *line* fulani ya moja kwa moja kwa Mhe. Rais wakaambiwa wawe huru kusema lakini inatakiwa uwe na uhakika kweli. Mhe. Spika, hapa kwetu mpaka leo hakuna kitu kama hicho. Hilo nalo tuone kwamba litaweza kutusaidia asilimia kubwa kwani watatishika hapa itakuwa anajua wazi kwamba mimi fulani ananijua kuwa naleta kitu fulani. Mhe. Spika, ni kwamba mimi naona tutakuja kuimba hapa hapa kila siku huku watoto wetu wanateketea.

Mhe. Spika, mimi ingekuwa hakuna sheria tungesema kwamba hawa wanaokula basi tuwaachie kwa sababu huyu kama utamzuia yule mletaji yule atakula wapi, hatonunua maisha. Lakini leo tunampa fursa anaingia Uwanja wa Ndege bila ya wasi wasi. Mhe. Spika, ni kwamba sasa hivi ni hatari zaidi kwani hata hawa wawekezaji na wao wanaleta madawa ya kulevya. Tumepona hapo Mhe. Spika. Ni kwamba hatuponi kwani sio kitu cha mchezo, serikali lazima sasa hivi tukaze kamba ya sheria ili kulivalia njuga suala hili na kulitekeleza inavyohusika. Mhe. Spika, hatimae tutaimba kila siku huku watoto wetu wanateketea.

Mhe. Spika, nakupa mfano jirani yangu ameibiwa simu mbili, motto wenyewe ukiulizwa umri wake unaambiwa anaanzia miaka kumi na tatu, sababu ni kwamba anatafuta pesa ya kula unga. Mhe. Spika, hiki kitu sio cha kufanyia mchezo kwani vijana wanateketea, masomo hakuna sasa hivi, mtu mtoto wako ndani ya nyumba unamuogopa.

Mhe. Spika, tuangalie na hivi vitengo husika nataka nitoe historia ndogo tu ambayo nimeiona mimi mwenyewe na imenishangaza sana baada ya kuambiwa kesi ile imefutwa kutokana na kile kitu chenyewe kimekuwa sicho. Mhe. Spika, kwa kweli mimi nimesikitika sana kusikia jambo hilo ile tarehe nimeisahau, lakini *reference* ya kuona kile kitu nilichokishuhudia ninacho. Mhe. Spika, niliitwa kule kituo kidogo cha Kiwengwa kulikuwa na kete zimekamatwa ni nyingi kwa kweli, kete hizo nikaitwa mimi na Sheha na mama mmoja pale aliitwa ili kuja kufanya upekuzi na kuhakikisha kuwa ile shughuli inatoka ndani ya maungo yake.

Mhe. Spika, mimi maishani mwangu sijapata kuona unga, lakini siku hiyo nimeuona unga. Mhe. Spika, kete zake nikikuonesha na ule unga wake sijui nikupe mfano wa aina gani kwa sababu unaambiwa kile kipimo chake kinatokana na ukuche mdogo wa kidole unatiwa kwenye karatasi maalum ndio shilingi elfu mbili. Kwa kweli nimeshuhudia jambo hilo na nikahakikisha kama huu ni unga, sasa la kunishangaza mimi niliwaambiwa kwamba huyu mama itakuwa sio peke yake lazima kutakuwa na mwengine.

Kwa hivyo, hebu tuangalie tukae baada ya muda hatotokezea tajiri mwenyewe. Mhe. Spika, kwa kweli nilishangaa kwani tajiri alitokezea na kujinasibu na mimi shahidi nipo akasema kwamba mimi ndiye mwenyewe huyo mama muachieni. Mhe. Spika, anasema maneno hayo mbele ya kituo sisi mashahidi tupo, lakini chakushangaza nikawaambia mimi pale pale muhusika awapigie simu wakubwa wakasema kwamba ata huyo usimkamate muachie huyo.

Mhe. Spika, ndio mimi nikasema kwamba hii ni hatari na nilishangaa anasema kwamba wakubwa wote mimi nimeshawanunua, hilo nitakubaliana nae kwa sababu anajinata mbele ya kituo cha polisi. Mhe. Spika, wale askari waliokuwepo wananiambia mheshimiwa sisi hatuna amri yoyote kama unavyoona tumeshapiga simu kueleza hali hii tunaambiwa tumkamate huyu huyu. Kwa hivyo, sisi mheshimiwa sisi hatuna amri tena ndio tumeshagonga ukuta. Mhe. Spika, ndio kweli unga utaondoka hapa hali wenyewe kama hii.

Mhe. Spika, baada ya muda nakuja kupigiwa simu nakuja kuambiwa eti ule unga sio ni unga wa kaki, mimi nikamwambia Sheha wangu usinitanie hiyo haiwezekani, Sheha akaniambia kwamba unga sio na kesi imeshafutwa. Mhe. Spika, kweli mimi sioni lakini kwa jambo hili nimeliona wazi wazi mwisho

nakuja kuambiwa kwamba unga ni wa kaki. Mhe. Spika, mimi ndio maana nikasema kwamba sitounga mkono basi unikubalie kwa sababu inanisikitisha kusema kweli kwamba tuunge mkono basi na hizi sheria zifanye kazi, sio tunaunga mkono sheria tunaziacha kwenye meza yako Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kuna mambo mengine inabidi mtu anachekea uchungu. Mhe. Spika, na ushahidi mwengine katika hivi vitengo vyetu ikiwa utafanya kazi vizuri basi kesho unaondoshwa kwani unaambiwa hufai au atafanyiwa kila mbinu ionekane kwamba unga ameleta yeye ilimradi afanyiwe vituko ili aweze kuondoshwa watu wapate pesa. Mhe. Spika, unga hautoki hapa utakuwepo pale pale, halafu wajumbe wengi walichangia suala la ripoti hata na mimi nimepeleka ripoti pale Ngambu nikawaambia pahali fulani kuna tatizo limejitokeza. Askari wale walikuja kufanya kazi halafu wananiambia mheshimiwa tumeshafanya kazi sisi, wananijia mimi kunambia kwamba wameshafanya kazi, eti hiyo ndio siri mimi nimekwenda pale kwa siri.

Mimi nimeshangaa kuja askari kunambia kwamba wao wameshafanya kazi sasa walikuwa wanataka mimi nifanye jambo gani na wao ndio wajibu wao. Mhe. Spika, hii ndio hatari wenyewe tuliyokuwa nayo kwamba askari wetu hawawezi kuvumilia kuweka siri na jambo kama hili ni kitu hatari tusifichane. Mhe. Spika, kuna waheshimiwa humu wanayajua mambo mengi wanataka kusema lakini wanaogopa, mimi nimeshajitolea kama kufa nitakufa kwa sababu nzi kufa kwenye kidonda ni halali kabisa, na nakufa kwenye sheria ili kuwaokoa wale watoto wadogo wanaoteketea. Hilo ni lazima tulisemee hilo kama nilivyokueleza mheshimiwa kwamba leo mimi najilinda kwa kutoa habari hizo. Eti wanatoka askari wanakuja kunambia kwamba mheshimiwa sisi tumeshafanya kazi vizuri nini lengo lake pale. Mhe. Spika, usalama wangu unakuwa hatarini kwa sababu mimi nimekwenda kufanya siri, hatimae leo askari wetu wananiweka hadharani kuonesha kwamba mheshimiwa ulilokuja kulisema tumeshalijua.

Mhe. Spika, kama nilivyokwambia kwamba tuangalie vizuri sheria yetu na iweze kufanya kazi kwa mujibu wa sheria na serikali tuwe makini kuiangalia kwa hali na mali na uwezo huo upo. Mhe. Spika, hivi karibuni tumesikia mwekezaji mmoja amekamatwa na madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, sasa nije kwa huyu Mkemia hii hadithi ya kutuletea kwamba ni unga wa kaki, basi ajue kwamba anawateketeza ndugu zake. Kama tulivyosema katika kifungu cha sheria mtu kupigwa faini kwa milioni ishirini au kwa miaka saba haoni kitu kwake, kwa sababu leo una unachukua unga kutoka nchi za nje kuleta huku unapata milioni pengine milioni arubaini. Mhe. Spika, tungesema kwamba kanuni haitokosea tungeweka kifo moja kwa moja ingekuwa afadhali,

kwa sababu kuweka sheria ya milioni ishirini au kifungo cha miaka saba hilo bado unga utaendelea kila siku.

Mhe. Spika, mimi ningeomba kabisa hizi sheria tunazozitunga hebu serikali iweze kuzisimamia ipasavyo kabisa ili hali hiyo tuweze kuondokana nayo. Mhe. Spika, naona kama kungekuwa na sheria ya msimamo kabisa kuwa hili neno unga kuingia hapa nchini lisiingie kabisa isiwe sheria nyepesi kama hii ya sasa hivi.

Mhe. Spika, magendo ya karafuu kama sikusahau ilikuwa na sheria kali sana. Kwa hivyo, mimi naomba na sheria hii ya madawa ya kulevya iwe kali zaidi kwani suala hili ni lazima litiliwe mkazo kabisa ili kunusuru watoto wetu. Vyenginevyo watoto wetu wataharibika kwani hao ndio taifa letu la kesho.

Mhe. Spika, mimi sikuwa na mengi sana niliyoyasema ni hayo tu kwanza nataka kumnusuru waziri wangu hii sheria isimfanye aibebe yeye, wahusika wenye ubavu wapo pia apewe fedha za kukimu katika kile kitengo ili aweze kuwaendeleza hawa vijana wawe katika maadili mazuri.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuhudhuria katika kikao cha jioni ili kutekeleza majukumu ambayo tumepangiwa na wananchi wetu.

Mhe. Spika, baada ya hapo basi nichukue nafasi hii vile vile kukushuru wewe kunipatia nafasi hii na mimi kuwa mchangiaji jioni hii kwa Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji wake.

Mhe. Spika, kwanza nataka niseme kwamba mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wa Jimbo langu la Chaani tunaunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, niseme kwamba pamoja na kuunga kwangu mkono mswada huu, ningeomba kwa dhati kabisa na kwa imani yangu kwamba ili tuweze kutekeleza mswada huu vizuri basi lazima tunahitaji kuhakikisha kwamba tunakataza maovu. Mhe. Spika, kwa kuyaondoa maovu, au kuyazuia kwa macho basi tukishindwa Mwenyezi Mungu anatutaka tuchukie.

Mhe. Spika, mimi nataka tusichukue huko katika hatua ya mwisho kwamba tuchukie kwani bado uwezo wa kuzuia upo. Kwa hivyo, kama uwezo wa

kuzuia upo basi hebu tujirudishe na tujikumbushe kwamba mara baada ya Mapinduzi matukufu ya 1964 Mhe. Rais wa Zanzibar Marehemu Mzee Abeid Karume alituweka katika mahala ambapo kwamba sisi wananchi wa Zanzibar tunafurahia yale Mapinduzi matukufu. Kwa nini nikasema hivyo? Mhe. Spika, katika kipindi cha Rais wa kwanza hakukuwa na mtu ambaye anazembea haya masuala madogo madogo kwa sababu kwanza alikuwa anatisha, ile akikwita tu unasema hee mzee amenita hataki kuona serikali inachezewa.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, sisi ndio warithi kwa maana tumechaguliwa na wananchi leo tumekuja hapa katika Baraza lako tukufu, mimi sitaki nimlaumu kiongozi mmoja lakini nasema kwamba sisi ndio tutakaoulizwa kesho mbele ya haki. Mhe. Spika, kila mmoja wetu anategemea kwamba ikifika siku ya mwisho ya hesabu atakabidhiwa kitabu chake kwa mkono wa kulia na sio katika wale ambao watapewa katika mkono wa kushoto.

Mhe. Spika, ninachosema kwamba tukirudi katika dini ya Mwenyezi Mungu masuala mengi tutaepukana nayo, kwa sababu humu tutaepuka suala la rushwa, kutokuwajibika na mambo mengine yote. Mhe. Spika, kwa hivyo sheria hii ifanye kazi kama alivyosema Mhe. Aziza Nabahan Suleiman asubuhi kwamba yeye ana mtoto wake lakini kama huna mtoto basi una mdogo wako au mjuu wangu. Mimi nataka niseme na mimi nina mtoto wangu ni mtoto wa dada yangu.

Mhe. Spika, kijana huyu yuko Dar es Salaam kwa bahati nzuri na mimi kipindi fulani niliishi kwa muda mwingi, lakini kipindi chote ambacho mimi nipo pale hakuwa na matendo hayo. Baada ya muda akaja kuonekana na matatizo hayo, nilipokuwa nakwenda baada ya muda nilikuwa namuona anavuta sigara anajificha mwisho ikiwa anavuta hivi hivi. Kwa hivyo, kijana huyu amekuwa mtumiaji wa madawa ya kulevya Mwenyezi Mungu akamjaalia kuna siku alipata ajali ya kawaida kwenye gari na hiyo gari aliyopata ajali ilikuwa na bima kwa hivyo akalipwa na bima. Wakati alipolipwa na bima alipata fedha akanunua gari nyengine na gari hiyo akamkabidhi mdogo wake ikadumu ndani ya miezi sita tu, akawa ni mkali kila anachofahamishwa.

Kwa hivyo, mali ile ikenda ovyo mwisho ile gari ikauzwa na hatima yake ikawa hana chochote ni mtu ambaye sasa hivi hawezi kujitegemea kila kitu afanyiwe ni mtu ambaye alikuwa na nguvu na uwezo mkubwa. Mhe. Spika, hivi sasa ukimuona utasikitika kwani hawezi kufanya kitu chochote na hatusaidii chochote katika familia yetu isipokuwa kesi za kila siku. Mhe. Spika, hili jambo ambalo kila mmoja wetu anatakiwa alione kwamba lipo na linaweza likamtokezea wakati wowote.

Mhe. Spika, mimi nia yangu ni kutaka kuona mswada huu umekuja kwa ajili ya kuondoa haya madawa ya kulevya. Mhe. Spika, nataka tujipange vizuri na tukishajipanga vizuri basi hili linawezekana kwani tunaelewana kwa maana ya kwamba unajua wapi unga unauzwa, nani anauza na nani anatumia madawa.

Mhe. Spika, mimi nikubaliane na wale ambao wametoa mapendekezo kwamba hii adhabu kali imkute yule mletaji. Kwa sababu huyu mtumiaji wa madawa tunamuhitaji awe mtu mzuri na kwa sababu tunamuhitaji awe mzuri maana yake arekebishwe na vipi tutamrekebisha. Tumesema hapa kwamba kuna haja ya kuwa na kituo ambacho kitawekwa watu hawa kwa ajili ya kurekebishwa tabia na ushauri nasaha. Mhe. Spika, tulizungumza na wenzetu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii wametupa mifano hai ya kwamba kuna baadhi ya watu tayari wameweza kuwarudisha katika hali za kawaida baada ya kupata ushauri nasaha sasa hivi wamekuwa ni watu wazuri na wanafanya shughuli zao kama kawaida. Kwa hivyo, hawa nafikiria ndio jambo la kufanya tuwape matibabu mazuri.

Mhe. Spika, wale ambao wanaleta madawa tuone kwamba wanakomeshwa na narejea kusema kwamba hili tusimtazame fulani tu hili ni letu sote. Mhe. Spika, hili ni janga la taifa kwa hivyo linamuhusu kila mmoja inatakiwa kila mmoja aone kwamba anawajibika kwa nafasi aliyonayo kuona kwamba matendo haya hayaendelei tena.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kusema ni kwamba wizara husika imeona hapa inayohusika na madawa ya kulevya kwamba tatizo kubwa ni kwamba hizi kazi hazifanikiwi vizuri utekelezaji wake ni mgumu. Mhe. Spika, unapoweka masharti kwamba huyu mtuhumiwa wa madawa ya kulevya ameshakamatwa, lakini kuweza kufikishwa Mahakamani nani atamuhukumu lazima kuwe na Mahakama ya Rufaa na tunaelewa kuwa suala zima la Mahakama ya Rufaa kidogo lina tatizo kwa sababu Mahakimu ni wachache.

Kwa hivyo, moja kwa moja hapa ugumu utapatikana, lakini ingelionekana kwamba hili suala la madawa ya kulevya likaonekana kama ni suala la kawaida kama ilivyokuwa na tatizo Mahakama ya Ardhi. Mhe. Spika, tulikuwa na tatizo kubwa la Mahakama ya Ardhi kwani tulikuwa hatuna kwa hivyo kesi nyingi zikaonekana zinarundikana hazipatikani ufumbuzi. Kwa hivyo, kwa makusudi tumeamua kuwa na Mahakama ya Ardhi na hivi sasa sisemi kwamba tatizo limekwisha lakini tumepunguza kiasi fulani kwa sababu zile kesi zinakwenda katika Mahakama maalum. Kwa hivyo, na hili ni vyema likawekewa Mahakama maalum kwa sababu kesi ni nyingi, makosa ni mengi kwa hivyo kuna haja ya kuwa na Mahakama maalum ambayo itahusiana na kesi hizi tu. Kwa hivyo, tukifika mahala hapo basi ule urahisi wa kufanya kazi zetu utafanikiwa.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningetaka kulizungumza ni kwamba madawa ya kulevya mengi yanatoka nchi za nje sio kwamba inatoka hapa nchini kwetu ukiondoa bangi ambayo inaweza kuota mahala popote. Mhe. Spika, hapa Zanzibar tunakumbuka kwamba katika kipindi kile nilichozungumza cha Marehemu Mzee Abeid Amani Karume kwamba ukikamatwa na bangi basi unafungwa miaka kumi. Hapa hakukuwa na mtu pengine anaweza kuona kwamba mimi nina mkubwa fulani atanilinda kwa sababu kila mmoja alikuwa anaogopa. Kwa hivyo, mimi ningeomba sana ili tuondoe tatizo hili basi tuwe makini na sheria zetu baada ya kuzifanyia marekebishowatekelezaji wa sheria wanafanya kazi vizuri.

Mhe. Spika, kwa sababu madawa ya kulevya ni madawa ambayo ni haramu na kila jambo baya linakuwa na nguvu katika dunia maana yake hili suala lina fedha nyingi. Kwa hivyo, mtandao wa watu wake ni mkubwa, lakini huu mtandao unaweza kukatika tu baada ya kufanya kazi yetu vizuri. Mhe. Spika, ukimkamata mtu sisemi kama auliwe kwa sababu wenzetu duniani hawataki mtu auliwe kwa mazingira yoyote yale hata kama ameuwa. Mhe. Spika, ili arekebishike basi afungwe kifungo kikubwa.

Mhe. Spika, katika mswada huu kuna tume ambayo imeundwa humu baadhi wajumbe wenzangu wamezungumzia suala zima la tume na kutoa mapendekezo yao. Mhe. Spika, nilipokuwa nachangia sheria hii nimeona kwamba kuna haja ya kupunguza baadhi ya wajumbe hasa Waheshimiwa Mawaziri.

Mhe. Spika, hapa kuna Mwenyekiti ni Mhe. Waziri Kiongozi nakubali kwa sababu haya madawa ya kulevya yapo katika eneo lake, lakini Waziri wa Afya na yeye pia aingie hapa. Mhe. Spika, hapa mimi nafikiria kumuondoa Waziri wa Afya tungeongeza waziri mmoja ambaye katika orodha huu hayumo Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi kwa sababu humu bandarini na kwenye Viwanja vya Ndege ndimo yanamotoka madawa. Sasa kama ndimo yanamotoka madawa maana yake tuone kwamba anapewa uwezo na yeye kuona pale bandarini hakupatikani, hakutokei hayo matatizo. Kama atapatikana mtu ambaye anatokana na Wizara yetu ya Mawasiliano, sisi kama tutapata udhibiti kwamba mtu wetu ameshiriki jambo hilo kwanza tutamfukuza kazi, lakini baadae sheria ifuate.

Kwa wale ambao watakuwa ndani ya wizara nyengine basi nao vile vile Mhe. Spika, napendekeza wafukuzwe kazi. Kwanza ni kufukuzwa kazi halafu sheria nyengine ifuate. Isije ikawa lile suala la kwamba pengine mtu huyu anafungwa lakini akirudi anarudia kazini, ama kama ana mali anaendelea kuitumia. Kama inathibiti Mhe. Spika, na mali alizonazo basi zifilisiwe ziende serikalini.

Mhe. Spika, ukimfilisi mtu ambaye ana milioni au bilioni 20 na zinaeleweka katika *account* yake zimekuja serikalini baada ya kubainika kama anafanya kazi hii ya madawa ya kulevya, mimi nasema kwamba hili zoezi litakuwa zuri na tutahakikisha kwamba muda mfupi suala hili linaondoka. Lakini iwapo tutasema labda tumfunge jela miaka 10 au 5 akirudi ataendelea kufanya kazi hii. Kwa sababu kazi hii kwa watu ambao wanapenda maovu ni kazi njema kwao kwa sababu inawapatia fedha, haidhuru ni fedha haramu na ambazo zinaweza kumpelekea kupata matatizo huko mbele twendako.

Mhe. Spika, mimi katika mswada huu sikutaka nichangie sana, lakini niliona kuwa sitojitendea haki mimi mwenyewe pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Chaani kama sikuuchangia. Na sio maana kwamba sina mengi ya kuchangia, lakini nilitaka nichangie machache ili na wenzangu wapate nafasi, kwa sababu mswada huu ni wetu sote na kila mmoja ana uwezo wa kuuchangia. Huu si mswada wa kitaalamu ni mswada ambao una maeneo mengi ya kuchangia.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chaani, naunga mkono mswada huu ili uweze kutekeleza majukumu ambayo tutaupa. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kunipa nafasi ya kuchangia mswada huu. Nasema ninalazimika kuuunga mkono kwa sababu ya hii *line* niliyokuwepo. Huu ni mswada muhimu lakini pia ni mgumu sana. Mhe. Spika, mchango wangu utakuwa mdogo sana.

La pili napenda sana niwapongeze na niwasifu wakemia wetu, pamoja na kuandamwa kwao pengine wanafanya hivi, wana hivi, mimi nasema kwa kweli wakemia wetu ni waadilifu vya kutosha kabisa. Labda nitoe mfano, sina hakika na ingawa si malaika, lakini mwenzetu ambaye ameshafika mbele ya haki Marehemu Rashid Omar kwa wajihi wake tu hakuelekea kwamba awe mtu wa kutoa taarifa ya uongo. Alikuwa ni mtu muadilifu, mtu mkweli na kwa wale wanaomfahamu haiwezekani akaweza kutoa taarifa ya uongo kwa kazi.

Mhe. Spika, vile vile sina hakika kama ndiye au siye, anayekaimu nafasi ya Mkemia Mkuu hapa sasa hivi, kwa sura anaonekana kama ndiye, huyu mama kulia kwangu. Kwa wajihi wake, sura yake, ile *beautiness* yake haonekani kama kweli anaweza akatoa taarifa ya uongo, kwa hivyo hili tuliangalie. Lakini, nasema tena lakini, kwa Kingereza wanasema *but* na mimi naongezea *and a big but*. Hivyo kuanzia pale ulipokamatwa ule unga hiyo inayoitwa kama *cocaine*, nini na nini sijui? Kutoka pale mpaka siku ambayo utafika kwa mkemia hawa kati kati ni malaika? Tunawaamini kiasi gani?

Kwa hivyo, ni wazi kabisa unaweza ukakamatwa huo unga Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kasema baadae ukawa unga wakati sijui kutoka Kiwengwa huko au popote pale utachukua ikiwa siku moja au mbili, wale walioukamata mpaka wakaufikisha huku unakotakiwa kwenda tunajua wamefanya nini kati kati?

Wenzetu hawa wanaofanya biashara hii ni mahodari tayari, kwanza ana wakili wake na ameshamlipa pengine zaidi ya shilingi milioni mia moja kabla, anafanya biashara hiyo ameshamlipa. Anakuja kwa Mhe. Ame Mati ndiye mwanasheria, wakili anayejulikana anampa kabisa tena anamwambia, Mhe. Wakili nataka uwe mwanasheria wangu, mimi nafanya biashara ya unga, hamfichi, nafanya biashara ya unga kwa hivyo sijui wakati gani nitakamatwa, lakini siku nitakapokamatwa wewe ndiye mwanasheria wangu na anampa *advance* kabisa, pengine *hundred million* kwa wakili wake na ndio maana anakuwa na kiburi kama alivyosema Mhe. Makame Mshimba. Anasema huyu siye mwenyewe, mwenyewe ni mimi.

Mhe. Spika, katika kuweka sawa jambo hili la kati kati, kutoka kukamatwa mpaka kufikia kwa mkemia ambapo hujui siku gani! Mimi kabla ya kuja hapa kwenye siasa nilikuwa nikifanya kazi ya *audit* karibu miaka 20, tulikuwa na utaratibu wa kufanya ile tunayoiita *surprising audit*, unakwenda pale bahati mbaya pengine umekwenda *cashier* hayupo kwa sababu mkienda hamsemi na mkifika pale mkimkuta unachomwambia ni kwamba tunaomba ufungue *safe* lako tuone fedha ulizokuwanazo, mnazihesabu kutokana na *document* zake. Lakini kama hayupo hamna tatizo wala hamsemi kwa nini ameondoka, unachofanya unachukua karatasi tu ndogo, unaiweka pale unatia saini yako ukisha unaziba kwenye tundu pale kwa gundi ambayo una hakika hii haiwezi kutoka. Akija yeye akitaka kufungua kama alikuwa na madudu yake pale hawezi, kwa sababu akiifungua ataichana, akishaichana maana yake kesho mkija mtamwambia hapa jana tulizuia hii makusudi usifungue kwa nini umefungua?

Nilichokuwa nataka kusema lazima kuwe na utaratibu kuanzia siku pale *point* inapokamatwa, wapi unahifadhiwa mpaka siku ambayo utamfika mkemia, lakini hivi hivi katika *loose cargo* kwa sababu ndio mzigo mnasema, wanatumia neno kontena. Katika hiyo *loose cargo* ni kweli leo utakuwa unga wa kaki, kesho unga wa saruji, keshokutwa na mtondogoo unga wa nini siuji? Kidole hiki cha shahada Mhe. Spika, uzuri wake msikitini tu, lakini pengine popote sikizuri, mtu akikunyooshea kidole hiki anakuapiza na utakwenda tu. Kwa hivyo, kutoka hapo tunamuelekeza kidole mkemia ametupa ripoti ya uongo, amesema huu unga wa sembe, lakini huku ulikotoka hatuangalii. Sasa nasema tuwe waangalifu sana katika jambo hili vyenginevyo tutawaandama wenzetu hawa, tutawaonea, tutawafukuza, kumbe ni msururu umeanzia mbali.

Mhe. Spika, hakuna hata mmoja katika familia zetu kama vile ambavyo hakuna hata mmoja katika familia zetu hapa Tanzania ambaye hajaathirika kwa namna moja au nyengine na UKIMWI, ama mwanawe, mjukuu wake, jirani yake, rafiki yake, anayemjua tayari ameshapotea. Hivyo hivyo, na ndani ya suala hili la unga.

Mhe. Spika, hapa ndani ya Baraza tupo hapa kuna watoto wetu wa kuwazaa tumo humu, akiondoka ana wasi wasi nyumbani kwake hajui akirudi atakuta nini kimechukuliwa! Kwa hivyo, kwa kifupi kila mmoja ameathirika. Wakati mwengine sitetei, wale wanaopika gongo msije mkasema kwa kuwa kule jimboni kwangu, lakini tunawaonea, tunakwenda pale tunawashika, tunawa*haras* wakati gongo haileti madhara kwa jamii inaleta madhara kwake mwenyewe, *alcohol* ile inamuathiri mwenyewe, sigara inamuathiri mvuta sigara.

Wakati mwengine Mhe. Spika, samahani, hata bangi inamuathiri *simple* mtu mmoja tu, lakini anayekula unga Mhe. Spika, nataka waniwie radhi dada zangu. Kwa sababu mla unga yule anaiba chochote, mtu amethubutu katika kuiba mpaka chupi ya mama yake ameiiba! hii ni fedheha, aibu. Sasa utaona athari hiyo, ndio maana nikasema siwatetei wapika gongo, lakini kila siku vyombo vyetu vinawakamata wapika gongo. Hawa wanaoleta unga hatuwakamati, hatuwaoni, hatuwajui, ni jambo ambalo unaweza ukashangaa!

Sasa nasema tuangalie, kama tunamudu kuja Kiboje, kwenda Bumbwisudi, Fuoni tukapeleka watu wetu wakamate wapika tende, iweje tukashindwa kuwakamata wale wanaoleta hizo kontena na tunawajua, hata maeneo yanayouzwa? Hivi sasa unga hauuzwi kwa siri, kabisa hauuzwi kwa siri! Unaweza ukaona mtu anaingia tu pale ‘vup’ ameondoka, ni kitendo cha dakika moja tu, na yule muuzaji nadhani anakuwepo pale sawa sawa na pale hospitali penye kidirisha panapotolewa madawa, mgojwa anapokwenda na cheti akapeleka basi na pale akifika hata dakika moja au nusu dakika nyingi, anafika anapeleka mkono anatoka!

Tunaona lakini hata watu wetu huko mitaani nao ni wabaya, wanalalamika hawasemi, unga unauzwa nyumba ya pili kwa jirani yake anaona, labda ndio hivyo anahofia kama yale ya Mhe. Makame Mshimba akaja kuambiwa baadae Mheshimiwa tumeshafanya kazi nzuri na akapeleka taarifa hii. Sasa nasema ukweli katika suala hili vita hivi ni vya wote, si vya polisi, sheha, mwakilishi, diwani, Kificho, Tafana ni vyetu sote. Kama kweli tutajidhatiti kabisa hili linawezekana.

Lakini jengine nataka kusema kutunga sheria ni kitu chengine, na kusimamia na kutekeleza ni kitu chengine. Nataka nitoe mfano, tuna utaratibu wa nchi hii wa ajabu tu. Agizo atoe Rais au atoe *Chief* basi litafuatwa kwa siku mbili tatu, watu watakimbizana mbio, baada ya mwezi tunasahau, tena sijuikama ni sheria au agizo la Mhe. Waziri Kiongozi hapa la mifuko ya *plastic* iko wapi? Ilikuwa inauzwa kwa siri sasa inauzwa hivi hivi *jahara l-fasada!* Wanasubiri Waziri Kiongozi akae pale akifunga hotuba yake keshokutwa aseme tena, akisema tutakurupuka siku mbili tatu tutasema aa! *Chief* keshasahau tunaanza tena, tunakwenda wapi? Nataka nikupeni mfano huo tu.

Tulikuwa na sheria ya *helme*t hapa, ilipoanza sheria ile askari walikuwa wakali iko wapi sasa hivi? Kwa hivyo, hata hii sheria ambayo leo tunaitunga tumekaa hapa Mhe. Spika, tumeshapewa posho *alhamdulillahi* zinatusaidia huko, lakini utekelezaji wake ndio tatizo. Ndio maana nikasema sheria hii tusiachie kundi fulani tu aa, ni yetu sote.

Mhe. Spika, nije kwenye ukurasa wa 111 kifungu cha 4(1), imeanzishwa Tume ya Kitaifa kuratibu udhibiti wa madawa ya kulevya, kuna msururu mkubwa wa watu, Waziri Kiongozi, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, na wengineo; ingawa pia wako Kamishna wa Polisi. Lakini naomba katika orodha hii tuwaingize wenzetu pamoja na kwamba yupo Kamishna wa Polisi pale, lakini tumuingize Mkuu wa Kitengo cha ile *dog section.* Mhe. Waziri unanielewa? Napendekeza mkuu wa mbwa wa polisi tumuingize, pengine si ajabu kamishna ata hajui utaratibu wa mbwa wake wa polisi, anajua wapo lakini huyu wa mbwa mkuu pale awepo.

Nasema awepo kwa sababu nina kumbukumbu, tulitoa vijana hapa wakaenda Afrika ya Kusini na mbwa wao wale. Mbwa wale walikwenda kujifunza kule, sina hakika kama mbwa wale wako hai au washakufa? Wameshakufa ee? Kama mbwa keshakufa tumekaa tutaweza ku *detect* kweli? Sio rahisi.

Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Spika, mtu huyo wa *section* ya mbwa awepo aongezewe ili aweze kutoa mchango mkubwa kuliko kundi hili kubwa ambalo tumeliweka hapa. Wako wataalamu kweli lakini bado nadhani mtu wa mbwa awepo.

Mhe. Spika, nasema hivyo siku moja sitaki kusema ni sehemu gani nilikuwa nimekwenda na rafiki yangu mmoja. Mimi mbwa nawapenda sana Mhe. Spika, sana tena, tulikuwa tumekwenda huko na rafiki yangu mmoja amechukua mbwa wake kwenye gari baadae tukenda na baadae akanambia “Tafana turudi hii sehemu sio nzuri”, nikamwambia twende zetu tu, baadae akanambia “Unajua kwa nini nimekwambia turudi”? Nikamwambia sijui, akasema huyu mbwa wangu anaelewa ku *detect* madawa ya kulevya, sasa kule alikuwa

ananipa tabu huyu mbwa, ina maana pale kuna nyumba ambayo tulipita karibu inauzwa madawa ya kulevya. Kwa hivyo, ndio maana nazungumza umuhimu wa kumuongeza Mkuu wa Kitengo cha Mbwa hawa wa Polisi.

Jengine nije kwenye ukurasa wa 114 kifungu cha 12. Mhe. Spika, kinasema Mfuko wa udhibiti wa matumizi wa madawa ya kulevya. Kumetajwa hapa vipi tutaweza kupata fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli zetu hizi. Lakini kwa namna nilivyoona hapa Mhe. Spika, hatujakuwa *serious* kabisa, ninazo sababu. Ukiacha fedha iliyotengwa na serikali kwa Mfuko huu, kuna zile njia za kupatia fedha, kwanza kuna (a) fedha iliyotengwa na serikali kwa Mfuko, ni sawa kabisa. Pili (b) anasema mapato ya asilimia 25 ya mauzo ya mali iliyofilisiwa chini ya sehemu ya 7 ya sheria hii.
Mhe. Spika, hivyo hiyo mali itakayofilisiwa itafilisiwa lini? itakamatwa lini? na pindipo hakuna mali iliyokamatwa maana yake hakuna kitakachofilisiwa na kama hakutakuwa na kitu hicho maana yake hakutakuwa na fedha itakayopatikana kutokana na kifungu hiki. Kwa hivyo, kuwepo kwa kifungu hiki hapa haioneshi ile *seriousness* ya Mfuko huu namna gani utapata fedha.
Lakini (c) ruzuku zote zitakazotolewa na mtu. Ruzuku hizo nani atatoa? Hao watu tuna miadi nao wa kutupa hizo ruzuku. Hebu tuliangalie hili.

Tatu anasema mapato yote kutokana na kitega uchumi cha kiasi cha fedha kilichoelekezwa kwa Mfuko chini ya masharti ya sheria hii. Sina hakika kitega uchumi hicho ni cha aina gani? Ninachotaka kusema kama jambo hili tunataka lifanikiwe ni lazima serikali itenge fedha kwa ajili yake tusitegemee mjomba, ruzuku watokee wajomba hawakutokea, au mali itakayofilisiwa, haikufilisiwa, haikupatikana, kwanza kesi yenyewe hata kama mtu akikamatwa mwaka mzima haijesha na huwezi ukaihimiza, wakati huo unahitaji fedha kweli ndio unasema kesi imalizike labda utaweza kufilisi hiyo mali.

Kule Bara walikamata samaki ambao walivuliwa kinyume cha sheria sasa hivi sijui mwezi wa ngapi wako kule kesi haijesha. Hizo gharama zishakuwa kubwa zaidi kuliko thamani ya samaki wenyewe. Sasa nasema kifungu vipi tutapata fedha tukiangalie upya, ni lazima kwa kweli serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya shughuli hizi na sio kutegemea ruzuku ambayo hatuna uhakika nayo. Tunageuka *taxi driver* kwa sababu yeye anamngoja mtu hana miadi nae.

Mhe. Spika, kuna ukurasa mwengine huu wa 122 kifungu cha 40 wajibu wa wamiliki wa ardhi kutoa taarifa za ukulima wa mazao usio halali. Mhe. Spika, inawezekana tukaja kuwaadhibu watu kwa kifungu hiki, tunao utaratibu mtu unaweza kuwa unalo shamba lako Mhe. Samia Suluhu ana shamba lake hapa lakini sio yeye anayelilima, pengine yeye analima sehemu ndogo tu ya shamba lake sehemu iliyobaki tuna utaratibu wa kuwaazima watu, mtu unaemuazima

mle ndiye anayepata nafasi ya kukusafishia shamba lako, mle atalima bangi, atalima nini , Mhe. Samia yeye haijui hata akiiona.

Mhe. Spika, lakini baadae atokee mtu tu, na Mhe. Samia anamjua tu huyu anakuja kugombea jimbo la Uzini nampatia hapa hapa kwa sababu shambani kwake kunalimwa bangi, siku zote hizo sijamuona lakini kwa sababu anakuja Jimbo la Uzini nataka nimtoe kwa *technical knock out* tunaita ile, basi mimi nakwenda kwenye vyombo vinavyohusika nasema shambani kule kwa Mhe. Samia analima bangi, hili shamba lake masikini ya Mungu anakuja pale anachukuliwa anakwenda huku mpaka ikija kubainika kwamba Mhe. Samia siye wala hajui, kweli shamba lake lakini hajui chochote muda umeshapita.

Kwa hivyo, nasema katika kiumbe ambaye ana akili ni binadamu na sijui kama *airport* na bandarini wapo wanao uhodari wa kuweza kuwatambua watu wenye unga. Mhe. Spika, leo hii naweza nikatoka Dar es Salaam nikaja na unga na nikaja nao mkononi, nikapita bandarini nisikamatwe na wasijue, siwezi kusema hapa naweza kufanya vipi wasijue ambapo tutasema unga unapita bandarini ni kwa taratibu zake unaweza kusema ni za kipumbavu sana mtu anapita pale wala humjui, na anapita nao hivi hivi na siajabu wewe ndio ukampokea. Kwa sababu wenzetu wamejiandaa kwa sababu wanajua nani adui yake na vipi afanye.
Labda nitoe mfano, hivyo nichukue unga niutie ndani ya mpira huu wa *football* kwa kawaida tu mle nakuja nao kwenye nyavu najua nina timu zangu za jimboni napita nao pale pale nimeikamata, askari wanaoangalia pale wataangalia kwenye mipira? Ataangalia kwenye mizigo niliyofunga hatoangalia kwenye mipira na hivyo hivyo kuna vitu vya aina hiyo vingi vinatumika vinapita pale, tunaweza tukawalaumu bandari, tukawalaumu *airport* lakini kabisa katika akili yake mtu haiwezi kumjia. Sasa kwa kweli si rahisi kuwakamata watu hawa kwa urahisi pale bandarini na *airport* na tukitilia maanani kwa Mhe. Samia Suluhu anavyoninong'oneza hatuna mbwa.

Mhe. Spika, naomba niseme ni lazima tuwe na mbwa ambao wamejifunza mambo haya ya madawa ya kulevya na mbwa hao inawezekana wakatushinda kwa sababu hawa mbwa hawatakiwi wapikiwe sembe. Kwa sababu mbwa wetu wa polisi pale chakula chao sembe tu, mimi kwa sababu nilikuwa napenda sana mbwa na ninawasifu sana watu wa polisi pale. Kwa sababu Mheshimiwa naweza kuwa na tatizo nikenda saa nane za usiku wakanisaidia, lakini mbwa wetu wale chakula chao sembe tu, mbwa wale ni mbwa maalum apigishwe msuwaki, apelekwe saluni, sio mbwa tu hivi hivi, chakula chake makusudi kinaagiziwa tutaweza? Na ndio maana nikasema ile namna ya kupata fedha tunatakiwa tujifunge mkaja kweli vyenginevyo *never.*

Kwa hivyo, nasema kitengo kile cha *dog section* kiimarishwe na wapewe nyenzo, vijana wale wapewe taaluma wale wanaokwenda sasa hivi mmoja nilimkuta Chwaka hivi karibuni nikamuuliza uko huku wewe? Akanijibu ndio, wewe si ulikwenda Afrika ya Kusini kwa mafunzo ya mbwa wale na sasa uko Chwaka unasubiri gari zilizojaa abiria? Sasa unapeleka watu kujifunza akirudi hapa kwa sababu alichokwenda kujifunza hawezi kukitumia kwa vile hana nyenzo. Kwa hivyo, nashauri tuliangalie hilo.

Jengine labda niulize Mhe. Spika, sina hakika kama kweli Mhe. Waziri atanambia, inasemekana wakati wa vita askari bangi ni sehemu yao ya *ration*, sina hakika kama lina ukweli au vipi. Nasema kwa sababu linamuongezea mori, hatuko kwenye vita lakini kwa mfano ikitokea hivyo inakuwaje? Nasema sina hakika hilo.
Jambo la mwisho Mhe. Spika, tuna sheria humu ngumu kweli, faini ya shilingi milioni ngapi, miaka mingapi, ukubwa wa hizi faini zinatoa mwanya mkubwa wa rushwa. Nasema ukubwa wa hizi faini mamilioni mwengi mengi tu, sijui milioni 30, 40, hizi faini kwa kweli Mhe. Spika, zinatoa nafasi kubwa ya rushwa kwa wale watu ambao watakuwa wanafanya kazi hizo.

Kwa mfano, mtu amekamatwa na unga na akapelekwa kwenye vyombo vya sheria kama vile alivyosema Mhe. Makame Mshimba, amekamatwa askari aliyemkamata akawa mtiifu kweli, akawa muaminifu kweli, akawa anawajibika kweli, na pengine alishawishiwa akapewa shilingi milioni kumi akazikataa kwa sababu ya ule uchungu aliokuwanao. Kwa sababu pengine anaona namna gani mwanawe alivyoathirika, jamii inavyoathirika, akawa muungwana akakataa akasema hapana, lakini baada ya wiki au mwezi mtu yule yule aliyekamatwa anapita mbele yake anadunda, vijana ndivyo wanavyosema siku hizi anamwambia utakufa masikini hivyo hivyo, anaifikiri ile kwamba nitakufa masikini, niliacha milioni kumi hizi kuna mwenzangu amezichukua, huyu niliyemkamata leo anapita mbele yangu hapa anadunda ananambia nitakufa masikini, kesho hakubali tena kufa masikini, hatakubali kamwe atasema jana nimetimiza wajibu wangu lakini kumbe kuna mwenzangu hakutimiza wajibu wake. Kwa hiyo na hili tuliangalie.

Mhe. Spika, wakati fulani hapa ndio tulikuwa bado tuko wageni na Mhe. Ame Mati Wadi tukapitisha sheria moja hapa kwa makofi ya mambo ya mazingira, mambo ya mchanga nadhani iko mpaka leo. Gari itakayokamatwa na mchanga inafilisiwa.

Mhe. Spika, ikatokea siku moja Mhe. Ame Mati Wadi mpiga kura wake mmoja kakamatwa na mchanga, akanambia mimi lakini wakati ule nilikuwa mgeni, ningelikuwa nimeshalizoea Baraza nisingeipitisha hii sheria. Kwa sababu unaangalia ile thamani ya mchanga kweli ni athari ya mazingira, lakini

umeweka sheria ya kuifilisi ile gari. Gari ule mchanga aliochukua ni 40,000 na wakati ule ilikuwa nafikiri 20, 25, thamani ya gari ni milioni 5 na 10, lakini tukasema hapa unafilisi gari kitu ambacho kilikuwa haiwezekani. Kwa hiyo, kwa *formula* ile ile ilikuwa imetoa mwanya wa rushwa. Nasema tuwe waangalifu na jambo hili. Sheria ni nzuri, utekelezaji wake ni muhimu. Kuathirika tunaathirika, hakuna jamii kati yetu ambayo haijaathirika kwa namna moja au nyengine.

Nilisikia sasa hivi dada zangu na kaka zangu mtanisamehe hata *saloon* humu na kwa vinyozi namo mnauzwa unga, sina hakika lakini wanasema hivyo. Nani inaweza kumjia kama *saloon* pale ambapo watoto wazuri kama Mhe. Aziza Nabahan Suleiman wanakwenda pale kujipamba wakapambuliwa wakapendeza tukawapenda leo mnauzwa unga. Lazima nimtanie dada yangu huyu tunatoka Kiboje sote kule, usipomtania dada yako wa baba mkubwa na mdogo utamtania nani.

Lakini mazingira kama haya kwa vinyozi hawa sasa kunauzwa unga. Mhe. Spika, hali ni mbaya, hali ni ngumu, nasema hakuna lisilowezekana. Rais Barack Obama amesema pale *"Yes we can".* Nasema hili tunaweza kama sote kwa pamoja tutajifunga mkaja wenzetu wakicheza basi sisi tudemke. Mnajua kudemka eee mshanifahamu.

Mhe. Spika, la mwisho nisije nikasahau jana kwenye semina ile wakati wa majibu kuna kitu mimi sikiamini, wanasema ule muda inawezekana kukatokea *chemical reaction.* Mimi siamini kwa muda mfupi kama kweli unga ule unaweza uka-*change* mpaka ukapata kitu kipya, si kweli. Hii sumu ya panya hata ukiambiwa imesha-*expire* kaijaribu. *(Kicheko)*

Leo wanakaa wataalam pale wanatwambia kwa kipindi kifupi kunatokea *chemical reaction.* Aaa jamani, ikiwepo hiyo inakuwa unga wa kibuki, si kweli. Kwa kawaida Mhe. Spika, wanavyosema kwa mfano pombe ingawa pombe sio madawa ya kulevya lakini kidogo inaleta ile nishai, pombe kadri ikikaa sana ndio inakuwa *more strong.*

Kuna meli moja ambayo ilizama zaidi ya miaka 40 iliyopita karibuni imeonekana na ile meli inasema haikuwa na bidhaa yoyote zaidi ya pombe na vifuniko vya chupa ilikuwa vile vya plastiki. Waliposema pombe ile ilikuwa bado ni nzima, makampuni mbali mbali yalikuwa yanagombea tenda ya kwenda kutoa ile kwa sababu ilikuwa ni pombe sasa imeshakaa muda mrefu na ni kali sana. Leo ukaseme ime-*mature* muda sijui wa miezi miwili kukatokee *chemical reaction, chemical reaction* hiyo mpaka ilete kitu kipya, kitu kipya hicho basi iwe hamna hata ile *substance* moja inayoonesha hiyo *cocaine* sijui *heroine,* hili haliwezekani. Hili jana kwa sababu hapa chombo chako hiki ikiwa

ni semina, ikiwa ni Baraza, kina utaratibu wake, huwezi ukamwambia mtu mwongo unanidanganya.

Lakini jana nilipokuwa namsikiliza yule bwana pale nikasema hawa wasomi wana hatari zao. Mhe. Spika, hili la kusema katika kipindi kifupi kunatokea *chemical reaction*, hiyo ndio tunatoa mwanya sasa kusema hayo tunayoyasema.

Mhe. Spika, baada ya hayo, nasema kazi ya kupambana na madawa ya kulevya ni yetu sote. Napendekeza kitengo cha mbwa kiimarishwe vya kutosha.

Kwa mfano sasa hivi Mhe. Rais au kiongozi yeyote anapokuja katika maeneo tunapeleka mbwa wana-*detect* mle, yule mbwa anayekwenda ku-*detect* pale hajui chochote, anachokijua pale ni baruti, aina ya silaha ile harufu ndio anayojua yeye. Anakwenda pale ana-*detect* hakuna silaha iliyofichwa hapa. Hakukemezi yule, hata ukiwa unaiba pale hajui, yeye amefundishwa kufahamu miripuko, silaha, ndio maana anapokwenda kiongozi pale tunampeleka. Mhe. Spika, Wamarekani hata wale askari wao hawawaamini wanawaamini mbwa.

Mhe. Spika, alipokuja Mama Laura Bush wameleta askari hapa, madege na nini, wote hawakuamini wakaja kuamini mbwa, mbwa aliposema hapa ni salama basi waliamini zaidi. Kwa hiyo, ndio maana nikawa nasisitiza sana kitengo hiki cha mbwa ni muhimu na ni lazima. Mhe. Spika, mbwa hawa waweze kutumika, tunashuka na mizigo yetu pale bandarini awepo.

Mhe. Spika, kuna watu wanasema mbwa ni haramu, si kweli na aje shekhe anambie mbwa haramu, uharamu wa mbwa upo kwa namna yake, mbwa anakuwa haramu kwa namna hii na kwa namna hii mbwa anakuwa si haramu. Sasa mbwa anakwenda pale ananusa mizigo, tunaanza kusema hii serikali inatuletea mbwa ananusa mizigo yetu, hanusi mizigo yako. Wenzetu hawa wanakuwa waangalifu sana kuona mbwa haharibu wala hatii najsi katika hali hiyo. Mhe. Spika, jengine tukamatane sote.

Mhe. Spika, baada ya haya, nasema naunga mkono mswada huu na wenzetu tuwasaidie vya kutosha. Tunawapongeza sana wakemia wetu na kama ndio huyu mama kwa sura ana-*act* nataka Mwenyezi Mungu amjaalie awe hivyo hivyo. Kwa ninavyomtazama kwa sababu unajua kwenye TV watu wengi wanafuata kipindi chake siku hizi. Kwa hivyo, nina imani kabisa kwa alivyo hawezi kutuletea unga huu kesho akasema hii kaki, hawezi akapelekewa unga akasema hii sembe, hawezi kupelekewa hii *brown sugar* sijui nini akasema vyengine.

Mhe. Spika, nataka niwapongeze wote, kama binadamu inawezekana wakawa na kasoro zao ndogo ndogo za hapa na pale, lakini kasoro hizo haziwafanyi

kwamba tusiwaamini. Tuwaamini, tuwape kazi, tukubali kazi zao, lakini tukubali kuona mianya hii midogo midogo ya njiani nayo tunaidhibiti. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kuwa mzima wakati huu na kuzungumza yale mambo ambayo Wazanzibari wanapenda yasiwepo. Pili nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuchangia mswada huu utakaojulikana kama Sheria ya Kufuta Sheria ya Madawa Haramu Nam. 16 ya Mwaka 2003 na Kutunga Sheria Mpya ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya na Kuweka Masharti ya Uuzaji, Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Nakotiki na aina za Saikotropiki na utekelezaji wake.

Mhe. Spika, ukikisoma hiki kichwa cha maneno kama si mimi Mjumbe wa Kamati utahisi kwamba serikali ina utaratibu wa usafirishaji wa madawa haramu. Hata mimi nilipokuwa mjumbe nilikuwa na hoja hiyo kuona hivyo kumbe serikali ina utaratibu wa kuuza madawa haramu ya kulevya. Lakini nikaambiwa kumbe serikali huwa inahitaji madawa ya kulevya kwa madhumuni maalum.

Kwa hivyo, inapotokea haja ya kuwa madawa haya yaingizwe nchini basi pia huwa yanaingizwa, yanasafirishwa, yanatolewa. Lakini tunachotaka kujua kwamba serikali katika hili lazima iwe na udhibiti mzuri ili wale watakaohalalishwa kuingiza madawa ya kulevya basi wawe waaminifu kwa sababu Wazanzibari wengi ni maskini.

Nasema hili kwa sababu miaka iliyopita tulihalalisha vituo vya afya maeneo mbali mbali na tukategemea kwamba masoko ya madawa wataagizishia nje. Lakini wengine walitugeuka maafisa wale au madaktari fulani wanazitoa zile zile zetu kwa mlango wa nyuma tunauziwa. Kwa hivyo, katika nchi hutakiwa kwamba watu wote wawe makini juu ya jambo ambalo linakatazwa.

Mhe. Spika, kwanza nilipendelea kuzungumza kwamba sisi wenyewe tuwe makini na lazima tuone kwamba tunafanya kazi kama vile ambavyo sheria inaagiza.

Mhe. Spika, la pili nataka kuzungumza kwamba kwa mswada huu tuwe pamoja sote kuunga mkono kama tulivyounga mkono hoja ya mafuta Zanzibar. Kwa sababu inaonekana katika mswada huu watu wengi sana wameathirika na katika kuathirika hakuna chama wala mkakati. Kwa hivyo, sote tunapiga vita kitu hiki. Sasa mimi nitakuja kushangaa jinsi vile Mhe. Mjumbe Aziza Nabahan Suleiman alivyochangia asubuhi analia, anasikitika mtoto wake kaumia na watoto wa jirani, lakini wakati wa kuja kupitisha mswada ikawa

yeye hatumjui kama kaunga mkono au kakataa, maana atakuwa hanyanyui kwa kuunga mkono wala hanyanyui kwa kupinga.

Mhe. Spika, jana wanasemina walitwambia kwamba lile tatizo ambalo lilitokea kabla ya sheria hii itakayopitishwa ya kuwa kesi zinapelekwa Mahakamani hazipati ufumbuzi, ulikuwa ni utaratibu wa Mahakama ulivyopangwa juu ya kesi za madawa ya kulevya, ilikuwa haitoi ruhusa ya urahisi ya kuendesha kesi. Sasa hivi kwa mujibu wa sheria hii inavyotungwa itakuwa na urahisi wa kwamba kesi zinakwenda.

Watu wanasema njia ya muongo fupi, hebu tuungeni mkono tuangalie. Bado mrundikano wa kesi utakuwa kama ule na kesi haziendi? Kama zitakuwa haziendi tutajua pana namna, lakini kama baada ya kupita sheria hii kwa mujibu wa semina ya jana kesi zitakuwa zinakwenda, basi ni jambo la msingi kuona kwamba marekebisho ya sheria hii itakuwa imefanya kazi. Kwa hivyo, nawaomba wajumbe tujitahidi kuchangia na kuboresha lakini mwisho tuunge mkono tusimamie utekelezaji wake.

Mhe. Spika, katika mswada huu mimi ningeanzia na sehemu ya pili ukurasa wa 111 hasa kifungu cha 3. Mhe. Spika, katika nchi yoyote serikali haitakiwi ifanye kazi peke yake, lakini majukumu ya serikali ni kuandaa utaratibu. Mhe. Spika, katika kifungu cha 3 (1) naomba ninukuu kwa ruhusa yako. Maneno ya pembeni “Jukumu la Serikali ni kuchukua hatua za kuzuia matumizi mabaya ya madawa ya kulevya”.

Sasa kuzuia madawa kwa upande wa serikali ni kuweka zile taratibu ambazo kama zilivyoandikwa hapa.

Kifungu cha 3 (1):

> “Bila ya kuathiri masharti ya sheria hii serikali itachukua hatua zote zinazofaa kwa ajili ya kuzuia na kupiga vita matumizi mabaya ya madawa ya kulevya.”

Mhe. Spika, hii kazi ya serikali kuzuia madawa ya kulevya. Wajumbe wengi walichangia kwamba utaratibu iliopanga serikali kwa sheria iliyopita ilikuwa haitoi tafsiri nzuri juu ya kuendesha kesi Mahakamani katika kushughulikia madawa ya kulevya. Sasa serikali imejiamini kuweka utaratibu mzuri wa kuzuia madawa ya kulevya. Kwa hivyo, nawaomba tena wajumbe kwamba tuunge mkono mswada huu ili tuangalie hatma ya baadae.

Mhe. Spika, kifungu cha 4 (1) inaonekana kwamba serikali kweli imejiandaa. Kwa sababu miswada iliyopita Mhe. Makame Mshimba Mbarouk aliona

kwamba bado serikali haijakusudia kupiga vita madawa ya kulevya, alihisi kwamba Mwenyekiti wa Tume atakuwa Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. Mwenyekiti atakuwa Mhe. Waziri Kiongozi na sote tunamuamini, au nani hamuamini kwa kufanya kazi, maadam kimya wote wanamuamini.

Sasa hii tume itakuwa haina sababu ya kuona kwamba haifanyi kazi zake vizuri. Kwa hivyo, serikali imepania na inaonekana itafanya kazi vizuri. Wajumbe wale waliotajwa sina shaka nao, sio kwamba watafuata posho tu, lakini watakwenda kufanya kazi kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Spika, ukurasa wa 112 kifungu cha 5 kinasema "Mikutano ya Tume" naomba kunukuu kistari chake kidogo tu lakini kina maana kubwa.

Kifungu cha 5 (1):

> "Tume itafanya mikutano yake mara nne kwa mwaka".

Hapa inaonekana kila ripoti ya miezi mitatu ya tume itapatikana. Bahati nzuri kuna kifungu cha 8 kinasema kwamba "Ripoti hii ya tume itachapishwa na kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi".

Sasa itakapokuja huku ndani ya mwaka mmoja tutaijadili upya. Kwa nini tusiamini kwamba serikali sasa hivi imekusudia kweli kweli. Nawaomba tena Waheshimiwa Wajumbe tuichangie, tuiunge mkono, tuje tuiulize.

Kwa bahati nzuri mimi bado ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii na tunakuwa tunapata muda wa kupitia kamati kila kipindi kila mmoja kwa wakati wake. Nilikuwa nashawishika sana na Kamati ya Fedha na Uchumi lakini baada ya kuona kwamba kamati hii ndio yenyewe hasa ya kushughulikia jamii, basi nimeona bora kamati hii kuliko ile Kamati ya Fedha na Uchumi. Kwa sababu tutapata kuona na ningemuomba Mhe. Spika, akaona kwamba kila kipindi tunakwenda kuyaona maendeleo ya tume hii. Katika kila miezi mitatu ya Kamati ya Baraza hii lazima tuwe tunashughulikia sana na ikiwezekana ripoti tunayoleta hapa Barazani tuijadili kweli kweli kwa kina. Hapa tutakuwa sisi tumeshirikiana na serikali kuihoji matumizi yake lakini pia kuihoji kazi zake.

Mhe. Spika, niombe tu kwamba serikali yenyewe ikubali sisi kuiuliza. Kwa sababu unajua wakati mwengine inaweza kuundwa kwa mfano Tume ya Ukimwi, hupati ripoti yoyote labda pale unapokwenda kwenye kamati tu kidogo ndio unapata hizi ripoti za kushtukiza. Lakini ripoti hii ya Tume ya Madawa ya Kulevya tuipate kwa kina sana ili kupunguza hili tatizo kwa sababu hili tatizo ni kubwa, shamba halijafika maeneo mengi, limeanza Kiwengwa,

linakwenda na Matemwe, halafu litatokezea Nungwi. Kwa hivyo, hili tatizo litakuwa sio dogo.

Katika kushughulikia tatizo hili basi tungeweka vipengele vya adhabu kwamba afisa yeyote wa Polisi atakayebainika kamsamehe mtu ambaye anashughulika na madawa ya kulevya, basi mtu huyo awe kapoteza ajira yake. Kama si hivyo itakuwa bado rushwa kama walivyozungumza wenzangu inatumiwa sana kwa sababu mtu akitupiwa pesa kidogo hawezi akafanya kazi yake kwa uaminifu.

Si mtu tu, nasikia hata mbwa kwa wale wezi wanaotaka kwenda kuiba anachukua utumbo mwingi anamtupia mbwa yule mwenye kulinda ananguruma na utumbo mtu anakwenda kuiba, akirudi anamtupia tena apate kupita. Kwa hivyo, mbwa habweki wala hafanyi chochote. Mhe. Spika, sasa tuone kwamba tunakuwa makini sana.

Mhe. Spika, jengine ni makosa na adhabu. Mhe. Spika, tulijaribu sana kuona kwamba adhabu ambazo zimewekwa katika makosa ziwe kubwa, tukajaribu kuziongeza ongeza ili ziwe zinakidhi haja. Kwa mfano, kifungu cha 19 kwa mujibu wa uono wa ghafla utahisi kwamba mtu akipangiwa adhabu ya milioni 40 ni kubwa kwa mtazamo wa kawaida. Lakini katika mjadala huu watu wanahisi kwamba adhabu ya milioni 40 ni ndogo.

Mhe. Spika, napendekeza tena, kule nilipendekeza maana haikuwa milioni 40 au miaka hii hapa ambayo imeandikwa. Kwa hali ya kukomesha jambo hili, kwa wale watu ambao wameainishwa katika sehemu hii basi ni bora wakapata adhabu ile ya milioni 40 na kifungo kama kilivyoonesha hapa cha miaka 35, labda hii inaweza kidogo ikawapunguza wale watu ambao wanajishughulisha na biashara hii.

Maana hii kazi ya shughuli za madawa ya kulevya nasikia ina mikondo mitatu. Upo mkondo wa wasafirishaji tu wanatoa huko wanaleta hapa, kwa hivyo mtu kama huyu yeye milioni 40 kwake si tatizo, lakini ukimwambia umfunge siku 40 kwake yeye mtihani. Lakini wapo watu mkondo wa pili hawa ambao wanauza, huyu milioni 40 kama hutomfunga miaka hii 35 kama ile 7 tu, tayari kwanza akatumikie miaka 7 halafu akija milioni zake zile 40 kasalimika nazo, kwa hivyo mtu kama huyu ni tatizo.

Mhe. Spika, wapo watu ambao tuliona kwamba na wao wawe na adhabu kidogo hawa wanaotumia unga na ndio wengi. Sasa hawa bado mjadala upo kwa sababu unaweza ukampiga faini ya milioni 2 mpaka 10, lakini kumbe yeye alikuwa anakwenda pale kwa kutoa ule uraghba. Sasa huyu usimtazame pale kwamba yeye amekwenda kustarehe tu, inasemekana hawa ndio watu wakorofi wanakuwa wezi, mwizi ukimkuta basi sharti uwe makini.

Mhe. Spika, nilikwenda hospitali ya Mnazi Mmoja hapo kumuangalia jamaa yangu kaanguka kwenye majumba yale ya wazungu alikuwa anaezeka, lakini nimemkuta yeye bora kuliko ambaye alikuwa anapambana na mwizi. Maana kampiga kisu cha kichwa hapa jamaa fahamu hana akiamka anapiga makelele tu. Kwa hivyo, mwizi mbaya kuliko msafirishaji na huyo msafirishaji mbaya kabisa kuliko muuzaji. Kwa sababu bila ya msafirishaji hauji. Hapa ukimuacha huyu mtumiaji nae hatari maana yake hili jambo kubwa. Sasa kila mtu aone kwamba tunafanya *chain* ya kujiunga kupiga vita masuala ya madawa ya kulevya na haya si kitu rahisi sana.

Mhe. Spika, kwa kule shamba huwezi ukajua wapi yanauzwa utaona tu watu wanatokeza wanatetemeka, lakini huku yanakouzwa mnakujua tuisaidie serikali. Maana yake serikali mikono yake mingi lakini sasa mikono yenyewe imeungana na sisi, tuisaidieni serikali kupiga vita hili tusiwe na mihali. Lakini tuone tu kwamba sheria tuipitie vizuri maana humu bangi pia imo na bangi inaweza kuota kwa bahati mbaya njiani au maeneo mengine akawa mtu anatumia. Pia nayo maadam imo katika sheria hii basi tuone tunaondoa huruma.

Kwa sababu ziko nyengine zinatengenezwa, nasikia hizo saikotropiki na nyengine inaweza kuwa inakuja kitu kimoja kimoja ambacho huwezi ukakijua kwamba hii ndio dawa yenyewe hasa. Nafikiri ndio hizo alizoambiwa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk jana iligeuka kaki.

Lakini kumbe inaweza kuja dawa moja leo, nyengine ikaja kesho kutwa na siku nyengine ikaja nyengine wakawa wanatengeneza hapa ikawa imeshatimia dawa kamili. Kwa hivyo, tuwe makini sana katika haya, tusiende kwamba tunatafuta wale watu ambao tayari imeshatimia tu ile dawa. Tuone kwamba tuna wataalam wa kuona hii ikichanganywa na hii inageuka ile. Kama hatutokuwa wataalam wa hivyo zitakuja na watu watalewa zinavyokuja hatuzioni. Sijui kama nimefahamika.

Kwa hivyo, watu wanachanganyia hapa nchini sasa nasikia pana mabingwa mimi siwajui. Hawa ndio wa kuwapiga vita hasa na hawa zaidi wanasayansi, maana wanasayansi wazuri lakini wakati mwengine wabaya, anatengeneza kitu kizuri kinageuka madhara.

Mhe. Spika, humu ndani ya mswada huu nafikiri hamna kifungu kinachoonesha kwamba kama mtu kaja na dawa moja akachanganya na nyengine itakuwa dawa ya kulevya. Lakini ipo haja kielekezeni kiwepo kwamba dawa yoyote ikichanganywa na dawa nyengine ikageuka dawa ya kulevya, akikamatwa nayo basi mtu huyo mkosa. Kama si hivyo watu watatupiga chenga sana.

Mhe. Spika, jengine ni ukurasa wa 119 kifungu cha 24 mpaka 27, vifungu hivi ndio vinavyomtia mtu kwenye adhabu na faini zake ndio hizi. Lakini watu wengi sijawaona kupendekeza katika mswada huu, kwamba katika kifungu kipi kirekebishwe ama kupunguza faini au adhabu au kuongeza. Kwa sababu tulitegemea kwamba wajumbe zaidi wataingia ndani ya huu mswada kuliko yale maelezo ya jumla jumla. Kwa sababu kwa maelezo ya jumla jumla hawa maafisa wetu hawatopata cha kuongezwa na madhumuni ya kuletwa humu ni kuutungia sheria.

Katika kutunga sheria Mhe. Spika, kuna utaratibu wa kutuuliza kifungu kwa kifungu na sisi tunasema hicho kimepita. Sasa kama hatuchangii ndani ya mswada tunakwenda nje kidogo, basi vile vifungu ambavyo tunavipitisha vitakuwa havijachangiawa, havijaguswa na havina mapendekezo.

Ndio itakuja kutokea ile ya Mhe. Tafana katika sheria ya mwaka nafikiri 1996 ya mambo ya mazingira. Tukaona tu kwamba mtu kumnyang'anya gari ya milioni 5 au 6 ni kuuhamisha mchanga kutoka hapa kupeleka kwengine rahisi. Kumbe ilikuja kunikuta mimi kwa rafiki yangu. Sasa niliona tabu sana kwenda kwa Mhe. Waziri, na nilipokwenda kwa Mh. Mussa Ame wakati ule alikuwa mkali sana, akasema mimi hapa natengeneza sheria. Sasa kwa rafiki yangu hakwendeki na kwa Mh. Mussa Ame hakujiki.

Kwa hivyo, mimi nilifikiria tutatengeneza hapa kuona kwamba je, kifungu 26 kwa mfano, kinachomtia mtu hatiani akapigwa faini ya Shs. 40 milioni au kifungo cha miaka 35 tunakiafiki vipi? Kwa sababu kwa mtizamo wa ghafla faini kubwa na miaka ni mingi. Lakini tumesema kwamba kumpa adhabu hii ya miaka 35 itakuwa inasaidia kuwapunguza wale wengine wafanyabiashara wa hili. Tukasema kwa Shs. 40 milioni kwa watu ambao wanafanyabiashara hizi hata habari hawana.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba kwa kila mjumbe atakayechangia hapa katika ukurasa wa 119 aweke baraka zake, kwa sababu kuna watu wanaweza wakahusishwa na makosa kumbe hawana makosa, lakini kuna watu wakawa wanahusishwa na makosa yaliyokuwa madogo kumbe wana makosa makubwa. Kwa hivyo, ningeomba sana katika mswada huu tukaona kwamba zaidi tunatembelea katika hivi vifungu vyenyewe ili kuona kwamba wanakwenda na mswada.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 121 nilifikiria kwamba watu wanaweza kushawishika sana hasa kifungu cha 36, kifungu hiki kinataja zawadi. Zawadi Mhe.Spika, wanapewa wale watu ambao watatoa taarifa za uhakika za kuweza kuwanasa hawa watu ambao wanashughulika na haya madawa ya kulevya.

Lakini zawadi hizi hasa zitatoka kwa wale watu ambao watatoa taarifa kwa watu ambao wanasafirisha. Maana yake kwa wale watu tu wa kuwabaini kwamba hawa wameshatumia basi ingekuwa sio kazi kubwa, maana ukimuona tu yule mtumiaji basi ule mwendo wake unajua kuwa huyu keshatumia. Lakini zaidi tungependekeza kuona kwamba wale watu ambao wanasafirisha na wanatengeneza, basi wakawa wanapewa hizi zawadi ili kuona kwamba wao ndio wanaisaidia Serikali katika hili.

Kwa hivyo, kazi hii kwa kifungu hiki sio ya Serikali wazi wazi. Serikali kazi yake ni kudaiwa hiyo zawadi yenyewe. Lakini kifungu hiki ndio kinatuhusu hasa sisi jamii. Kwa hivyo, tuone kwamba kila mtu anatoa mchango wake kwa kifungu hiki.

Mhe. Spika, na kifungu hiki asifuate zawadi tu, hiki maana yake ndio nafasi ambayo inapiga vita hili tatizo ambalo tunalo, kwa sababu hapa kila mtu anakaa kwao. Mimi nakaa Matemwe, sio wengi ambao hawakai jimboni, wengi wanakaa maeneo hayo na tunawajua hawa watu, wengine rafiki zetu na wengine wana wafadhili hawa watu wa majimbo. Wanawafadhili mipira na mambo mengine. Lakini mwenye kufadhili kwa hili basi huo ufadhili aliofadhiliwa hauna maana kuliko kutoa taarifa ya tatizo hili na hii haikuja leo tu.

Mhe. Spika, kuna aya nimeisahau inasema '*msiuze uongofu kwa upotofu'*. Kwa hivyo wewe kupokea msaada kwa mtu huyu ambaye anaua jamii ambayo inakuhusu ukaona ule msaada ni bora kuliko kumtolea taarifa akaondoa lile tatizo, basi utakuwa umeingia katika aya hii. Nafikiri wazee wakija hapa kuchangia hiyo aya wataniambia iko wapi na ni sura gani?

Mhe. Spika, katika hali ya kawaida binadamu huogopa asijulikane na ni kweli, kama alivyosema alivyosema Mhe. Mshiba. Lakini katika ukurasa wa 122 kifungu cha 37(1) kinasema namna utakavyolindwa utakapotoa taarifa. Inaonekana hapa tutalindwa, lakini tunaaminiana katika haya, kwa sababu tunajua hapa Zanzibar tuna tatizo, hata sisi tuliokula kiapo. Utakula kiapo kwamba nitaitetea Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Jamhuri ya Muungano, basi jambo halijatoka unaanza kulisikia huko na ndio unaitetea katiba.

Kwa hivyo, na hapa katika kutetea basi unayatetea maisha ya mtu yule ambaye kakupa taarifa. Kwa hivyo, hapa tuwe makini kweli kweli. Ningeomba kwamba mtu ambaye katoa taarifa sio taarifa hii iliyokusudiwa, katoa taarifa kwa mtoa taarifa. Maana yake nafikiri kipengele hiki hatukukifanyia marekebisho, kwamba mtu katoa taarifa kwa nia nzuri juu ya mtu ambaye ana madawa ya kulevya, lakini akatokea mtu mwengine akamtolea taarifa kwa yule aliyetolewa taarifa. Hili Mhe. Spika, ni tatizo kubwa je, tutamlindaje? Lazima tuone

kwamba tunamlinda na yeye ili tuone kwamba ile faini ambayo atapigwa huyu mtoa taarifa mbaya kwa mtoa taarifa mwenye nia nzuri, basi yeye ilikuwa adhabu yake iwe kubwa zaidi kuliko hiyo.

Baada ya hayo Mhe. Spika, mimi nilikuwa mjumbe wa kamati hii na *Alhamdulillah* kwa wakati huo wa kupitisha, sio sasa hivi, sasa hivi sio mjumbe, sasa hivi ni mjumbe tu katika hali ya kawaida. Ningewaomba sana wajumbe wenzangu watakapochangia kwamba zaidi watembee juu ya huu mswada, ili hivivifungu vipate baraka. Kwa sababu kwa mazungumzo ya jumla jumla sote tunajua kwamba madawa ya kulevya ni tatizo kubwa. Madhara yake tunayaona, kama alivyosema Mhe. Tafana wengine wanawaibia baba zao, wengine wanawaharibia mali ndugu zao na wengine wanatishia maisha ya watu.

Kwa hivyo, tukiyapendekeza yale mambo ambayo wataalamu wetu wameyaleta hapa, basi ingekuwa raha zaidi na Mhe. Waziri angekuwa na maelezo mengi zaidi ya kufafanua. Kuliko kuwa tunapita juu juu kwa jumla jumla itakuwa hatueleweki vizuri katika kuchangia mswada huu, tutaonekana kwamba hatujaupitia na tutaonekana kwamba tukifika hapa tunanyanyuka na kubakwa bakwa ili kuona kwamba tuhami wakati, lakini sio malengo. Malengo yetu ni kuvipitia vifungu, tukavizungumza na baadae Mhe. Spika, akatuweka katika kamati ya matumizi tukawa tunavipitisha vifungu ambavyo tumeviridhia sisi wenyewe. Baada ya hayo Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Matemwe, kwa kupiga vita hali hii ya hatari tunaunga mkono mia kwa mia, nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ile kamati kwa miswada inaitwa Kamati ya Baraza Zima.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nikazungumza machache kuhusu huu mswada uliopo mbele yetu wa mapambano dhidi ya madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, mimi nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuona umuhimu wa waheshimiwa, kile kilio ambacho siku zote tunakizungumza, suala la mapambano dhidi ya madawa ya kulevya na namna vijana wetu wanavyoathirika katika majimbo yetu, baada ya kuona waheshimiwa wa pande zote mbili wakililia suala hili. Mhe. Waziri ametuletea mswada ambao unasaidia kuboresha ni namna gani tunaweza tukapiga vita na tukaweza kuzuia haya madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, kwa kweli suala hili sio jepesi. Suala hili nadhani kama tumeuangalia mswada unaeleza kwamba kuna mikakati ya kimataifa mbali mbali, kuna *convention* za kimataifa ambazo zimeanza kuridhiwa tokea mwaka

1961 huko Newyork. Kuna makongamano mbali mbali ya kimataifa yameendelea mwaka 1971 hadi mwaka 1972.

Vile vile katika mwaka 1988 kule Vienna Austria kulikuwa kuna *convention* nyengine inayoboresha namna gani mataifa yaweze kushirikiana kupambana na biashara hii haramu ya madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, kwa Zanzibar biashara hii ya madawa ya kulevya imeanza kushamiri hasa baada ya kufungua milango ya biashara. Mhe. Spika, tukiangalia suala zima la madawa ya kulevya linatokana zaidi na uhuru wa uingiaji na utokaji katika nchi mbali mbali duniani. Kwa hivyo, suala la mapambano dhidi ya madawa ya kulevya haliko Zanzibar peke yake. Suala la madawa ya kulevya liko dunia nzima na ndio maana mataifa yakakaa na kuumiza vichwa na kuweka mikutano mikubwa ya kuweka mikakati ya namna gani ya kuweza kushirikiana dunia nzima kulipiga vita suala hili.

Mhe. Spika, kila nchi na utaratibu wake wa namna ya kupambana na madawa ya kulevya. Kuna nchi za Kiarabu ukikamatwa na madawa ya kulevya basi huonekani tena, kwa sababu wameamua kabisa kwamba hili suala hawataki kuliona katika nchi zao. Ingawa sasa hivi katika dunia kuna sindikizo la kupiga vita adhabu ya vifo, lakini bado kuna nchi ambazo tumeshuhudia katika miaka ya hivi karibuni yale mambo ambayo hawataki kuyaona yanaendelea katika dunia au katika nchi zao, basi kuna hatua kama hizi zinachukuliwa.

Kwa hivyo, ndio maana tukawa tunasema kwamba suala hili ni vizuri tukaliwekea adhabu kali, ili kwamba badala ya mtu kumnyonga au kumtoa shingo, basi ile adhabumbadala iwe nusu ya kule kumnyonga. Kwa sababu sehemu nyingi duniani hukumu ya kifo hazijafutwa katika nchi zao. Lakini tatizo linakuja katika utekelezaji wa ile hukufu ya kifo, kwa hivyo ndio maana watu wanaachwa rupango mpaka umri wake unamalizika huko huko kwa kukimbia ile moja kwa moja kuitoa roho ya mtu kwa mara moja. Kuna baadhi ya nchi kama nilivyosema masuala haya wao wameshaamulia kabisa, ukiingia nayo hayo, basi ujuwe tena ndio mwisho wako.

Hii Mhe. Spika, imesaidia sana nchi zile kuwa na tatizo la madawa ya kulevya, kwa sababu mtu akijua kwamba fulani amekamatwa, hamuoni tena basi na yeye inakuwa hafanyi labda awe jasiri kweli kweli kwamba awe keshaamua tena yeye hata akifa basi potelea mbali.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, suala hili la madawa haya ya kulevya sio suala dogo, hii ni vita na vita inapoingia katika nchi kama alivyosema Mhe. Ame Mati haichagui Sheikh wala padri. Vita ikiingia katika nchi aliyekuwa kakaa upande kidigo basi inampiga mwereka. Kwa hivyo, ndio maana nikasema vita,

ukiangalia wenzangu wamezungumza kwamba katika familia zetu basi ni koo chache ambazo utazikuta bado hawajaguswa na mtu ambaye hajaathirika na madawa ya kulevya. Miongoni mwetu wengine ndani ya majumba yao wanakaa na watu ambao tayari wameshaathirika.

Sasa vita hii ukitaka uijuwe hasa uchungu wake, basi ndani ya familia yake mtu awe na mtu wa madawa ya kulevya. Kwa sababu Mhe. Spika, kijana akiathirika na madawa haya basi tena huesabu kama ndani ya nyumba una mtoto isipokuwa una mzigo na mzigo wenyewe unakuwa ule ambao hauna cheti, kwa sababu mzigo uliokuwa hauna cheti wewe mwenyewe kila wakati unaangalia huku na huku hujui nini kitatokezea, hujui kama utakamatwa na polisi au vipi.

Mhe. Spika, suala la madawa ya kulevya mapambano haya tusaidiane sana katika maeneo yetu zaidi katika kutoa taarifa. Mhe. Spika, pamoja na malalamiko mengi ambayo yanatolewa kuhusu suala la madawa ya kulevya namna gani kesi zinavyoendeshwa. Lakini vile vile na taarifa zinakuwa tabu kweli kweli. Kwa sababu kuna watu wengine ile kutaja kwamba fulani anahusika na madawa ya kulevya basi inakuwa ni vigumu kweli kweli.

Mhe. Spika, waheshimiwa baadhi yao wamezungumza kwamba angalau kungekuwa kuna sehemu ambayo wananchi wanapeleka taarifa. Suala hili Mhe. Spika, tutalifanyia kazi, ziko njia nyingi tunaweza tukatafuta mtandao na tukatoa namba na wala hatutokuambieni namba ile anaipokea nani. Namba ile itakuwa haipigwi ila inatumwa ujumbe tu. Tunaweza hata tukatoa na Email ikawa tunasoma taarifa kwamba fulani na fulani wanahusika. Kwa hivyo, kitengo chetu kitakuwa na kazi nyepesi kweli kweli, lakini tukiwa tunasema tu kwamba wapo tunawajua, sasa wapo tunawajua bado, kwa sababu lazima tupate pale pahala pakuanzia.

Mhe. Spika, ni lazima tukubali madawa ya kulevya ukiangalia katika mazingira yetu ya Unguja na Pemba, udhibiti wake kuingia ni mgumu kweli kweli. Mhe. Spika, sio wengi wenye kupita na madawa ya kulevya Airport, watakaopita Airport zaidi ni wale wanaobeba tumboni. Lakini wale wenye mizigo mizito mizito Mhe. Spika, kwa sababu katika viwanja vyetu vya ndege sasa hivi ulinzi uko mzuri kweli kweli. Katika suala ambalo tumejitahidi katika viwanja vyetu vya ndege basi suala la uingizwaji wa madawa ya kulevya mimi nathubutu kusema kwamba asilimia kubwa ya madawa yanayoingia hapa nchini basi hayapiti uwanja wa ndege, hao wachache wanaopita tayari ndio hao ambao tunawa-*screen* na tunawatoa ndani ya matumbo yao.

Kwa hivyo, tuna panya *road* nyingi Mhe. Spika, kuna bandari bubu, kuna watu wanasafirisha ng'ombe huko wanapita Kisakasaka, kuna wengine wanapita kwenye bandari mbali mbali, kuna bandari ya Mkokotoni pale hakuna *screen*,

hakuna mbwa wala hakuna chochote na mbwa tutakuwa nao wangapi. Kwa hivyo, ni kazi kubwa kweli kweli.

Mhe. Spika, kitu cha kufanya sisi kuweza kujua, hata kama mtu anaingia kwa njia yoyote anayoijua yeye, lakini tukipata taarifa kuwa fulani ndiye anayejihusisha na biashara ya madawa ya kulevya, basi hiyo kazi kwetu inakuwa ni nyepesi kweli kweli.

Kuna mheshimiwa mmoja alizungumza kwamba mtu akikamatwa basi afilisiwe na mali yake. Mhe. Spika, tunayosheria, tumepata semina kidogo. Tunayo sheria ya *money laundry*, moja katika madhumuni ya sheria hii ya *money laundry* ni kwamba tukimkamata mtu anafanya shughuli ya madawa ya kulevya na tukipata uthibitisho ina maana biashara zake mtaji wake ni ule, kwa hivyo kabla hajapeleka mtaji wake katika londry kusafisha ili ziwe sawa sawa basi na sheria ile vile vile ina *a play* katika suala hili la madawa ya kulevya.

Lakini bado narudia tena Mhe. Spika, nadhani hili baadae Mhe. Waziri atakapokuja kutoa ufafanuzi, atatoa taarifa au kauli ya serikali katika suala hili, kwa sababu sisi linatuuma sana tena sana. Kwa wananchi wa kawaida huko waliokuwa hawajui wanasema aah!hii biashara ya wakubwa kwa kuwa wao wakubwa wanafanya wao ndio maana watu hawakamatwi, lakini mkubwa gani jamani, kuna mkubwa gani atakayependa watu anaowaongoza waathirike. Leo kweli atakuwemo mheshimiwa humu ndani ya Baraza awe kweli anafanya biashara ya madawa ya kulevya, sasa hao wananchi wake ndio atawaongoza vipi. Yeye anawategemea wananchi waje wamchaguwe, halafu wananchi wale unawatoa akili. Mimi nafikiri sio rahisi suala hili.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, sisi tutafanya utaratibu ili tuweze kupata taarifa. Tukishapata taarifa kwamba fulani anafanya biashara hizo basi atakuwa hana raha. Kwa sababu akiamka tunaye, akenda sokoni tunaye na atakapokwenda popote tunaye. Sasa huyu tutaangalia namna gani tutaweza kum-*monitor* mpaka tukaweza kumkamata basi tutaweza kupunguza kwa kiasi fulani. Kwa sababu mtu akishajua anafuatwa fuatwa Mhe. Spika, ataacha.

Lakini Mhe. Spika, kama nilivyosema kwa kutegemea tu mbwa pale *airport* na kwengineko, hili zoezi la kuzuia uingizwaji wa madawa ya kulevya litakuwa gumu kweli kweli.

Mhe.Spika, suala hii hata nitaomba sana ndugu zetu wa viwanja vya ndege, pamoja na kuwa nimesema kwamba asilimia kubwa ya madawa yanayoingizwa katika nchi yetu hayapiti katika viwanja ya ndege, lakini bado tuwe na matumizi mazuri ya viwanja vyetu vya ndege.

Mhe. Spika, kuna watu wanapita VIP hawastahili na kuna wakati watendaji wetu wanapokuwa wanataka kuwasachi inakuwa mbinde kweli kweli. Kwa hivyo, hili hatukubaliani nalo. Kwa hivyo, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi nafikiri yupo tutazidi kuzungumza, lakini katika suala zima la matumizi ya VIP ni lazima tuwe makini sana.

Mhe. Spika, hata VIP yetu utaratibu tunaoutumia pia hauko sawa. Kwa sababu unaposafiri pale ndio unaingizwa katika *screen*, lakini unaporudi unapita tu. Sasa unaposafiri bado kama ulikuwa unamzigo angalau unatusaidia unaukumbiza, sithubutu kusema kwamba tupitishe *airport* kwamba unatusaidia kuukimbiza, hapana. Lakini unapokuja sasa pale kama kuna kitu cha hatari ndio unakiiingiza nchini. Ndio maana nikasema hata matumizi yetu ya VIP tunahitaji kuyaangalia upya.

Mhe. Spika, ukipita pale mlango kile kifaa kinalia ‘chwiiii’ kama unakitu cha chuma na mzigo wako unaupitisha katika *screen*, *screen* zetu zile zimeboreshwa kwamba kama una mzigo wowote wa hatari, madawa ya kulevya au silaha basi pale katika *screen* ni lazima itaonekana. Lakini unapoingia sasa hupitishwi katika *screen*, kwa hivyo ina maana kama unakuja unamzigo wako unapita tu. Kuna wengine kwa kuwa mheshimiwa rafiki yake au shemegi yake tu mheshimiwa sasa yeye tena ndio anaitumia fursa ile pale, akihojiwa anakuwa mkali kweli kweli. Kwa hivyo, suala hili nilikuwa nawaomba ndugu zangu ambao tuliowakabidhi dhamana katika viwanja vya ndege basi ni vizuri wakatekeleza vizuri ule wajibu wao.

Mhe. Spika, ukiangalia katika maeneo mengi. Kwa mfano, tuna magendo hapa ya karafuu, kwa hivyo yale yale magendo ya karafuu vile vyombo ambavyo vinatoa karafuu kupeleka nje ya Zanzibar basi ndio vyombo vile vile vinaweza kutumiwa wakachukua madawa ya kulevya wakaingiza nchini. Kwa sababu biashara ya haramu inazaa haramu vile vile. Kwa hivyo, ndio maana nikasema kwamba tuna kazi kubwa sana.

Vile vile Mhe. Spika, katika sheria hii tumeeleza kuna mfuko ambao utakaochangia kupatikana mapato kwa ajili ya mapambano haya ya madawa ya kulevya. Mhe. Spika, katika eneo hili tuna mtihani mkubwa sana. Kwa sababu kwanza chombo kikubwa ambacho kinafanya kazi kubwa ya kupambana na madawa ya kulevya ni Jeshi la Polisi. Kwa hivyo, ni lazima tujitahidi katika huu mfuko basi kitu cha mwanzo tutakachokifanya kuboresha vile vitendea kazi tulivyokuwa navyo, tunajitahidi lakini bado uwezo wao wa kuweza kufuatalia, uwezo wao wa kuwawezesha kufika katika maeneo unakuwa mgumu kweli kweli.

Mhe. Spika, kuna kipindi tuliwahi kufanya *operation*, lakini *operation* nyengine hata uwezo wa vyombo vyetu unakuwa tatizo. Kuna meli inakuja haiko Tanzania wala haiko Kenya na meli ambayo iko nje ya mipaka yako huwezi ukaifuata. Kuna meli zinakuja kwenye ukanda baina ya Mombasa na ukanda wa Zanzibar, yaani baina ya Mombasa na kisiwa cha Pemba. Wakati mwengine mnapotaka kujaribu sasa muzifuate, kule sio kwenu. Lakini utakuta kuna baadhi ya viboti vyengine havitoki huku, lakini kuna viboti vyengine vinaonekana, kwa sababu wavuvi kwa bahati nzuri wanatupa sana taarifa, wanatuambiwa waheshimiwa kuna meli tumeikuta nje, kuna meli nyengine zinakwenda ubavuni, sasa kule mnaanza kujiuliza wanateremsha kitu gani. Ndio maana nikasema hizi biashara zinakuwa ngumu kweli kweli.

Mhe. Spika, katika *operation* ambayo imefanywa hivi karibuni ambayo na hiyo basi tulipata mashirikiano na Jeshi la Afrika Kusini pamoja na Kenya tukashirikiana na Tanzania. Matokeo yake tukakamata hiyo meli ya samaki. Lakini moja katika hofu mbayo iliyokuwa inafikiriwa ni hayo madawa ya kulevya, kwa sababu inaonekana meli inakaa kule wiki nzima. Meli haina kibali, haina chochote wala hakuna taarifa SMZ wala hakuna taarifa SMT.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, hizi shughuli za madawa ya kulevya ni lazima wananchi ndio watu pekee watakaoweza kutoa taarifa, kwa sababu wananchi tunawajua na tunakaa nao, hao watu ambao wanazifanya hizo shughuli kuna waheshimiwa wanasema wanawajua. Sisi wakituambia nani anafanya hizo shughuli tutashukuru sana, lakini hii kazi ni ngumu sana.

Mhe. Spika, sasa hivi haya madawa ya kulevya huku kwetu ndio kwanza yameanza, lakini katika nchi za wenzetu tokea walikuwa wanatunga sheria kama hizi kila siku walikuwa wanabadilisha. Mwisho sasa ikawa kwamba mtu anayegundulikana anashughulika na madawa ya kulevya wala hapelekwi mahakamani. Marekani madawa ya kulevya hupelekwi mahakamani, unachukuliwa unawekwa katika sehemu mabayo wanaijua wao. Nakumbuka kuna Rais fulani alikuwa akiitwa Noriega kama sikosei, alikwenda kuchukuliwa nchini kwake, kwa sababu alikuwa anajulikana kwamba nchi yake yeye mwenyewe kiongozi wa nchi ndio chanzo kikubwa cha madawa ya kulevya, ndio hayo tuliyokuwa tukizungumza nafikiri Colombia kama sikosei ilikuwa nchi yake, kwenye *charter* baada ya rubani na msaidizi wake, mzigo wote ni unga, unaikuta ndege inaanguka basi huo moshi wake wewe ukikaribia kufika taaban. Kwa hivyo, tujuwe kwamba haya mapambano ya madawa ya kulevya hayakuanza leo.

Mhe. Spika, kuna meli zinakamatwa na shehena za madawa ya kulevya, sio hawa wanaokuja na vikontena ndani ya tumbo hapa kwetu, kuna watu na mashehena. Kwa hivyo, Mhe.Spika, watu hawa wana cheni kubwa sana. Kuna

mheshimiwa mmoja alizungumza hapa kwamba cheni ya watu hawa mpaka ukaweza kuivunja una kazi kubwa kweli kweli.

Mhe. Spika, watu wana uwezo wa kusafirisha madawa kwa meli, sasa hao mawakala wao unafikiri, ndio maana nikasema hata hizi mahakama zetu zina kazi kweli kweli, kwa sababu nyinyi mmemkamata hapa basi bosi wake keshapata taarifa Marekani au Pakistani, kwamba yule wakala wangu sasa hivi tayari yuko ndani, kwa hivyo na yeye huko ana mawakala wake wengi. Unaweza kukuta watu wanafanya shughuli zao za biashara lakini cheni yao ni moja. Hiyo milioni 20 au milioni 40 tuliyosema sisi ni kubwa, hii bwana kwa watu wa madawa ya kulevya ni pesa ndogo kweli kweli. Kwa sababu yeye haoni tabu yule mtu wake kumtoa kwa milioni 40, kwa sababu kesho asubuhi anamtengenezea milioni 80 au milioni 100. Kwa hivyo kwa kweli tuna kazi kubwa sana.

Mhe. Spika, mimi kitu ninachokiomba zaidi sisi, sasa hivi tumeshakuja tunaboresha sheria zetu, vile vikwazo vya kwamba mtu akipatikana na kishwea, ni lazima aende kwenye mahakama kuu na mahakama kuu tunajua kule, kesi za mahakama kuu sio kama katika Mahakama za kawaida, kwa sababu kesi zinakuwa nyingi mpaka kuwapata hao maafisa na kesi kama ile kwanza lazima iende, yaani itajwe, halafu watu waende tena, warudi, matokeo yake pamoja na ushahidi wakati mwengine inakuwa mlolongo mrefu.

Mhe. Spika, sasa haya ndio maana sheria hii ikaletwa kwa ajili ya kupunguza ule mlolongo wa yale masharti. Ili mtu atiwe ndani ya hatia, ndio maana hivi sasa kuna baadhi ya kesi zitahukumiwa katika ngazi ya Mahakama za Mikoa. Kwa hivyo, ni kitu ambacho nadhani tujitahidini sana na zaidi kuhusiana na suala hili tushirikiane na watendaji wetu, yaani uaminifu pamoja na uadilifu.

Mhe. Spika, kwa mfano ukipewa kazi ya madawa ya kulevya kama roho yako nyepesi baada ya wiki kama ulikuwa unapandia baskeli, basi huanzi na honda, isipokuwa utaanza na *benz*, yaani kama moyo wako utakuwa mwepesi.

Ndio maana tukasema kwamba kazi hii inatakiwa zaidi na uzalendo, nia njema, vile vile kama alivyotoa mfano Mhe. Ame Mati Wadi. Na kwa kweli ule mfano wake nimeusahau kwa sababu alinukuu kwenye aya. Lakini tusione kwamba labda ile kupokea hidaya, ambayo pengine itakusaidia wewe, kumbe vile hidaya ile ikawa inakuja kuangamiza watu wengine.

Kwa hivyo, Mhe. Spika wenzangu wamezungumza kwamba mbwa tuliyekuwa naye amekufa kutokana na kazi kubwa ambayo tuliyokuwa tukimpachika, kwa sababu kazi ya kunusa madawa yale halafu baadaye na wewe yanaweza

kukuathiri. Kwa kweli mbwa wale ni thamani kubwa sana, yaani wana gharama kubwa sana.

Mhe. Spika, hivi sasa Jeshi la Polisi linafanya utaratibu wa kuwasiliana na wenzetu wa Afrika ya Kusini kuweza kutupatia mbwa wengine. Kwa sababu suala lile mbwa anayo asilimia 90 kugundua madawa ya kulevya kuliko binadam wa kawaida. Kwa maana hiyo, mbwa walikuwa wanatusaidia sana katika kutafuta haya madawa ya kulevya.

Lakini kimsingi Serikali kwa upande wetu kwa hali tuliyonayo tunajitahidi sana katika kuhakikisha kwamba tunapambana na haya madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, kuna baadhi ya mambo ambayo wakati mwengine tunakuwa tunayatunga sisi wenyewe. Lakini kama nilivyosema kwamba kuna *convention* za kimataifa ambazo kila baada ya muda zinakuwa zinakuja. Kwa hiyo, *convention* hizi tunatakiwa na sisi kudhiridhia.

Sasa changamoto ambayo tunayo moja katika kupitisha hizi sheria za madawa ya kulevya, kuna baadhi ya mambo lazima tushirikiane na mataifa na tumeshirikiana vizuri tulipopitisha. Kwa sababu kuna baadhi ya watu ambao tunaowakamata Mhe. Spika, tunapata taarifa moja kwa moja kutoka *Interpol*, yaani tokea huko na hii inatokana na watu kutoa taarifa.

Kwa hivyo, yule mtu tokea kule anakotoka anajulikana huyu shughuli zake ni hizi basi anatafutwe ile njia anayotoka. Kwa mfano, hivi sasa kama *Passport* yako itakuwa imegongwa Muhuri wa Pakistan utapata tabu kweli viwanja vya ndege, yaani ile *Passport* yako kwanza itabidi wajiulize huyu *Pakistan* amekwenda kufanya nini au shughuli gani, yaani huo muhuri mmoja utakupatisha tabu kweli.

Kwa hiyo, taarifa hizi sio kama kila anayekamatwa pale kwamba tunamkamata kwa kuweza kumjua sisi wenyewe. Lakini ndio kama hivyo kuna taarifa ambazo zinazopatikana kupitia vyombo mbali mbali mpaka baadaye ndipo tunaposhirikiana na sisi na kuweza kukamata. Mhe. Spika, baada ya kukamata na wale wenzetu wa *Interpol* wanafuatilia, yaani baada ya ile kesi kuikamata kuna jitihada gani ambazo tunazoweza kuchukua.

Sasa ndio maana tunasema kwamba wakati mwengine hizi kesi tunapozikamata mlolongo unapokuwa mrefu mpaka ile kesi inaonekana kwamba haina ushahidi, basi hata wale wenzetu wanaotupa taarifa tunawavunja moyo. Mhe. Spika, mambo kama haya kama tulivyosema kwamba kama kazi mtaifanya vizuri, basi kuna baadhi ya misaada mnakuwa mnaipata kwa ajili ya mapambano ya haya masuala ya madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, ndio maana niliposema kwamba uaminifu pamoja na uadilifu kwa watendaji wetu, ambao tumewakabidhi hizi dhamana za kuweza kushughulikia masuala haya, ndizo zitakazoweza kutusaidia katika kupata nguvu ya kuweza kupambana na haya madawa ya kulevya.

Nadhani pamoja na kwamba Waheshimiwa Wajumbe kusema bado tunakamata vidagaa, lakini wale wakubwa au wahusika hasa hatujawakamata. Mhe. Spika, kama nilivyosema taarifa ndiyo inayoweza kutusaidia.

Lakini kama wale madagaa hatujawakamata hali hii itazidi kuwa mbaya. Kwa sababu tumejaribu kufuatilia ukiwakamata wale wasambazaji ndio kama hivyo ingawa baadaye watatoka kutokana na mapungufu ya sheria zetu, lakini hata ile hali kidogo unahisi inautulivu kiasi fulani, yaani kwa kile kipindi ambacho mnachofanya *operation*.

Mhe. Spika, hizi *operation* zina gharama kubwa, kama vile kazi ya doria pamoja na kufuatilia na wakati mwengine tunakuwa na matatizo ya magari. Kwa hivyo, kama hatukuwakamata hawa madagaa wadogo wadogo, nadhani hivi sasa baada ya kupitisha hii na kuanza kupata taarifa, basi pengine haitochukua muda mrefu tutasikia hayo mapapa yataanza kunasa.

Kwa hivyo, yatakapoanza kunasa hayo na wala hatutaki kusema kwamba tutakuwa tunaingilia uhuru wa mamlaka nyengine. Lakini Serikali tutakuwa tupo karibu sana kuona kwamba je hizi kesi zitakuwa zinafuatiliwa vipi.

Mhe. Spika, nakumbuka katika miaka ya nyuma kuna jamaa fulani walikamatwa na madawa ya kulevya kutoka Asia, yaani Wahindi, basi ile kesi inaahirishwa Mahakamani, kuna ndege tayari kama ilikuwa ikiwasubiri. Kwa sababu wale baada ya kukamatwa Jeshi la Polisi na hata ile sheria ilikuwa bado haijabadilishwa. Kwa sababu Jeshi la Polisi kazi yake ilikuwa ni kukamata na halafu inakwenda kwa *DPP* na wao ndio wanaosimamia, yaani Jeshi la Polisi ilikuwa wao ndio wanaokamata pamoja na kusimamia kesi.

Kutokana na hali ile basi jinsi walivyokasirika baada ya kujua kesi imekuwa *dismiss* walitaka kumkamata. Wapi? waliambiwa tayari ameshakimbia. Mhe. Spika, ndio maana tukasema kwamba suala hili la madawa ya kulevya ni shughuli pevu kweli, yaani yule mtu alipotoka Mahakamani basi moja kwa moja *Airport* na kwa kuwa si raia wa Tanzania ina maana alitoka.

Mhe. Spika, ndio maana tukasema kwamba sheria yetu pamoja na askari wetu ambao tumewapa dhamana ya kukamata, hivyo vidagaa wanavyovikamata tusiwavunje moyo, kwa sababu tukiwavunja moyo ndio wanakuja kututokea

udenda chini ya mlango. Kwa sababu kama tunavyowajua watu hawa wakeshaanza shughuli zao basi udenda moja kwa moja.

Mhe. Spika, kwa mfano na humu katika sheria limo eneo ambalo la kuwarejesha katika hali zao. Lakini tunajaribu kutafuta fedha Mhe. Spika, kwa ajili ya kupata ufadhili wa kujenga lile jengo ambalo la kuwahifadhi wale, ili kuwarejesha katika hali zao. Kwa kweli tumehangaika sana bado hakuna *donors* yeyote aliyetu-*support*.

Kwa hivyo, tunasema bado Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tutajitahidi hivyo hivyo na tutajenga jengo ambalo tutakuwa tunawachukua wale vijana waliokwisha kuathirika na kuwarejesha katika hali zao. Mhe. Spika, kazi hii ni ngumu tena yenye gharama kubwa sana.

Kwa sababu mtu ambaye ameathirika na madawa ya kulevya kuna wengine wanasema wanakwenda kubadilishwa damu, lakini mtu yule anatakiwa katika kumrejeshe hali ya kawaida lazima aupate tena ule unga. Kwa mfano, unapomkamata na kusema humpi tena basi anaweza kufa.

Mhe. Spika, wakati tulipofanya *operation* Siku Kuu iliyopita tuliwaweka pale Madema, basi utafikiri kuna kipindupindu, yaani kule rumande jinsi wanavyoharisha tena wanasema hasa nipatie kidogo na kama hujampatia basi anaweza kwenda.

Kwa bahati nzuri wale askari wetu wamesomea haya masuala ya madawa ya kulevya pamoja na namna ya matibabu yake pia wamesomea. Kwa hivyo, yale waliyokamatwa nayo inabidi wapatiwe *dose* vyenginevyo unaweza kumkosa, akifa kule polisi *Allahhuakbar* huyo mama yake atasema kwamba mwanangu wamemuua.

Mhe. Spika, ndio maana anapoamka yule kama hajapata, basi suti ambayo unayotaka kuvaa kwa ajili ya kuja Barazani atakapoiona ataichukua na kwenda kuiuza wakati huo huo, yaani wewe mwenyewe unakoga basi yeye tayari suti ameshaichukua na kwenda kuiuza. Kwa sababu ataanza kutetemeka na mwili wake hajisiki, yaani anajihisi kama anataka kufa, kwa kweli ni kazi ngumu.

Sasa ile *dose* ya kumrejesha yule ya mwezi mmoja ni shilingi 400,000/- na mtu yule unatakiwa ukae naye si chini ya miezi mitatu mpaka sita, kwa ajili ya kumrejesha katika hali yake ya kawaida. Kwa hivyo, hata tukijenga lile jengo la kuwarejesha katika hali zao za kawaida, bado kuna mzigo mkubwa ambao Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii itakuwa na kazi ya kupata hiyo *dose* ya kuwarejesha wale, hivi sasa tukiangalia wako wangapi?

Kwa mfano, hivi sasa kama Mhe. Spika utatoka na gari yako basi Miembeni unaweza kuwachukua kama 100, Kundemba pia 100, tukija Mji Mkongwe ndio wote umeshawachukua, kwangu pale Mikunguni alimradi ni kazi ngumu kweli. Mhe. Spika, kituo hiki sijui kitakuwa na ukubwa gani, lakini kazi kubwa tunayo.

Sasa Mhe. Spika, kazi hii si ndogo na wala sio kubwa isipokuwa tunatakiwa sisi kama serikali tuingize nguvu zetu zote, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapambana na vita hivi.

Mhe. Spika, narejea tena kwamba tukiweza kupata taarifa na sisi kama mtu atajiamini, kwa sababu watu wengine wanaogopa kuambiwa kuwa wao ndio waliotoa taarifa. Lakini tunawahakikishia kuwa tukipata taarifa hasa mtu huyu ndiye anayeshughulika na madawa ya kulevya, basi tunakuhakikishieni kama ameshaleta basi hamalizi kuuza tutamkamata na ikiwa hajaleta basi tutamkamata ndani ya mwezi mmoja, kwa sababu itakuwa ndio kazi yetu.

Kwa kweli tutampa askari na ndio maana Mhe. Mjumbe mmoja alisema kwamba hii ni kazi kubwa sana. Kwa mfano, wenzetu Tanzania Bara walipounda ile Kurugenzi yao ya kupambana na haya madawa ya kulevya Mhe. Spika, hiyo mishahara yao si ya kawaida. Vile vile tukiacha ule mshahara kuna posho maalum ya kununua taarifa, sasa kazi hii ni kubwa kweli.

Mhe. Spika, pia wenzetu Tanzania Bara sheria yao wameangalia Afrika ya Kusini, Namibia pamoja na nchi nyengine. Kwa kweli yule Kamishna ambaye anasimamia kile Kitengo cha Madawa ya Kulevya, basi kama yale marupurupu ya viongozi wa kitaifa, kwanza anatakiwa apatiwe gari mpya, nyumba, ulinzi, yaani kazi kubwa. Kwa hivyo, ndio maana tukasema kwamba suala la madawa ya kulevya mapambano yake ni kazi kubwa yenye kuhitaji gharama nyingi sana, lakini zaidi ni mashirikiano makubwa tukiyapata kwa wananchi, basi naamini tutaweza kufanyakazi vizuri.

Baada ya hayo machache na mimi sikuingia moja kwa moja kwenye mswada, lakini nilikuwa nikijaribu kutoa namna gani shughuli hii ilivyongumu, isipokuwa tuwape moyo vijana wetu hasa askari katika kuhakikisha kwamba mapambano haya tunayasaidia nguvu, ili tuweze kuokoa vijana wetu.

Mhe. Spika, baada ya hayo mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja *(Makofi)*.

Ahsante sana.

(*Saa 1:45 usiku Kikao kiliakhirishwa hadi tarehe 23/10/2009 saa 3:00 asubuhi*)